**5 SEPTEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Sita – Tarehe 5 Septemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake yaliyochapishwa tangu Mkutano wa Bunge uliopita kama ifuatavyo:-

1. Toleo Na.14 la tarehe 07 Aprili, 2023;
2. Toleo Na.15 la tarehe 14 Aprili, 2023;
3. Toleo Na.16 la tarehe 21 Aprili, 2023;
4. Toleo Na.17 la tarehe 28 Aprili, 2023;
5. Toleo Na.18 la tarehe 05 Mei, 2023;
6. Toleo Na.19 la tarehe 12 Mei, 2023;
7. Toleo Na. 20 la tarehe 19 Mei, 2023;

8. Toleo Na. 21 la tarehe 26 Mei, 2023;
9. Toleo Na. 22 la tarehe 02 Juni, 2023.
10. Toleo Na. 23 la tarehe 09 Juni, 2023;
11. Toleo Na. 24 la tarehe 16 Juni, 2023;
12. Toleo Na. 25 la tarehe 23 Juni, 2023;
13. Toleo Na. 26 la tarehe 30 Juni, 2023;
14. Toleo Na. 27 la tarehe 07 Julai, 2023;
15. Toleo Na. 28 la tarehe 14 Julai, 2023;
16. Toleo Na. 29 la tarehe 21 Julai, 2023;
17. Toleo Na. 30 la tarehe 28 Julai, 2023;
18. Toleo Na. 31 la tarehe 04 Agosti, 2023;
19. Toleo Na. 32 la tarehe 11 Agosti, 2023;
20. Toleo Na. 33 la tarehe 18 Agosti, 2023;
21. Toleo Na. 34 la tarehe 25 Agosti, 2023; na
22. Toleo Na. 35 la tarehe 01 Septemba, 2023.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**:

Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Taarifa ya Majumuisho ya Majibu ya Serikali na Mpangokazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):**

Taarifa ya Majumuisho ya Majibu ya Serikali na Mpangokazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali.

Na. 74

**Mafunzo yanayotolewa kwa vijana**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuliza:-

Je, ni mafunzo ya aina gani yanatolewa kwa vijana wa Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatoa mafunzo ya ujuzi Stadi na stadi za kazi kwa nguvu kazi ya vijana iliyopo katika soko la ajira, yaani

kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yanayotolewa ni: -

(i) Mafunzo ya kukuza ujuzi wa ufundi katika fani mbalimbali kwa njia ya Uanagenzi yaani *Apprenticeship training* ambapo kijana anatumia zaidi ya 60% ya muda wa mafunzo katika maeneo ya kazi;

(ii) Mafunzo ya kurasimisha ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo yaani *Recognition of Prior Learning Skills* ambapo vijana wanafanyiwa tathmini ya mapungufu waliyonayo, kupatiwa mafunzo na hatimaye kupatiwa vyeti ambavyo vitawasaidia kuendelea na mafunzo ngazi zinazofuata kwa ajili ya kuajiriwa au kujiajiri;

(iii) Mafunzo ya Uzoefu wa Kazi kwa wahitimu yaani *Internship Training* ambapo wahitimu wa ngazi mbalimbali za elimu wanapelekwa maeneo ya kazi kujifunza kazi;

(iv) Mafunzo ya kukuza ujuzi kwa wafanyakazi waliopo makazini yaani *Skills Updating and Upgrading* ili kuziba mapengo ya ujuzi yanayotokana na mabadiliko ya teknolojia na utendaji wa kazi na utoaji wa huduma;

(v) Mafunzo ya ujasiriamali, usimamizi wa biashara, miradi, Urasimishaji na Uendelezaji. Mafunzo haya huenda sambamba na utoaji mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana;

(vi) Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana hasa wale walio nje ya mfumo wa shule ili kuwawezesha kujitambua, kuwa na uzalendo na kufanya maamuzi sahihi kuhusu maisha yao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Latifa.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya kwa vijana nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Wizara mnampango gani au mnafanya utafiti kuona mafunzo haya jinsi gani yanawanufaisha vijana hao mara baada ya kumaliza mafunzo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; nataka kujua kama Wizara mnamkakati gani sasa wa kuweza kuwaongezea au kuwapa mitaji mikubwa zaidi kwa vile vikundi ambavyo vinafanya vizuri zaidi ili kuweza kuzalisha bora zaidi na kuzalisha vitu vizuri zaidi ili kuendelea kujiajiri na kuajiriwa ili kuweza kuongeza mapato kwa nchi yetu?

**NAIBU SPIKA:** Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Latifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunao mpango wa ufuatiliaji na tathmini ambao kila baada ya miezi mitatu tunafanya kupita kwenye maeneo ambayo vijana hawa wapo wakipata mafunzo lakini pia wale ambao wanapewa mitaji mbalimbali. Tumekuwa na utaratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ili kubaini na kuona kama kuna tija katika fedha ya nyingi ya Serikali ambayo inatolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweza kuwawezesha vijana kujikimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye hatua ya pili ambapo ameniuliza swali kama tunawapa mitaji? Ni kweli kwamba vijana hawa hatuwaachi tu kwa maana ya kuwatambua na kuwapeleka kwenye maeneo yao ya kupata mafunzo na wanapomaliza kupata mafunzo tunawaunganisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo ambao tunawapeleka *VETA*, wapo amabao tunawaunganisha kama wamefuzu vizuri kwenda kwenye maeneo ya ajira. Lakini pia tunwaratibu na kuwasaidia kuweza kupata ile mikopo ya 10% ya halmashauri ambapo mwongozo kwa sasa nikijibu swali la kwamba tuwape mitaji inayojitosheleza, tilikua tunatoa kwa vikundi vya watu 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua ya sasa na kwa Mwongozo mpya na kwa usikivu wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa vijana aliona ni vema aweze kubadilisha badala ya kuwapa vijana 10, sasa tunatoa mkopo kwa kuanzia shilingi milioni moja mpaka shilingi milioni 10 tumetoka sasa shilingi milioni 10 mpaka shilingi milioni 50 kwa kijana mmoja mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hatua nyingine tunawasaidia pia kuweza kupata mikopo kupitia benki. Zipo benki ambazo zimekwisha kuanza kuonesha mfano. Benki a Azania inatoa mikopo kwa *single digit* kwa sasa lakini zaidi ya hapo pia tunayo mifuko mingine, katika Wizara ya Kilimo tunao Mfuko wa Pembejeo za Kilimo ambapo vijana hawa nao pia wakimaliza kwenye mafunzo mbalimbali iwe *VETA* au kule kwenye programu za unenepeshaji ng'ombe au *BBT* tunawaendeleza kwenda mbali zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni ninayo furaha kukwambia tumepeleka vijana tena awamu nyigine ambao watafikia sasa 700 wanaoenda kupata mafunzo nchini Israel ili kuweza kuwatengeneza vijana na kuweza kuhakikisha kwamba kwa kweli wanatumia fursa za kiuchumi na kushiriki ujenzi wa Taifa lao, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa tunaendelea, Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mheshimiwa Regina.

Na. 75

**Kukamilisha ujenzi wa mabweni yaliyoanzishwa na wananchi nchini**

**MHE. REGINA N. QWARAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mabweni yaliyoanzishwa na wananchi kwa michango yao katika shule za kata nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023, Serikali iliidhinisha kiasi cha shilingi bilioni 9.21 kwa ajili ya ukamilishaji wa mabweni 461, kati ya hayo mabweni 28 ni kwa ajili ya shule za msingi zenye wanafunzi wenye mahitaji maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2023/2024 Serikali imetenga kiasi cha shilingi milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mabweni ili kuunga jitihada zilizofanywa na wananchi za kujiletea maendeleo. Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya mabweni kila mwaka kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Regina.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafsi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza, imekuwa ikiripotiwa mara kwa mara majanga ya moto katika mabweni ya shule zetu. Je, Serikali imefanya uchunguzi gani kujua chanzo ni nini na ni upi mkakati wa Serikali kupambana na janga hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika shule ambazo tayari mabweni yamekamilika kumekuwa hakuna walezi wa watoto au walezi wa wanafunzi katika shule zetu yaani *patrons* na *matrons* je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuwaajiri walezi wa watoto katika shule zetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Regina Qwaray, la kwanza hili juu ya majanga ya moto ambayo hujitokeza katika shule za bweni. Serikali kupitia Jeshi letu la Zima Moto na Uokoaji imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali hasa katika shule hizi za bweni juu ya namna bora ya kujikinga na majanga ya moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, na tutaendelea kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji kuhakikisha kwamba mafunzo haya yanazidi kutolewa kwenye halmashauri mbalimbali na nitumie nafasi hii mbele ya Bunge lako hili kutoa wito kwa halmashauri za Wilaya zote hapa nchini ambazo zina shule za bweni ziweze kuhakikisha zinashirikiana na Jeshi la Zima Moto na Uokoaji katika kutoa elimu ya kujikinga na moto katika shule zote za bweni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la pili la Mheshimiwa Regina Qwaray la mabweni kutokuwa na ma-*patron* na ma-*matron,* kwa sasa Serikali imeweka kipaumbele katika kuhakikisha inaajiri walimu wa kutosha kadiri ambavyo bajeti inaruhusu tunaajiri. Pale ikama itakapotimia tutaanza kuangalia ni namna gani tutaweza kuajiri ma-*patron* na ma-*matron* lakini kwa sasa walimu waliopo ndio wanateuliwa kwa ajili ya kuangalia watoto katika shule zile mabweni ambao ndiyo wanaokuwa ma-*patron* ndiyo wanaokuwa ma-*matron*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakaa na wenzetu wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kuona ni namna gani bora tunaweza tukapata vibali kwa ajili ya kuajiri ma-*matron* na ma-*patron* kwa ajili ya kutimiza ikama na upungufu ambao upo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga Sekondari mpya Kata ya Ketare eneo la Nyaburundu na Kata ya Mihingo eneo la Machimero kwa sababu ni muda mrefu Serikali imeahidi kujenga sekondari hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, lini Serikali itajenga sekondari mpya katika maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa Serikali inajenga shule mpya katika kila halmashauri hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwa Mheshimiwa Getere pia amepata zaidi ya shilingi milioni 580 kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya na tutazidi kutafuta fedha kwa sababu Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele cha kuhakikisha kata zote ambazo hazina sekondari zinajengewa sekondari mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira tutakapomaliza ujenzi wa hii shule ya shilingi milioni 580 ambayo iko jimboni kwake tutaendendelea kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari katika kata ambazo amezitaja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa kuna *smoke detecters* ambao ndio utaaalamu wa kisasa wa kujua kama moto unakuja.

Kwa nini Serikali haioni ni muhimu chombo hicho kuwekwa katika kila jengo la shule au taasisi inayojengwa ili waweze kupata *alert*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shally Raymond hili la *smoke detectors*. Kama nilivyokuwa nimeshazungumza hapo awali tutashikiana kwa karibu na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Jeshi la Zima Moto na Uokoaji kuona sasa ni namna gani tunaweza kuhakikisha majengo yote ya shule zetu yanakuwa ya *smoke detectors* hasa zile shule za bweni ambazo zina wanafunzi wanaolala pale muda wote.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea swali namba 78 Mheshimiwa kimei.

Na. 78

**Ujenzi wa barabara ya Chekereni – Kahe – Mabogini – *TPC***

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mchepuo kwenda Moshi kupitia Chekereni – Kahe – Mabogini - *TPC* kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii iko kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2020 kujengwa kwa kiwango cha lami. Hadi

sasa *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro imefanya usanifu wa barabara yote kilometa 31.25 ambapo kwa kuanzia makisio ya ujenzi wa kilomita 12 kwa kiwango cha lami yenye jumla ya shilingi bilioni 15 yamewasilishwa *TARURA* makao makuu kwa hatua zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES. S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Serikali imetoa majibu mazuri na nimeyafurahia sana, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, Bodi ya Barabara ya Mkoa wetu wa Kilimanjaro imeshatuma maombi kwenye Wizara ya kuipandisha hadhi Barabara hii ya Chekereni – Kahe – Mabogini – *TPC*.

Je, tutapata uthibitisho gani kwamba maombi haya yameshughulikiwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, nashukuru sana Serikali imeweza kutengeneza Daraja la Marangu Mtoni; lakini tunaomba kauli ya Serikali kuhusiana na kukamilisha kipande kilichobaki cha barabara hiyo kuanzia Kawawa – Nduoni kuja Marangu Mtoni ambayo ipo pia kwenye Ilani ya CCM, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Vunjo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni juu ya Bodi ya Barabara kuipandisha hadhi Barabara ya Kahe – Chekereni. Suala hili ni la kisheria na taratibu za namna ambavyo barabara inatakiwa kupandishwa hadhi na kwenda kwa wenzetu wa Wizara ya Ujenzi zipo wazi. Hivyo basi, tutakaa na Mheshimiwa Kimei kuona ni hatua zipi ambazo maombi haya yamefikia ili kuona kama tayari yamefika kwa Waziri wa Ujenzi mwenye dhamana ya kupandisha hadhi barabara hii. Kama maombi haya hayajafika basi tutaona ni namna gani yanaweza kufika ili

timu iweze kwenda kufanya *assessment* na barabara hii iweze kupandishwa hadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naenda kwenye swali lake la pili linalohuau Saraja la Marangu Mtoni, ambalo linaunganisha barabara ya Kawawa – Kahe – chekereni. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Vunjo, kwamba Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga zaidi ya shilingi milioni 989 kuhakikisha kwamba barabara katika jimbo la Mheshimiwa Kimei zinafanyiwa ukarabati ikiwemo Barabara hii ambayo inaitwa Fungate – Mabogini – Kahe – Chekereni ambapo kwa sasa kuna shilingi milioni 39. Inasubiri tu daraja lile likamailike ili barabara nayo iweze kuendelea kutengenezwa na iweze kupitika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mji mdogo wa Mbalizi una kilomita 33 za vumbi. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hizo kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Suma Fyandomo juu ya barabara hizi za Mbalizi zenye urefu wa kilomita 33. Tutatuma timu ya kuweza kufanya tathmini kutoka Wakala wa barabara za Vijijini na Mijini *(TATURA)* ili kuona ni kiasi gani kinahitajika ili kujenga barabara hizi kwa kiwango cha lami. Baada ya kufanya tathmini hiyo tutaona ni kwa namna gani Serikali inaweza ikatafuta fedha kadri ya upatikanaji wake kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hizi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunarudi kwenye swali namba 76, Mheshimiwa Amar.

Na. 76

**Kufunguliwa Kituo cha Afya Kafita na Zahanati ya Nyijundu – Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Je, lini Kituo cha Afya Kata ya Kafita na Zahanati ya Kijiji cha Nyijundu zitafunguliwa na kupelekewa vifaa baada ya ujenzi kukamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mbunge wa Jimbo la Nyang'hwale kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilitenga bajeti ya shilingi milioni 500 katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya ujenzi katika Zahanati ya Nyijundu ambayo imepandishwa hadhi kuwa kituo cha afya. Ujenzi huo umekamilika na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 120.4 vimepelekwa na huduma zimeanza kutolewa mwezi Aprili, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Kituo cha Afya Kafita unaendelea kwa fedha za *TASAF* shilingi milioni 500 ambapo majengo yanayojengwa ni jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje, jengo la maabara, jengo la wodi ya wazazi na jengo la upasuaji. Aidha, ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje na maabara umekamilika na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 120.4 vimepelekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri inaendelea na taratibu za ukamilishaji wa majengo yaliyobakia na huduma za

awali zitaanza kutolewa kwenye majengo yaliyokamilika ifikapo mwezi Octoba mwaka 2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza. Kwanza naishukuru Serikali kwa kupeleka fedha zaidi ya shilingi milioni 240 kwenye vituo hivyo vya afya, nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa tuna upungufu wa wahudumu wa afya kwenye vituo vya afya ikiwemo Kafita, Nyijundu, Kalumwa na Nyangh'wale na zahanati zote za Jimbo la Nyang'hwale; je, Serikali iko tayari kutupelekea wahudumu wa afya ili kuweza kukidhi mahitaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa pamoja na kwamba vituo vya afya vimejengwa vingi lakini bado tuna uhitaji wa ujenzi wa kituo cha afya kwenye Kata ya Busolwa; je, Serikali iko tayari kutujengea kituo cha afya kwenye Kata ya Busolwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Amar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napokea shukrani zake kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupeleka fedha nyingi za vifaa tiba katika Jimbo la Nyangh'wale na nchi nzima kwa ujumla. Kuhusu upungufu wa watumishi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote tumekuwa mashahidi, katika kipindi cha miaka hii miwili Serikali imeajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya zaidi ya 17,000 na kuwapeleka katika vituo vyetu vipya pamoja na vya zamani ambavyo vinaendelea kutoa huduma. Kwa hiyo zoezi hili ni endelevu, ajira zitaendelea kutolewa kwa awamu ili kuhakikisha kwamba vituo hivi vinaendelea kupata watumishi wa kutosha na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa swali la pili linalohusiana na Kituo cha Afya cha Busolwa, Serikali imeshaweka mkakati wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika maeneo ya kimkakati, tukizingatia umbali kutoka kituo cha karibu zaidi, idadi ya wananchi katika maeneo hayo na aina ya jiografia ya eneo husika. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutafanya tathmini kuona Kata ya Busolwa kama inakidhi vigezo, na kama inakidhi vigezo tutaanza na mapato ya ndani ya Halmashauri na baadaye Serikali itaona uwezekano wa kuongeza fedha kwa ajili ya kukamilisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itamalizia Kituo cha Afya cha Kata ya Kidaru katika Jimbo la Iramba, hasa ukizingatia watu wake wako pembezoni na hivyo hutembea umbali mrefu kufuata huduma hizo za afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeanza kujenga kituo cha afya ambacho amekitaja ambacho kipo katika Jimbo la Iramba, na sisi tutahakikisha kituo kile kinakamilika. Ujenzi wa vituo hivi vya afya unakwenda kwa awamu, tuna awamu ya kwanza, ya pili na ya tatu. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali itatoa kipaumbele kutafuta fedha ili tukamilishe ujenzi wa kituo hiki cha afya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Mji wa Mafinga imejenga Kituo cha Ifingo na Kituo cha Bumilayinga. Hata hivyo vituo hivi havina huduma kwa ajili ya kulaza akina baba, akina

mama na watoto isipokuwa tu kina jengo la mama na mtoto. Je, Serikali iko tayari kutusaidia na kuhakikisha tunapata hizo *facilities*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliweka mpango wa kujenga vituo vya afya vya kimkakati kwa awamu, na katika awamu ya kwanza ilitoa shilingi milioni 500. Kipaumbele ilikuwa ni majengo ya *OPD*, Maabara, Jengo la Mama na Mtoto pamoja na majengo ya upasuaji na kichomea taka. Hata hivyo, vituo vyote hivi ambavyo vimejengwa bado vinakosa huduma ya wodi ya wanaume, wanawake na wodi ya watoto. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Serikali itaendelea kwa awamu zinazofuata kujenga wodi kwa ajili ya kulaza wanaume, wanawake na watoto ikiwemo katika Kituo hiki cha Ifingo pamoja na Bumilayinga katika jimbo la Mafinga.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, Mheshimiwa Hassan Zidadu.

Na. 77

**Ujenzi wa Kituo cha Kisasa cha Mabasi - Tunduru**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Kituo cha mabasi cha kisasa katika Halmashauri ya Wilaya Tunduru?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru iliwasilisha andiko la mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi. Baada ya kuchambuliwa andiko hilo halikukidhi vigezo hivyo lilirejeshwa Halmashauri kwa ajili ya kufanya maboresho na kuanza kutenga fedha kupitia mapato ya ndani kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo ya mabasi limekodishwa kwa Kampuni ya *Kalpataru Power Transmissions Ltd* inayofanya kazi ya ujenzi wa gridi ya Taifa kwa miaka miwili, (2022/2023 na 2023/2024). Hivyo, Ofisi ya Rais TAMISEMI inaielekeza Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kukamilisha tathmini ya gharama za mradi na kuanza kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo katika mwaka wa fedha 2024/2025, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hassan.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza naomba kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali kwa majibu mazuri yanayoonyesha nia na mkakati wa kuanza mradi ule, lakini bado nina swali dogo la nyongeza. Je, Naibu Waziri yuko tayari kutembelea eneo la mradi ili kujionea umuhimu au ukubwa wa uhitaji wa mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nipokee pongezi zake kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyoifanya katika ujenzi wa vituo vya mabasi nchini kote. Nimhakikishie tu Mheshimiwa kwamba niko tayari baada ya kumaliza shughuli za Bunge, tutakubaliana

baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu tupange ratiba ya kwenda Tunduru tukapitie pale.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Florence.

**MHE. DKT. FLORENCE G. SAMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itajenga stendi ya mabasi katika Jimbo la Muhambwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Muhambwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawaelekeza Halmashauri ya Kibondo kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi na kuanza kutenga mapato ya ndani. Lakini kama uwezo hautatosha walete andiko hilo Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kutafuta fedha za kujengea stendi hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Momba hatuna stendi hata moja na kuna uhitaji mkubwa; je, ni lini Serikali itatupatia fedha tuweze kujenga kituo cha mabasi ili kitumike kama chanzo cha mapato kwenye Halmashauri yetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wajibu wa Wakurugenzi wa Halmashauri kutambua maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii ikiwemo stendi, pia, ni wajibu wao kuanza kutenga fedha kupitia mapato ya ndani na kuwasilisha maandiko Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi huo. Kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tunatoa maelekezo kwa

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Momba kufanya tathmini ili tujue gharama zinazohitajika ili waanze kutenga mapato ya ndani lakini pia ofisi ya Rais TAMISEMI tuone uwezekano wa kupata fedha kwa ajili ya shughuli hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea Ofisi ya Makamu wa Rais. Swali namba 79, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

Na. 79

**Mkakati wa dharura wa kunusuru athari za mabadiliko ya tabianchi - Nungwi**

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa dharura wa kunusuru athari za mabadiliko ya tabianchi - Nungwi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge wa Jimbo la Nungwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua changamoto za athari za mabadiliko ya tabianchi zilizopo eneo la Nungwi. Tayari, Serikali kupita Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 imetenga kiasi cha shilingi milioni 650 kwa ajili ya kufanya tathmini ya awali ya kuzuia athari hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo ni pamoja na kuelimisha wananchi kupanda mikoko pamoja na kuhamasisha ulimaji wa mwani

usioharibu fukwe. Serikali zote mbili za JMT na SMZ zitashirikiana katika kutafuta fedha zaidi ili kudhibiti uharibifu unaotokea eneo la Nungwi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sadiki.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa sasa ni mwaka wa tatu nimekuwa nikisimama katika Bunge hili kuulizia jitihada zinazochukuliwa na Serikali zote mbili katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi maeneo ya Nungwi lakini majibu tunayopata leo ndiyo kwanza shilingi milioni 650 zimetengwa kwa ajili ya kufanya utafiti. Ninachotaka kujua ni lini utafiti huu utaanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, shughuli za utalii na uchumi wa bluu zimekuwa zikiathiri sana ukataji wa mikoko katika maeneo ya fukwe za Bahari ya Hindi kule Zanzibar. Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuhakikisha kwamba mikoko inarejeshwa katika uhalisia wake? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumpongeza sana kwa kuwa jambo hili amekuwa akilipigia kelele sana na hatimaye sisi kama Serikali tumeshaandaa fedha kwa ajili ya kuanza angalau tathmini ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa fedha hizi zimeshapatikana naomba kumwambia tu Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa utafiti unaenda kuanza muda wowote. Kama tulivyosema kwamba kuna kuta za aina nyingi, kwa hiyo ni lazima utafiti ufanyike ili tujue ni aina gani ya kuta. Kuna kuta za *slope* ambazo zinatoa maji mitaani zinapeleka baharini, lakini pia kuna kuta ambazo zinakinga kutoka baharini maji yasije mitaani. Kwa hiyo ni vyema utafiti ufanyike ili tuone ni aina ya kuta na pia

tuweze kupima *current* ya maji ya *sea breeze* na *land breeze,* ni aina gani ya huduma ambayo wananchi wanatakiwa wapatiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, kwa upande wa swali la pili, tumechukua hatua nyingi. Moja ni kuendelea kutoa elimu wasikate, wapande na wasichome mikoko ambayo ipo *around* ufukwe wa bahari. Kubwa zaidi tumeendelea kuhimiza kupitia ilani ambayo inasema kwamba kila Halmashauri kila mwaka lazima ipande miti milioni 1.5. Kupitia miti hii tumehimiza mikoko ipewe kipaumbele ili kunusuru fukwe zetu lakini zaidi kuendelea na ile sera yetu ya soma na mti. Tunataka wanafunzi wa sekondari, msingi, vyuo na vyuo vikuu wapande miti, lakini miti ambayo tumeipa kipaumbele hasa kwa shule za fukwe ni mikoko, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Usonge.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa vile Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Muungano na Mazingira ndiyo ambayo inashughulika na masuala ya kuratibu na kushughulika na mabadiliko ya tabianchi. Nilitaka kujua je, mnatumia utaratibu gani wa kupokea miradi yote ambayo inatoka Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa kushughulika na haya mabadiliko ya tabianchi kwa upande wa Zanzibar?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu ni kwamba kwanza tunaandaa maandiko ambayo yanalenga kwenye mradi husika. Kinachofuata sasa ni kufanya tathmini na utafiti wa kujua mradi ulioombwa na baadaye mradi huo unaanza utekelezwaji kama miradi iliyotekelezwa huko Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ikupa.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Hivi karibuni Serikali imetangaza uwepo wa Mvua za El nino. Ni upi mkakati wa haraka wa Serikali kupunguza athari zitakazotokana

na mvua hizi ndani ya Jiji la Dar es Salaam na hasa mafuriko ambayo yanasababishwa na Mto Msimbazi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kipindi cha mvua kubwa mara nyingi kunakuwa na mafuriko makubwa ambayo yanasababisha athari hasa kwenye makazi ya wananchi. Wakati mwingine inafika hatua mafuriko yanagharimu maisha ya wananchi. Namwambia Mheshimiwa kwamba huwa tunachukua hatua nyingi. Moja, ni kuelimisha wananchi; kwa mfano sasa hivi tumeanza kutoa elimu kuhusu Mvua za El nino ambazo zinategemea kuja. Tunawaambia wananchi wasijenge kwenye maeneo au karibu na maeneo ambayo yanajaa maji ili kama wana mpango huo waanze kuondoka mapema ili zitakapokuja mvua wasiweze kupata mafuriko hayo ama mafuriko hayo kuleta athari kwa wananchi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, ni lini Serikali itaanza kujenga Mto Msimbazi ukizingatia sasa hivi wataalam wa hali ya hewa wamesema kwamba kuna mvua kubwa inanyesha; je, ni lini wataanza kutujengea ili wananchi wetu wawe salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ujenzi wa Mto Msimbazi umeanza, na nimwambie tu Mheshimiwa kwa kuwa ujenzi huu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umeanza au uko katika maandalizi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hatua tuliyofikia maana yake sasa tunakwenda kuanza.

**NAIBU SPIKA:** Haya, endelea.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namwambia Mheshimiwa kwamba uanzaji huu unakwenda kwa hatua. Hatua hizi zinakwenda kadri tutakavyokuwa tunapata fedha. Tutahakikisha kwamba maeneo yote yatajengwa na tutahakikisha kwamba tunapata usalama wa wananchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri pamoja na kwamba wewe uko Serikalini bado fidia za wakazi hazijalipwa, na mvua hizi zinazokuja zitaathiri maeneo yale tena. Tunaomba Serikali mlipe fidia za watu ambazo zimeahidiwa ili watu wahame na wakatafute makazi maeneo mengine.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, tumelichukua hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia, Mheshimiwa Almas Maige.

Na. 80

**Minara ya mawasiliano itakayosimikwa Uyui**

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE** aliuliza:-

Je, ni minara mingapi ya mawasiliano ya simu itasimikwa Uyui kati ya minara 780 itakayojengwa nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la

Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(DTP)*, Serikali imeainisha kata tisa zilizopo Uyuyi ambazo zimepatiwa watoa huduma *(Airtel, Halotel* na *TTCL)* hivyo kufanya idadi ya minara tisa itakayojengwa na tunatarajia vijiji 26 vilivyopo katika kata hizo vitanufaika na huduma baada ya kukamilika kwa ujenzi wa minara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wilaya ya Uyui ni miongoni mwa Wilaya zinazonufaika na Miradi ya Mawasiliano kupitia *UCSAF*, ambapo idadi ya minara 28 imejengwa na imekamilika katika kata 25 zilizopo wilayani humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha na kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa upande wa Jimbo la Tabora Kaskazini, Kata za Igulungu, Kalola, Ufuluma, Nsimbo na Upuge zimefanyiwa tathmini na sasa Serikali kupitia *UCSAF* inamtafuta mtoa huduma atakayefikisha huduma ya mawasiliano katika maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na Serikali imetoa majibu mazuri sana, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Kata ya Ibili ilikuwepo katika mradi wa kwanza ambao ulikuwa ujengewe mnara, je, imeondolewa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; wananchi wategemee lini mradi huu wa kata tano utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Athuman Almas Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Ibili imo katika Mradi wa Tanzania ya Kidigitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha pili, kama ambavyo nimesema katika jibu langu la msingi, Serikali kupitia *UCSAF* tunamtafuta mtoa huduma na mchakato utakapokamilika basi mtoa huduma atafika maeneo hayo kwa ajili ya kupata eneo na baadaye atapata vibali na kuanza shughuli ya ujenzi wa mnara huo kwa ajili ya wananchi wa Tabora Kaskazini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Naibu Waziri amefika kwenye jimbo langu. Je, minara ya Kata za Eshkesh, Endahagichan, Geterer, Maretadu, Gidarudagaw na Endamiley lini inajengwa?

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Flatei, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mbulu Vijijini lipo katika minara 758 na tayari watoa huduma wapo katika hatua mbalimbali, hivyo nwmwomba Mheshimiwa Mbunge, wanapofika katika maeneo yake wananchi watoe ushirikiano kwa ajili ya kupata eneo kwa ajili ya ujenzi wa minara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, akishirikiana na watoa huduma, basi ujenzi wa minara utaanza mara moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi ya swali la nyongeza. Kata ya Lihimalyao na Vijiji vyake vya Mangesani pamoja na Kisongo katika Jimbo la Kilwa Kusini, hakuna kabisa mawasiliano ya simu na katika awamu hii ya ujenzi wa minara 758 haijafikiriwa au haijapata nafasi. Nini

mpango wa Serikali kwenda kujenga minara katika Kata ya Lihimalyao?

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaongea na inawezekana kuna maeneo mengine ndani ya nchi yetu bado hayajapa mawasiliano. Serikali inaendelea kutekeleza miradi hii kwa awamu. Awamu ya kwanza tumemaliza minara 758, kuna awamu inayokuja ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametafuta fedha kwa ajili ya kuleta minara 600.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge, tukitoka hapa tukutane ili niweze kuchukua taarifa za uhakika kuhusu maeneo hayo ili tuwatume wataalam wetu, wakajiridhishe ili tuweze kuchukua hatua za kufikisha mawasiliano ndani ya kata hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili, Mheshimiwa Mkundi.

Na. 81

**Mapango ya Handebezya na jiwe linalocheza kuwa na tija kwa Taifa**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kuvifanya vivutio vya mapango ya Handebezya na jiwe linalocheza kuwa na tija kwa Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuendeleza, kukuza na kutunza vivutio vya utalii vilivyopo Ukerewe vikiwemo Mapango ya Handebezya na Jiwe linalocheza vinavyopatikana katika Kisiwa cha Ukerewe. Mikakati hiyo ni pamoja na kutangaza vivutio hivyo kwa kutumia vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Naibu Spika, mathalan, Wizara kupitia *TTB* iliratibu ziara ya Kituo cha Televisheni cha *ITV* kwenda kutembelea baadhi ya vivutio vya utalii vilivyopo Ukerewe vikiwemo Mapango ya Handebezya na jiwe linalocheza kwa ajili ya kuandaa *documentary* ambayo itakapokamilika itaonyeshwa katika kipindi cha *ITV* cha Chetu ni Chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mafunzo yanaendelea kutolewa kuhusu uanzishwaji wa utalii wa utamaduni ambapo hadi sasa kuna vikundi vya utalii wa utamaduni vikiwemo Ukerewe *(Ukerewe Cultural Tourism Enterprises)* na Nansio *(Nansio Cultural Tourism Enterprises)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii imeendelea kushiriki katika maonesho na matamasha mbalimbali yakiwemo Maonesho ya Biashara ya Afrika Mashariki na Tamasha la Bulabo yanayofanyika katika Kanda ya Ziwa kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii na fursa za uwekezaji zilizopo katika ukanda huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha uwekezaji wa miundombinu inayoelekea katika maeneo yenye vivutio vya utalii, ujenzi wa huduma za malazi zenye hadhi pamoja na kuboresha huduma za kijamii, ikiwemo maji, umeme, huduma za kibenki na mawasiliano.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Natumia nafasi hii kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa jitihada zinazofanywa, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Napongeza Wizara kwa kutumia *TTB* na kuratibu ziara ya waandishi wa habari kwa ajili ya kubaini vivutio hivi. Hata hivyo, huwezi kutenganisha utalii na rika mbalimbali kwenye eneo husika kwa maana ya watu wazima, wazee, rika la kati na watoto katika kubaini na kuendeleza utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara hii imefanikiwa, lakini bahati mbaya sana kuna rika la watu wazima, kuna kikundi cha KUMIDEU na vinginevyo ambavyo vinafahamu zaidi utamaduni, mila na desturi za watu wa Ukerewe, walitakiwa kuhusishwa. Nini sasa mkakati wa Serikali ili wakati mwingine vikundi kama hivi vishirikishwe ili kupata uhalisia wa vivutio vya utalii vilivyopo pale Ukerewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pamoja na jitihada zinazofanywa na Serikali, lakini tunakosa kiungo kinachoweza kuratibu mambo haya ya utalii. Halmashauri zetu zingeweza kutoa msaada mkubwa sana, lakini bahati mbaya sana hazina watu *specific* wanaoshughulika na utalii zaidi ya utamaduni. Je, ni nini mkakati wa Serikali sasa kuhakikisha Halmashauri zetu zote zinakuwa ama na idara au na vitengo vinavyohusika na utalii ili kuweza kuunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais katika kukuza Sekta ya Utalii? Nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ulimwenguni kote, *custodian* wa mila na desturi ni Machifu wakienda sambamba na wazee wa mila na desturi. Kwa bahati mbaya kwenye halmashauri zetu kumekuwa na upungufu wa kubaini makundi haya ya wazee wa mila na desturi. Natoa rai kwa halmashauri zetu, ziwe na mikakati ya kuwatambua wazee wa mila na desturi ambao ndio *custodian* wa tamaduni zetu ili tunapofanya jukumu la kutambua na

kutangaza vivutio vilivyopo kwenye maeneo yetu, basi wazee hawa waweze kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa rai kwa halmashauri zetu, zijielekeze kwenye kutambua maeneo yote yenye sifa za kiutalii, wawasiliane na Wizara ili maeneo haya yaweze kusajiliwa tuweze kuweka mpango mkakati wa pamoja wa kutangaza maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la pili la uhaba au kukosekana kwa kiungo, kwa kukosekana wataalam kwenye halmashauri zetu. Mamlaka ya ajira ya watumishi kwenye ngazi ya halmashauri, ni Wizara ya TAMISEMI. Naomba sana halmashauri zetu zijielekeze kwenda kuomba vibali vya ajira kwa TAMISEMI ili jambo hili liweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa kutambua *gap* lililopo, Wizara ya Maliasili inao wataalam kwenye kanda zetu. Kwa mfano, kwenye Kanda ya Ziwa Victoria, tunao wataalam wetu wawili walioko Mwanza, Kanda ya Kusini, tunao wataalam watatu wapo Iringa, Kanda ya Kaskazini, tunao wataalam sita wapo Arusha, Kanda ya Pwani, tunao sita wapo Dar es Salam lakini vilevile hapa Makao Makuu tunao wataalam. Tunaomba halmashauri zetu ziwatumie wataalam hawa wakati wakijiandaa kupata vibali vya ajira kutoka TAMISEMI.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Robert Chacha.

**MHE. ROBERT C. MABOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba kuuliza swali la nyongeza. Wananchi wangu wa Jimbo la Bunda Mjini 299 ambao wamelishiwa mazao yao, hawajalipwa fidia yao. Serikali inawalipa lini? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hilo swali nafikiri halihusiani na swali la msingi.

Kwa hiyo, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 82

**Kuweka Mdaki katika Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaweka Mdaki katika Bandari ya Dar es Salaam kwa meli za abiria na mizigo za *Azam Sea Link* ili kuondoa usumbufu na kero kwa abiria?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TPA* imenunua midaki mitatu kwa ajili ya kuimarisha shughuli za ukaguzi katika eneo la *Azam Link* na eneo la kuhifadhi mizigo *(Baggage room)* ambapo midaki miwili imeshafungwa eneo la kuingia na kutoka katika eneo la kuhifadhi mizigo *(Baggage room)* na mdaki mmoja utafungwa katika eneo la *Azam Link*. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali kupitla Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*, imetenga fedha kwa ajili ya kununua midaki mingine, kwa ajili ya eneo la *Lighter Quay* na yadi ya magari *(RORO Yard)*, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Waziri, swali la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba uko mdaki mmoja utafungwa katika eneo la *Azam Sea Link*, tunataka kujua, ni lini mdaki huu utakwenda kufungwa ili kuondoa adha kwa wananchi wanaotumia eneo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa vilevile Mheshimiwa Waziri amesema kwenye bajeti ya mwaka huu, wametenga fedha kwa ajili ya kununua midaki mingine. Je, ni midaki mingapi itakwenda kunuliwa kwa ajili ya eneo la *Azam Sea Link* ili kuendelea kuboresha eneo hili? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza kuhusu lini, ni ndani ya Mwaka huu wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu ni midaki mingapi itajengwa kwenye eneo hili ni kwamba hakuna mpango wa kuongeza kwenye eneo la *Azam Link* kwa sababu tayari umeshapatikana mmoja na kama kutakuwa na uhitaji tutakwenda kwenye maeneo mengine yenye uhitaji mkubwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Amandus hayupo, kwa niaba, Mheshimiwa Kuchauka.

Na. 83

**Hitaji la Maji Kata za Nachingwea**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA K.n.y. MHE. AMANDUS J. CHINGUILE** aliuliza:-

Je lini maji safi na salama yatapelekwa katika Kata za Kiegei, Kilimarondo, Matekwe na Namapwia – Nachingwea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amandus Julius Chinguile, Mbunge wa Jimbo la Nachingwea, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, katika kuhakikisha Kata za Kiegei, Kilimarondo, Matekwe na Namapwia zinapata huduma ya majisafi na salama na yenye kutosheleza, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 itafanya utafiti wa maji chini ya ardhi *(Hydrogeological Survey)* pamoja na kuchimba visima virefu vinne katika kata hizo. Kazi hiyo inatarajiwa kufanyika na kukamilika mwezi Disemba, 2023. Uendelezaji wa visima hivyo utafanyika mara baada ya uchimbaji kukamilika na maji kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali yanayotia moyo, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Mji wa Nachingwea ni mji unaokua haraka sana. Upo Mradi wa Maji pale Nachingwea ambao tayari sasa hivi imeonekana mradi ule hautoshelezi. Je, Serikali iko tayari kutupatia fedha Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea ili kupanua Mradi ule wa Maji wa Mji wa Nachingwea?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kama ilivyo kwa Mji wa Nachingwea unakua haraka, Mji wa Liwale nao una mradi sasa una miaka zaidi ya miwili kwa ajili ya maji katika Mji wa Liwale. Je, Serikali ipo tayari kutupatia fedha ili tuondokane na adha ya maji pale Mjini Liwale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Amandus, kwa niaba yake yameulizwa na Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu pesa Nachingwea kwa ajili ya kupanua mradi; nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, hili

tunalifanyia kazi. Tayari lipo kwenye mipango kuhakikisha katika Mji wa Nachingwea wanapata huduma ya majisafi na salama na ya kutosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa Liwale, nimelipokea, tutalifanyia kazi. Pia naomba kumpa taarifa, wale wawekezaji wetu walishafika Liwale, naamini atakuwa amewaona, watakwenda kufanya usambazaji wa visima vilivyochimbwa. Yote hii ni kuona kwamba jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kumtua mama ndoo kichwani Liwale nazo zinaweza kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Katika Mji wa Kasulu eneo la Mwilamvya kuna tatizo la upatikanaji wa maji. Je, ni lini Serikali itamaliza tatizo la maji katika Mji wa Kasulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Genzabuke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ya Kasulu tayari pia tuna mipango ya kuona kwamba tunakuja kuongeza huduma ya maji. Mwaka huu wa fedha tutafanya kazi kubwa sana Kasulu kuhakikisha maeneo ambayo maji hayajafika yaweze kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Kilave.

Na. 84

## Hitaji la Maji ya *DAWASA* Kata za Temeke

**MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka huduma ya maji ya *DAWASA* katika Kata za Buza, Vituka, Makangarawe na Sandali - Temeke?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Jimbo la Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha wananchi wa Kata za Buza, Vituka, Makangarawe na Sandali katika Manispaa ya Temeke wanapata huduma ya maji, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Usambazaji Maji wa *JET*-Buza ambao hadi kufikia mwezi Agosti, 2023, utekelezaji umeweza kufikia asilimia 30 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Mradi huo utanufaisha wananchi zaidi ya 173,810 wa Kata hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuboresha huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 itaanza utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji utakaonufaisha Jimbo la uchaguzi la Temeke, Kata za Buza, Vituka, Makangarawe na Sandali pamoja na Majimbo mengine matano ya uchaguzi ya Kibamba, Ubungo, Kinyerezi, Ukonga na Ilala. Kazi zilizopangwa kufanyika ni pamoja na ujenzi wa tenki la lita milioni tisa eneo la Bangulo na ulazi wa mtandao wa mabomba wa umbali wa kilometa 124. Mradi huo unatarijiwa kukamilika ifikapo Desemba, 2024.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini je, sasa Serikali haioni ipo haja ya visima vile ambavyo vilichukuliwa na *DAWASA* ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam viweze kurudishwa mikononi mwa wananchi, kwa sababu tangu vilipochukuliwa mpaka sasa hakuna marekebsho yoyote na ndiyo maana tunakosa maji mahali pengine kwa sababu visima vilikuwa ni vingi lakini *DAWASA* hawavifanyii kazi. Hivyo virudishwe kwa wananchi ili maji

yaendelee kupatikana kulingana na hizi asilimia 30 mlizosema mpaka sasa yanapatikana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili je, lini Serikali sasa mtarekebisha au mtaweka mabomba, kwani yaliyopo ni chakavu a ya zamani sana ambapo sasa hivi yanatitirisha maji tu na ni upotevu tu wa maji kwa Serikali lakini sasa tuombe muweze kuyarekebisha na wananchi tuendelee kupata maji safi katika mabomba ya majumbani? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawilii ya nyongeza ya Mheshimiwa Dorothy Kilave, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, visima vilivyochukuliwa kurudishwa kwa wananachi, visima hivi vilichukuliwa kwa sababu za kiufundi. Sasa hivi namna ambavyo kwa mfano Wizara ya Afya inaweza kumiliki hospitali zake, nasi Wizara ya Maji tunahitaji kumiliki vyanzo hivi vya maji vyote ili viwe chini ya uangalizi wa wataalam wetu. Kwa hiyo, cha kufanya hapa hatutavirudisha kwa wananchi bali tutaongeza nguvu kuhakikisha visima hivi vinakwenda kutumika na kuongeza usambazaji wa maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubadili mabomba chakavu tayari hili lipo kwenye mkakati wa mwaka huu wa fedha 2023/2024 utaona Mheshimiwa Mbunge kazi huko namna ambavyo vijana wanachakarika. Nimpongeze sana *CEO* wa *DAWASA* ameingia kwa kasi na watendaji wake wote wanafanya kazi kwa kasi. Wiki iliyopita nimefanya ziara pamoja na *DAWASA* maeneo haya yote ninayozungumzia Mheshimiwa Kilave, nimeweza kuyapitia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri hivi visima toka mchukue, hivi mmefanya tathmini ya ufanisi wake? Visima hivi vyote vya wananchi ambavyo *DASAWA* wamevichukua mmefanya tathmini yoyote?

Mheshimiwa Waziri, visima hivi vyote vimekufa katika Jimbo la Ilala, mnawapa taabu wananchi, mnajiongezea mzigo *for nothing*. Tunaomba mfikirie upya namna ya kuvirudisha visima hivi kwa wananchi ambapo watavi-*maintain* na watavifanyia kazi. Mheshimiwa Anatropia. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nataka kujua wananchi wa Kata ya Kamoli hutembea muda mrefu kufata chanzo cha Kitagata ambacho hakijatengenezwa vizuri, hivyo kukanyaga maji na kuchota maji machafu. Nataka nijue mkakati uliopo kuimarisha hicho chanzo cha maji lakini yakivutwa ili kuwa karibu na makazi ya watu badada ya kutembea umbali mrefu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hii ya Kamoli kuboresha chanzo na kuleta usambazaji. Katika mwaka huu wa fedha Mheshimiwa Mbunge kuna kazi itafanyika kuona kwamba chanzo hiki kinaendelea kuwa toshelevu kinakuwa endelevu na usambazaji wa kuwasogezea huduma wananchi ni moja ya kazi yetu mama Wizara ya Maji, tutafanya hilo Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mheshimiwa Ngassa.

Na. 85

**Mradi wa maji ya Ziwa Victoria Kwenda Igunga**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza mradi wa maji wa Ziwa Victoria kwenda vijiji na vitongoji vya Kata za Nguvumoja, Lugubu na Itumba – Igunga?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu spika, katika jitihada za kuboresha huduma ya maji safi na salama kwenye Kata za Nguvumoja, Lugubu na Itumba zilizopo Wilaya ya Igunga, Serikali inatekeleza mipango ya muda mfupi na muda mrefu, ambapo katika mpango wa muda mfupi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Serikali itafunga pampu za kutumia Nishati ya umeme jua katika visima virefu vya Vijiji vya Nguvumoja, Mwanshoma, Lugubu na Itumba ili kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji na kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Serikali imepanga kufanya utafiti wa maji ardhini na kuchimba kisima kirefu katika Kijiji cha Chagana kilichopo Kata ya Lubugu katika kipindi cha Mwezi Desemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa muda mrefu, Serikali itaboresha huduma ya maji safi na salama na yenye kutosheleza katika Kata za Nguvumoja, Lugubu na Itumba – Igunga kwa kutumia mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambapo upembuzi yakinifu na usanifu wake wa kina umekamilika na utaanza utekelezaji mara fedha zitakapopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ngassa.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wakati wa usanifu wa maji kutoka Igunga kwenda Shelui wataalam wa Wizara waliwaaminisha wananchi kwamba yangetengenezwa matoleo kwa ajili ya kusambaza maji kwenye hizi kata ya Nguvumoja, Lugubu na Itumba lakini mradi umekamilika na matoleo ya maji hayajawekwa na wananchi hawajapata maji.

Je, Wizara hamuoni kutokutekeleza kwa kipengele hichi ni kuwachonganisha wananchi na Serikali yao sikivu?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa Wizara mmekuwa na utaratibu wa kutoa fedha kwa matokeo *(P4R)* na Mkoa wa Tabora tunafanya vizuri sana.

Je, hamuoni ni wakati sasa mtoe fedha ili kwenda kukamilisha huu mradi ili wananchi waendelee kuwa wanafurahia Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote ninapenda kukupongeza Mheshimiwa Ngassa kwa ufuatiliaji, lakini Mheshimiwa Ngassa Wizara hata siku moja haitaweza kuwa chonganishi kati ya Serikali na wananchi, tutaweza kufanya kwa bidii kubwa sana kuhakikisha Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama mwenye uchungu wa wanawake wanaobeba ndoo kichwani inatekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutotoa matoleo ni sababu za kiufundi Mheshimiwa Mbunge, wakati fulani wakati usanifu unafanyika tulitarajia ingewezekana lakini *population* ya watu Tanzania sasa hivi inakua kila leo, kwa hiyo usanifu huu mpya utaleta maji ya kutosha na yatakuwa endelevu kwa eneo zima hili la Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *P4R* tuna kila sababu ya kumshukuru na kumpongeza sana Dkt. Samia, tulikuwa na Mikoa 17 pekee yenye kupata fedha za *P4R* lakini sasa hivi ni Mikoa yote 25 Mheshimiwa Rais Dkt. Samia amepambana fedha zimepatikana kwa Mikoa yote, na eneo la Tabora kama ulivyosema linafanya vizuri tayari fedha pia zimeanza kupelekwa na fedha zimeongezeka. Kwa hiyo, ninakutoa hofu, hili mimi na wewe naomba tuonane ili tuweze kuweka sawa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mradi wa maji wa Usalimwani - Mvumbi, Kitulo- Ijuni, Kidepwe - Madihani, Mariwa - Ikete ni miradi ambayo imesimama. Ni lini

Serikali itatoa fedha ili miradi hii iweze kukamilika kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Makete?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sanga, Mbunge machachari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha tayari zimeanza kutoka wiki hii, tutarajie hata Wakandarasi wanaofanya miradi hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge watalipwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar.

Na. 86

**Mchango wa uvuvi kwenye uchumi wa Taifa**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, ni kwa kiwango gani bahari zinachangia kukua kwa uchumi kupitia uvuvi?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uvuvi hutoa mchango katika uchumi wa nchi kupitia uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali zinazozalishwa ndani ya sekta. Aidha, baadhi ya bidhaa na huduma zinazozalishwa hutumika kama mali ghafi katika uzalishaji ndani ya sekta nyingine kama vile viwanda na kuwa na mchango mkubwa zaidi katika sekta hizo. Katika mwaka 2022, sekta ya uvuvi ilichangia asilimia 1.8 ya Pato la Taifa huku ikikua kwa asilimia 1.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, mazao ya uvuvi kutoka baharini yalichangia jumla ya tani 54,823 sawa na asilimia 10.6 ya mazao ya uvuvi ambayo ni tani 513,525. Vilevile, maduhuli ya Serikali ya shilingi bilioni 1.8 yalikusanywa kutoka katika shughuli za uvuvi baharini. Kiasi hicho cha mazao ya uvuvi kilichozalishwa kutoka baharini kilitokana na uvuvi mdogo na kilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 356.3. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana pia nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa sekta hii ya uvuvi kwenye Pato la Taifa kwa kiwango cha asilimia 1.8, tunakubaliana kwamba mchango huu bado ni mdogo sana, lakini nafahamu kwamba ipo mipango ya Serikali kununua meli kwa ajili ya uvuvi wa Bahari Kuu. Nataka kufahamu ni *stage* gani tumefikia kwenye uagizaji wa meli hizi kwenda kuvua kwenye Bahari Kuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kujua ni kwa namna gani mipango hii ya Serikali kwenye Wizara hii ya Uvuvi inaishirikisha Zanzibar katika kukuza Uchumi wa Bluu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar. Swali lake la kwanza anataka kujua kuhusu mchango.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mchango huu ni mdogo, mchango wa asilimia 1.9 ni mchango mdogo na ndiyo maana Serikali imekuja na mikakati mbalimbali ambayo itakuja kusaidia sana kuinua kipato hiki. Moja ya mikakati ambayo Serikali imekuja nayo ni pamoja na ujenzi wa Bandari ya Uvuvi. Tunakwenda kujenga Bandari ya Uvuvi pia kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya samaki, pia kufufua viwanda ambavyo tayari vimeshakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba asilimia 1.9 ni asilimia ndogo na Serikali iko na mkakati wa kufanya kazi hiyo ikiwa ni pamoja na kufufua Shirika la *TAFICO* ambalo tayari limeshakufa. Kwa hiyo, tunayo mikakati kama Serikali kwamba mikakati hiyo ambayo tumeiweka tukiitimiza vizuri tunaweza tukaongeza pato kutoka 1.9 kwenda juu zaidi. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge avute subira kwamba iko mikakati Serikali inajipanga kwa ajili ya kwenda kuimarisha jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ametaka kujua ni lini ununuzi wa meli hiyo utakamilika. Mchakato wa ununuzi wa meli upo unaendelea lakini umesimama kidogo kwa sababu za kibajeti. Kwa hiyo, mara Serikali itakapopata fedha ununuzi wa meli hiyo utaweza kufanyika mara moja. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Lupembe.

Na. 87

**Ujenzi wa lambo katika Kijiji cha Mwenge – Nsimbo**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa mradi wa lambo Kata ya Nsimbo, Kijiji cha Mwenge, Halmashauri ya Nsimbo?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Jimbo la Nsimbo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo hapa nchini, Serikali ilianza ujenzi wa mabwawa manne ya maji kwa mifugo likiwemo bwawa la Isulamilomo lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo. Aidha, ujenzi wa Bwawa la Isulamilomo haukukamilika katika muda uliopangwa kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati

wa utekelezaji wa mradi, ikiwemo kukosekana kwa barabara ya kusafirisha mitambo kwenda eneo la mradi na kipindi kirefu cha mvua nyingi katika eneo la mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto hizo, Mkandarasi aliomba kuongezewa muda wa kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo ambapo ujenzi unatarajiwa kukamilika mwezi Oktoba, 2023. Kwa sasa, Mkandarasi yupo katika eneo la mradi akiendelea na kazi ya ujenzi wa tuta na njia ya utoro wa maji. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lupembe.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya ucheleweshwaji wa mradi huu masika ikakuta mradi umecheleweshwa na mvua za masika, lakini Mkandarasi alichukua muda mrefu sana kuingia *site* katika kujenga mradi huu na mradi huu unajengwa na Wizara, haushirikishi Halmashauri ambayo wako katika eneo husika la mradi.

Je, Serikali ina mkakati gani kushirikisha kwa ukamilifu Halmashauri ya Nsimbo ili kuendelea kusimamia mradi huu?

Swali la pili, Serikali inachelewesha malipo ya Mkandarasi, Mkandarasi anashindwa kutekeleza mradi kutokana na kukosa kulipwa pesa. Je, ni lini Serikali itamlipa Mkandarasi pesa zake ili aweze kukamilisha mradi?*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza miradi hii ni miradi ya Serikali, haijalishi mradi unatekelezwa na Wizara ama unatekelezwa na Halmashauri, miradi hii yote ni ya Serikali. Miradi

hii inapokuja huku kwenye Halmashauri maana yake mamlaka zote za Serikali zinapaswa kushiriki katika kutekeleza mradi huo, kwa sababu miradi hii haimaanishi kwamba inapojengwa na Wizara ni kwamba Serikali nyingine haihusiki, Hapana! Sasa hii ni dhana ya uelewa katika Halmashauri zetu kwamba miradi inapokuja kwa namna moja au nyingine ni lazima watumishi wa Halmashauri washiriki kwa namna moja ama nyingine katika kusimamia mradi huo ili kuleta tija na ubora wa miradi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge ametaka kujua namna ya ucheleweshaji wa malipo. Malipo ya Serikali yoyote yanalipwa kulingana na *certificate* ya utekelezaji wa mradi alipofikia huyo Mkandarasi. Serikali inalipa fedha kutokana na *certificate* alizo-*raise* ambazo zinatokana na kazi aliyoifanya kwa kiwango hicho na huyu mkandarasi mpaka sasa ameshalipwa zaidi ya asilimia 70 ya malipo yake kwa sababu jumla ya shilingi milioni zaidi ya 270 amekwishalipwa kati ya milioni 510.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo Mkandarasi huyu anakwenda vizuri na ukiona mradi unachelewa ni kwa sababu ya upatikanaj wa fedha lakini ni pamoja na kwamba kazi anayoifanya ndiyo itakayo-*determine* analipwa fedha kiasi gani, kwa hiyo, huyu analipwa kulingana na kazi anayoifanya. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo.

Na. 88

**Idadi ya maprofesa inayozalishwa kwa mwaka nchini**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza:-

Je, ni maprofesa wangapi wanaozalishwa kila mwaka na ni wangapi wanastaafu kwa kipindi hicho?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mbunge wa Muleba Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa ni ngazi ya kitaaluma ambapo Mhadhiri au Mtumishi wa Taasisi za Elimu ya Juu hufikia baada ya matokeo ya kazi za kitaaluma ikiwemo kufanya machapisho na ufundishaji. Hivyo, kupanda cheo cha mwanataaluma kunatokana na jitihada za mhusika katika ufundishaji, kufanya tafiti na kuchapisha maandiko yake katika majarida yanayotambulika Kitaifa na Kimataifa. Hivyo, kuongezeka kwa idadi yao kunategemea zaidi jitihadi za mtu binafsi katika utekelezaji wa majukumu yake na kukubalika kwa jitihada hizo kwa wanataaluma wenziwe kwa kuzingatia miongozo waliyojiwekea. Hadi kufikia Mwaka 2022 tulikuwa na jumla ya Maprofesa 226 kati yao 163 wakiwa ni Maprofesa Washiriki *(Associate Professors)* na 63 ni Maprofesa Kamili *(Full Professors)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kustaafu linahusu zaidi Vyuo Vikuu vya Umma ambao umri wa kustaafu ni miaka 65. Kwa takwimu za mwaka 2022 idadi ya maprofesa kamili waliostaafu ni wanne na wanaotarajia kustaafu kwa mwaka 2023 ni watano, kwa mwaka 2024 ni Wawili, na mwaka 2025 ni sita. Maprofesa Washiriki waliostaafu kwa mwaka 2022 ni mmoja na wanaotarajiwa kustaafu kwa mwaka 2023 ni 18, mwaka 2024 ni wanne, na mwaka 2025 ni sita. Ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali ni majibu mazuri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia idadi ya Maprofesa nchini imeporomoka sana kwa kipindi cha miaka 10 iliyopita. Chuo Kikuu pekee cha Dar es Salaam kinahitaji Maprofesa 161 lakini wapo Maprofesa tisa. Sasa kwa nini Serikali isibadili umri wa

kustaafu kutoka miaka 65 mpaka miaka 70 ili kutunza hao wachache tulionao?*(Makofi)*

Swali la pili, kwa nini Serikali sasa kwa kuwa tunao uhitaji mkubwa wa Maprofesa isitoe *package* nzuri ili kuwavutia vijana wengi wakajitahidi kufanya *research* ili waweze kufikia hiyo hatua ya Uprofesa kwa ajili ya kutunza vyuo vyetu vikuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kikoyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la msingi, Serikali imeendelea kuchukua hatua za kukabiliana na upungufu wa watumishi na taaluma katika vyuo vyetu vikuu vya umma nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza, tunaendelea kuongeza nafasi za ajira kwa Wahadhiri pamoja na Wanataaluma katika vyuo vyetu. Jambo la pili, tunaendelea kuruhusu uhamisho wa watumishi wenye sifa kutoka taasisi nyingine za Serikali ili kuweza kuingia katika Vyuo Vikuu na kuhudumu kama Wahadhiri pamoja na kwenda kwenye nafasi za juu za Uprofesa. Jambo la tatu, tunaendelea kusomesha Wahadhiri ndani na nje ya nchi ikiwa na lengo pana la kuhakikisha tunaongeza idadi ya watumishi au wanataaluma hawa katika vyuo vikuu. naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itaendelea kufanya mambo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika mradi wetu wa *HEET* wa miaka mitano ambao tunaendeleanao. Serikali inaenda kusomesha Wanataaluma zaidi ya 600 ambapo tunaamini kabisa katika usomeshaji huu tutaweza kupata maprofesa wengi. Kwa hiyo, nimwondoe wasiwasi juhudi hizi zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo hili la kuongeza umri kwa wanataaluma hawa hasa Maprofesa, uliongezwa kutoka miaka 60 mpaka miaka 65. Mheshimiwa Mbunge hapa anashauri kwamba tuongeza tena iwe miaka 70. Tunachukua ushauri huu, tutakwenda kuufanyia kazi tuweze kuangalia namna bora ya kufanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili kuhusu kuongeza maslahi Serikali imekuwa ikifanya hivyo. Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea na jambo hili vizuri kabisa na imeendelea kuboresha maslahi ya watumishi wakiwemo na wenzetu wanataaluma katika vyuo vikuu na tutaendelea kufanya hivyo kwa kadri ya bajeti itakavyoruhusu, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Mussa Sima.

Na. 89

**Kuboresha maslahi ya Wadhibiti Ubora nchini**

**MHE. MUSSA R. SIMA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha maslahi ya Wathibiti Ubora wa Walimu nchini ili kuinua ubora wa elimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima, Mbunge wa Singida Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza kutekeleza Muundo mpya wa Utumishi wa Maafisa Udhibiti Ubora wa Shule kuanzia Julai, 2023 ambao unatoa maslahi na motisha kwa Maafisa Udhibiti Ubora wa Shule kwa kuwaongezea Mishahara na kuwabadilishia ngazi ya mishahara kutoka *TGTS* kuwa *TGQS*. Hii ina maana kuwa kwa sasa mwalimu atakayeteuliwa kuwa Mdhibiti

Ubora lazima awe amefikia ngazi ya mshahara ya *TGTS* G pamoja na sifa nyingine za uteuzi wa viongozi wa elimu kwa kuzingatia mwongozo wa uteuzi. Aidha, maslahi mengine ni kuongeza ukomo wa ngazi ya mshahara toka *TGTS I* hadi *TGQS J* yenye maslahi makubwa kuliko awali. Muundo huo umetambua majukumu makubwa ya Wadhibiti Ubora wa Shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi ya Wadhibiti Ubora wa Shule, Serikali imefanikiwa kutoa vifaa mbalimbali vya TEHAMA kwa Wadhibiti Ubora wa Shule Tanzania Bara, ambapo vishikwambi 1,680 vilitolewa kwa Maafisa Udhibiti Ubora wa Shule, *photocopia* 234, kompyuta za mezani 769, *printer* 450 na kompyuta mpakato *(laptops)* 1,002.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali imefanikiwa kujenga ofisi tano za Wadhibiti Ubora wa Shule katika Halmashauri za Wilaya ya Njombe, Tarime, Bunda, Ubungo, na Nyasa na hivyo kufanya au kuwezesha halmashauri 181 kuwa na ofisi. Lengo ni kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sima.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa ziko fedha za uchangiaji wa elimu zinazotolewa na Serikali kupitia kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Wakuu wa Vyuo kwenda kwa Wadhibiti Ubora, fedha hizi zimekuwa na usumbufu mkubwa sana, lakini zimekuwa kero kubwa sana kwa Wakuu wa Shule pamoja na Wadhibiti Ubora. Serikali haioni haja sasa kwamba umefika wakati wa kubadilisha miongozo yake na sheria ili fedha hizi zitoke moja kwa moja Hazina na kwenda kwa Wadhibiti Ubora? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa Wadhibiti Ubora wanafanya kazi yao vizuri sana; Serikali haioni sasa umefika wakati wa kuwajengea uwezo ili kuongeza ufanisi wa kazi katika majukumu yao? Ahsante sana *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali madogo ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwenye majibu ya swali la msingi, Serikali inaendelea kufanya juhudi mbalimbali kuhakikisha kwamba Wadhibiti Ubora wanakuwa kwenye mazingira salama ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kama nilivyosema kwamba tunakwenda kubadilisha muundo wa kada hii ya Wadhibiti Ubora na sasa tunakwenda kuondoa ile Udhibiti Ubora ngazi ya kanda na kupeleka katika ngazi ya mikoa na katika kufanya hivyo tunasogeza huduma karibu zaidi ya wananchi na vilevile tunaimarisha utendaji kazi kwa ufanisi mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya haya yote, tutahakikisha vilevile katika eneo hili la uchangiaji tunaenda kulifanyia kazi ili liweze kushuka moja kwa moja kwenda Ofisi za Wadhibiti Ubora badala ya kwenda kwa Walimu Wakuu au kwenda shuleni kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la pili la utendaji kazi, tumekuwa na utaratibu wa kuhakikisha kwamba Wadhibiti Ubora wanapata mafunzo ya mara kwa mara ili kuwajengea umahiri na kuwawezesha kufanya shughuli zao za kila siku kwa ufanisi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma.

Na. 90

**Hitaji la ukarabati wa Kituo cha Polisi Bububu**

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA** aliuliza:-

Je, lini Kituo cha Polisi Bububu pamoja na nyumba za Askari vitafanyiwa ukarabati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwantakaje Haji Juma, Mbunge wa Jimbo la Bububu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imepanga kukarabati Kituo cha Polisi cha Bububu kwa awamu. Kwa awamu ya kwanza Serikali inakarabati hanga la kuishi familia 18 za askari ambalo linagharimu shilingi 19,358,450 na kwa sasa umefikia katika hatua ya umaliziaji. Baada ya awamu hii, Serikali imepanga kutumia shilingi 46,000,000 kukarabati kituo hicho pamoja na nyumba za askari katika mwaka wa fedha 2024/2025, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwantakaje.

**MHE. MWANTAKAJE HAJI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Nilikuwa na swali moja, hiki kituo ni chakavu na cha miaka mingi, miundombinu yake ni mibovu; je, Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami kwenda kujionea kituo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ama Wizara ya Mambo ya Ndani tupo tayari kuja kukagua na kuona uchakavu wa kituo hicho ili kuona namna ya kuweza kupata hizi fedha na kuanza kukifanyia ukarabati, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri.

Na. 91

**Ukarabati nyumba za makazi ya polisi Moshi Manispaa**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa nyumba za makazi ya polisi Moshi Manispaa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini kwa ajili ya ukarabati wa nyumba 147 za makazi ya askari polisi zilizoko Manispaa ya Moshi imeonesha kuwa kiasi cha shilingi bilioni 3.6 zinahitajika. Fedha hizo zinatarajika kutengwa kwa awamu kuanzia kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2024/2025 ambapo ukarabati wa nyumba 15 unatarajiwa kuanza kutekelezwa, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuwakosoa au kuwasaidia wananchi hawa ambao ni Maaskari wetu wanaofanya kazi usiku na mchana ambao wanaishi katika mazingira magumu sana, kwa kuwa nyumba zao zinavuja na miundombinu imechoka sana?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami kwenda eneo la tukio akaone hali halisi ya makazi ya maaskari wetu wanavyoishi? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Zuena Athumani kuwa Serikali inatambua uchakavu wa Vituo vya Polisi lakini pia inatambua uchakavu wa nyumba za makazi kwa ajili ya askari hawa. Aidha, Serikali inatambua juhudi na kazi kubwa inayofanywa na Jeshi la Polisi katika ulinzi na usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kwa sasa tunaenda kuzitafuta shilingi bilioni 3.6, zitakapopatikana tunaenda kuanza ujenzi wa nyumba hizo, lengo na madhumuni ni Askari wetu waweze kuishi kwenye mazingira mazuri. Aidha, nimwambie tu kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, tupo tayari kuambatana naye kwenda mpaka kwenye eneo ili kukagua na kuona uchakavu huo na kuona namna ya kuweza kuwasaidia, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Rose.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami naomba niulize swali la nyongeza. Katika Mkoa wetu wa Geita kuna nyumba nyingi sana za Askari ambazo ni chakavu; je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kukarabati nyumba hizo za askari ili askari wetu wa Mkoa wa Geita waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rose, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema hapo awali kwamba kwa sasa Serikali tunatafuta fedha na zitakapopatikana, pamoja na maeneo mengine yenye uchakavu wa nyumba na vituo, tutahakikisha kwamba Mkoa wa Geita nao tunautazama, lengo na madhumuni sasa wananchi waweze kupatiwa huduma hizo vizuri zaidi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya makazi ya polisi katika Kituo Kikuu cha Iringa Mjini ni mbaya sana na majibu ya Naibu Waziri ni kwamba mpaka fedha zitafutwe. Nilitaka kujua wale askari wataendelea kuishi wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la ulinzi na usalama katika Tanzania yetu ni jukumu la kila mtu na jukumu la kusaidia kuona kwamba huduma zinapatikana ni jukumu la Serikali lakini pia ni jukumu la viongozi. Namwomba basi angalau Mheshimiwa Mbunge naye aanze kuonesha mfano halafu sisi kama Serikali tutakuja kuongezea ili tuone namna ambavyo wananchi wanaweza kupata huduma hizo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya swali la nyongeza. Mheshimiwa Waziri katika Kituo cha Polisi Wilaya ya Rungwe Tukuyu Mjini, hawana ukuta wa kutenganisha kituo cha polisi na shule ya msingi ili kuzuia watoto wadogo kuona jinsi wahalifu wanavyopelekwa kwenye kituo.

Je, ni lini Serikali mtawajengea ukuta wa kuzunguka ili waweze kuwa katika sehemu yao binafsi pekee kama polisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mara nyingi vituo hivi tunatakiwa tuviweke katika mazingira ambayo yanaweza pengine ingawaje vinatoa huduma kwa jamii, lakini jamii isiweze kuweza kuona mambo yanayoendelea pale lakini zaidi kuweza kukitengenezea mazingira ya usalama zaidi kile kituo. Nimwambie tu Mheshimiwa Sophia kwamba tunafanya juhudi za kutafuta fedha. Tutakapopata fedha hizo, tutakwenda kujenga uzio huo ili tuweze kutenganisha hayo maeneo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, swali la Wizara ya Madini limetolewa na Mheshimiwa Mbunge, kwa hiyo halitaulizwa na wala halitajibiwa.

Wageni waliopo Bungeni asubuhi hii waliokaa Jukwaa la Spika ni wageni watatu wa Naibu Spika kutoka Jumuiya ya Kuhifadhisha Qurani Tanzania wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mambo ya Nje ya Jamii, Ndugu Saleh Omar Saleh, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni saba kutoka Bunge la Jamhuri ya Kiislam ya Iran ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Kilimo; Mheshimiwa Hossein Alvandi, Balozi wa Iran nchini Tanzania; Mheshimiwa Ranmatollah Noroz, Mkuu wa Msafara; Mheshimiwa Mohamad Rezaae, Balozi Mdogo wa Iran nchini Tanzania; Mheshimiwa Ahadi Azadikhah, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Amanolla Hosseinpoor, Mjumbe wa Kamati; Mheshimiwa Naseer Gahrewani, Afisa Itifaki wa Iran; na Mheshimiwa Fatma Mussa, mkalimani, karibuni katika Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili kutoka Bunge la Kenya; Mheshimiwa Peter Kihungi na Ndugu Wambui Nyachae, Afisa wa Bunge, karibuni kwenye Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 33 wa Mheshimiwa Omari Kipanga, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni viongozi na Wajumbe wa CCM kutoka Jimbo la Mafia. *(Makofi)*

Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Hussein Nassor, ambao ni wapiga kura wake kutoka Nyang'hwale, Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Tunao wageni 61 wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni wanafunzi na walimu wa Shule ya Msingi ya *St. Maximilian* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 43 wa Mheshimiwa Rose Busiga ambao ni UWT kutoka Nyang'hwale Mkoa wa Geita, karibuni sana na kwa kweli mmependeza sana. *(Makofi)*

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Mbarouk Nassor ambaye ni Mjumbe wa Kamati za Siasa kutoka Bumbwini Kaskazini Unguja. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Ally Makoa ambao ni viongozi wa CCM, Wilaya ya Kondoa, Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Pia wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Michael Kembaki ambaye ni mpiga kura wake na Mwenyekiti Mstaafu UVCCM kutoka Tarime, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wawili wa Mheshimiwa Jafari Wambura ambao ni wapiga kura wake kutoka Rorya, Mkoa wa Mara, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *Simba Sports Club,* Dkt. Seif Muba na Ndugu Fatma Hassan, karibuni. *(Makofi)*

Makofi yametosha kweli hayo hayo! Haya tunakwenda. *(Kicheko/Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Emmanuel Shangai ambao ni wapiga kura wake kutoka Ngorongoro Mkoa wa Arusha. *(Makofi)*

Pia wapo wageni sita wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni viongozi wa Umoja wa *AMCOS* kutoka Liwale Mkoa wa Lindi. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Abubakari Asenga ambao ni wapiga kura wake kutoka Kilombero, Mkoa wa Morogoro. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 140 na walimu watano kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana ya *St. Christina* ya Jijini Tanga, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu kutoka *Zanzibar Housing Corporation* ambao wapo Bungeni kwa ajili ya maonesho, karibuni. *(Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa Shirika la Nyumba Zanzibar wapo katika Viwanja vya Bunge kwa ajili ya maonesho ya nyumba. Waheshimiwa Wabunge wote wanakaribishwa kutembelea mabanda hayo.

Katibu.

**NDG. ASIA MINJA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja pamoja na Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Moja

pamoja na Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni, kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Maelezo ya jumla; naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, pamoja na uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika, nakushukuru wewe binafsi kwa kuelekeza Taarifa hii iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za Bunge *(Order Paper)* kwa mujibu wa kifungu cha 10(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023. Uamuzi huo unaliwezesha Bunge lako tukufu kuangalia namna madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine mbalimbali Serikalini yanavyotekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuathiri msingi huo naomba nisome taarifa hii kwa muhtasari na kuomba taarifa yote pamoja na viambatanisho vyake iingie kwenye Taarifa Rasmi za Majadiliano ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhumuni ya taarifa hii ni kubainisha matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni na kuwekwa mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge. Aidha, taarifa hii inalenga kulijulisha Bunge hatua iliyobainika kufikiwa katika utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari za sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa Shughuli za Kamati. Shughuli za Kamati zinatokana na misingi mitatu; msingi wa kwanza ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyobainisha madaraka ya kutunga sheria. Msingi wa pili ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria inayozatiti Uandishi wa Sheria za Nchi. Aidha, msingi wa tatu ni Kanuni za Bunge ambazo zinaweka utaratibu wa uendeshaji wa Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli zilizotekelezwa na kamati. Maelezo ya jumla. Shughuli zinazotekelezwa na kamati zinahusu maeneo makuu mawili. Kwanza, ni Uchambuzi wa Sheria Ndogo na pili ni Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Aidha lengo la kuchambua taarifa za utekelezaji ni kuliwezesha Bunge kubaini hatua zilizofikiwa katika kurekebisha dosari za sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo. Sheria ndogo 192 ziliwasilishwa mezani tarehe 7 Februari, 2023 kwenye Kikao cha Sita wakati wa Mkutano wa Kumi wa Bunge. Aidha, tarehe 12 Aprili, 2023 kwenye Kikao cha Tano, wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Serikali iliwasilisha sheria ndogo 232. Baada ya hatua hiyo Kamati ilichambua sheria ndogo hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa lengo la kujiridhisha iwapo sheria ndogo hizo zina masharti yanayokinzana na Katiba ama Sheria Mama au sheria nyingine za nchi. Aidha, kamati ilitaka kubaini iwapo sheria hizo, zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria au zina masharti yasiyo na uhalisia, ama zina majedwali yenye dosari za hitilafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha kuwa sheria ndogo tatu zina masharti ya makinzano ya Katiba na mbili zina masharti ya makinzano ama Sheria Mama au sheria nyingine za nchi. Vilevile sheria ndogo sita zina makosa ya kutoendana na misingi wa uandishi na sheria mbili zina dosari ya kutokamilika kwa majedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuwezesha Bunge kuamua inavyostahili naomba kufafanua dosari hizo. Dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba. Kwa kuwa Sheria Mama hazipaswi kukinzana na Masharti ya Katiba, haitarajiwi sheria ndogo ikinzane na Katiba. Hata hivyo Kamati imebaini sheria ndogo zenye dosari hiyo, mfano ni *The Whistleblower and Witness Protection Regulations, 2023.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya 5(4) ya Sheria Ndogo hiyo inampa haki ya kukata rufaa mtoa taarifa ambaye maombi

yake ya kupatiwa ulinzi yamekataliwa. Kwa mujibu wa Kanuni hiyo, mtoa taarifa asiporidhika na uamuzi huo anapaswa kuwasilisha rufaa yake kwa Waziri ndani ya siku kumi na nne. Dosari ya Kanuni hii ni kutokuonesha muda ambao Waziri atashughulikia rufaa hiyo. Dosari ina sura ya kubariki ucheleweshaji wa mashauri ya rufaa, jambo ambalo ni kinyume na Ibara ya 107A ya Katiba. Kwa masharti ya ibara hiyo, mamlaka zote za utoaji wa haki hazipaswi kuchelewesha haki bila sababu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na Sheria Mama au Sheria nyingine za Nchi. Lengo la Bunge kukasimu madaraka yake ni kuwezesha utekelezaji wa sheria mama. Hivyo sheria ndogo inayokiuka masharti ya Sheria Mama imevuka mipaka. Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria kinakataza sheria ndogo kukinzana na Sheria Mama au sheria nyingine ya nchi. Licha ya masharti hayo Kamati imebaini sheria ndogo mbili zina dosari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya sheria ndogo zenye dosari hiyo ni *The Law School of Tanzania (Admission, Fees and Conduct of Practical Training) Rules, 2022*. Dosari ya sheria ndogo hiyo ni jedwali la kwanza kuonesha ada ya programu ya mafunzo maalum kwa Wasaidizi wa Sheria kinyume na masharti ya kifungu cha 2 cha *The Law School of Tanzania Act* ambayo ni sheria mama. Kifungu hicho kinachohusu matumizi ya Sheria Mama hakiwajumuishi wasaidizi wa sheria, hivyo jedwali limevuka mawanda, jambo ambalo ni kinyume na masharti ya kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria; misingi ya uandishi wa sheria, imewezesha sheria kufanikisha hatua za Serikali kisera, kueleweka kwa urahisi miongoni mwa wananchi wanaozisimamia na wanaozitafsiri. Bunge linapotunga sheria huzingatia misingi ya uandishi ambayo huwezesha mawazo ghafi kuwepo katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana halisi kutekelezeka. Kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria nchini inaliwezesha Bunge kuzingatia misingi ya Uandishi wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, iwapo Bunge lenye mamlaka kamili ya utungaji wa sheria linazingatia misingi ya uandishi, sheria ndogo zinatokana na Sheria za Bunge zinapaswa kuzingatia ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria. Hata hivyo, Kamati imebaini sheria ndogo sita zenye dosari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa sheria ndogo hizo ni Kanuni za Mawasiliano za Kielektroniki ya Posta kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023; Kanuni ya 10(a) inavyoweka utaratibu wa kusajili laini za simu kwa watoto ina dosari ya kiuandishi. Dosari iliyopo ni kumlazimisha mzazi au mlezi anayetaka kusajili laini ya mtoto, awasilishe kwa pamoja nakala ya cheti cha kuzaliwa kwa mtoto, nakala ya cheti cha kuasili mtoto, hati halali ya kusafiria pamoja picha ya mtoto anayehusika. Kwa masharti hayo mtoto anayekosa moja kati ya nyaraka hizo hataruhusiwa kusajili laini ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya uandishi wa majedwali. Madhumuni ya majedwali ni kukamilisha masharti ya kifungu cha sheria inayohusika hivyo, dosari yoyote ya jedwali inakwamisha sheria inayohusika, kama imebainika kuwa sheria ndogo mbili zina dosari ya uwandishi wa majedwali. Mojawapo ya sheria ndogo hizo ni Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu kuingia Ndani ya Nchi na kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, jedwali la pili la kanuni hizi limewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya Sita; kanuni hiyo inaanzisha vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu kuingia ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi. Uchambuzi umeonesha kuwa jedwali hilo lina hitilafu kwa kutokutaja maeneo mengine ambayo yanatumika kuingia ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo hayakutajwa ni bandari zote zilizoko katika Ziwa Nyasa, Ziwa Victoria na viwanja vya ndege. Kutokutambuliwa kwa maeneo haya katika jedwali ni mwanya unaoweza kutumika kupitisha mazao ya misitu hayo bila kukaguliwa. Uwezekano huo unafifisha lengo la Sheria ya Misitu ambayo ni usimamizi wa misitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge linapokasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine halitarajii mamlaka hizo zitatunga sheria ndogo zinazokiuka masharti ya katiba zinazokinzana na Sheria Mama au sheria nyingine za nchi, zisizoendana na misingi ya uandishi wa sheria na zisizozingatia uhalisia na uandishi bora wa majedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge likibaini dosari hizo na kuzifumbia macho litakuwa liomeruhusu mamlaka hizo zikiuke katiba au madhumuni ya Bunge lenyewe. Kwa kuwa utungaji wa sheria za nchi ni mamlaka ya Bunge linalazimu mjadala wa leo uhitimishwe kwa kusisitiza marekebisho ya dosari 29 zilizobainika katika sheria ndogo sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Ni wajibu wa Bunge kuhakikisha kwamba madaraka yake ya kutunga sheria yanatumika inavyostahili. Kwa kuwa Kamati ya Sheria Ndogo inasimamia madaraka ya kutunga sheria ndogo ilitaka kujiridhisha iwapo dosari zilizobainishwa zimerekebishwa kwa namna inavyoazimiwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini mambo makuu manne yanayohusu hatua ya utekelezaji; Jambo la kwanza, ililenga kubaini iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio na; la pili, ilikusudia kuona iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara. Katika jambo la tatu, kamati ilitaka kujiridhisha iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya rasimu ya marekebisho kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki. Jambo la nne. lilihusu kubainisha iwapo utekelezaji wa maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa kutoka Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi yanaonesha hatua nne zilizofikiwa na mamlaka mbalimbali. Hatua hizo ni maazimio kuhusu dosari 19 kutokuwa kumetekelezwa na maazimio kuhusu dosari tatu kutekelezwa kwa hatua ya rasimu ya marekebisho katika ngazi za Wizara. Vilevile matokeo yamebainisha maazimio kuhusu dosari 15 kufikia hatua ya rasimu ya marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria

Mkuu wa Serikali kwa uhakiki wakati maazimio ya dosari 46 kufikia hatua ya mwisho ya marekebisho kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufafanuzi wa hatua zilizofikiwa umewekwa katika jedwali la uchambuzi ambalo ni kiambatanisho namba mbili cha taarifa. Naomba kueleza hatua hizo angalau kwa muhtasari ili kuliwezesha Bunge kupata taswira halisi. Maelezo ya hatua hizo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Maazimio ya Bunge kutokuwa yametekelezwa; kutokana na uchambuzi Kamati imebaini kuwa, maazimio kuhusu dosari 19 kati ya 83 ambazo ni sawa na 22.89% ya dosari zote hayajatekelezwa. Mchanganuo wa maazimio hayo unaonesha kuwa maazimio kuhusu dosari 16 yanagusa sheria ndogo zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na maazimio kuhusu dosari tatu yanagusa sheria ndogo inayosimamiwa na Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya maazimio hayo ambayo hayajatekelezwa yapo yanayohusu dosari katika sheria ndogo tisa zinazosiomamiwa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI; dosari hizo zinawagusa na kuwaathiri moja kwa moja wananchi katika ngazi za Halmashauri za Wilaya ya Ikungi, Mji wa Bunda, Wilaya ya Msalala, Wilaya ya Mvomero, Manispaa ya Temeke, Wilaya ya Nsimbo na Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hiyo wananchi wanaendelea kuathiriwa na dosari zilizobainika, kwa mfano wa dosari zinazoendelea kuwaathiri wananchi kutokana na kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge ipo katika sheria ndogo ya usafi wa mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ya mwaka 2023, kifungu cha 22(2) cha sheria ndogo hizi kinaweka adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayevunja masharti ya sheria ndogo hii. Kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi 200,000 au kifungo cha miezi 12 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, adhabu hiyo inatofautiana na adhabu ya jumla inayowekwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria Ndogo hiyo. Kwa mujibu wa kifungu hicho adhabu ya jumla kwa

kosa la kukiuka Masharti ya Sheria Ndogo hiyo ni faini isiyopiungua shilingi 50,000 au kifungo kisichopungua miezi 6 au adhabu zote mbili kwa pamoja. Mkinzano huo wa adhabu unaendelea kuwepo kutokana na mamlaka inayohusika kutokutekeleza Maazimio ya Bunge. Athari yake katika maisha ya watu ni kuendelea kupata madhara ya mkanganyiko wa adhabu jambo ambalo halikuwa dhamira ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya rasimu ya marewkebisho katika ngazi ya Wizara; hatua ya rasimu ya marekebisho kuwa katika ngazi ya Wizara, inaonesha kutokukamilika kwa utekelezaji wa maazimio. Hali hiyo inaendeleza dosari zilizobainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari tatu za sheria ndogo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira yapo katika hatua hiyo. Dosari zilizobainishwa zipo katika sheria ndogo ya *The Environmental Management (Control and Management of Carbon Trading) Regulations, 2022*. Sheria ndogo hii ilibainika kuwa na dosari katika sehemu c ya jedwali la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari iliyopo ni kutoka kiwango cha gharama za mradi zikiwemo gharama za maandalizi, gharama za uanzishaji na gharama za jumla ya kipimwe cha thamani kuanzia dola za Marekani 1,000,000. Kutokukamilika kwa marekebisho ya dosari hiyo kunaendeleza changamoto ya kutowajumuisha watu wenye mitaji iliyochini ya dola 1,000,000 za Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya rasimu ya marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; hatua ya rasimu ya marekebisho yaliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni muhimu. Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari 15 katika sheria ndogo sita upo hatua hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo unaonesha kuwa dosari nane za sheria ndogo tatu zilizosimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Aidha, dosari nne ni za sheria ndogo mbili

zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na dosari tatu zinahusu sheria ndogo moja inayosimamiwa na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya sheria ndogo zipo sheria ndogo tatu zinazowagusa moja kwa moja wananchi wa Halmashauri za Mji wa Bunda, Wilaya ya Nsimbo na Wilaya ya Misungwi. Vilevile zipo kanuni mbili zinazosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muunganio na Mazingira ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua za marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Marekebisho ya Sheria ndogo kutangazwa katika Gazeti la Serikali ni hatua inayokamilisha utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kwa hatua hii mamlaka zinazohusika zinakuwa zimesahihisha dosari zilizobainishwa. Kamati imebaini kuwa dosari zilizorekebishwa kufikia hatua hiyo ziko kwenye sheria ndogo ishirini na tatu. Katika sheria ndogo hizo, kumi na nane zinasimamiwa na Ofisi ya Rais TAMISEMI, mbili zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na tatu zinasimamiwa na iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa sheria ndogo unajumuisha kufuatilia utekeleaji wa maazimio kuhusu dosari zilizobainishwa. Utaratibu huo ni muhimu kwa uzingatiaji wa mgawanyo wa madaraka. Katika kufanya hivyo mamlaka zilizochelewa kutejkeleza maazimio zinapaswa kuhimizwa. Aidha, mamlaka zilizofikia hatua ya mwisho ya kurekebisha dosari zinastahili pongezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo, maelezo ya jumla. Msingi wa mapendekezo ya Kamati unatokana ana dosari zilizobainika kuathiri tija ya Bunge ya kukasimu madaraka ya kutunga sheria ndogo. Aidha, athari za dosari hizo ni kusababisha ugumu wa kueleweka kwa sheria na kuzalisha kero kwa mwananchi kutokana hitilafu katika sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, madhara mengine ni uwezekano hafifu wa kutimia kwa lengo la sheria zilizotungwa na Bunge na

kuendelea na desturi isiyofaa kutokana na utaratibu wa sheria za nchi. Hivyo Kamati inapendekeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya Katiba; kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kukinzana na Masharti ya Katiba, suala ambalo ni kinyume na misingi ya sheria inayotambua ukuu wa katiba,

Na kwa kuwa ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria yoyote ni kinyume na Ibara ya 64(5), Bunge haliwezi kutunga sheria hiyo iliyo kinyume na Katiba na wala kukubali madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine, yatumike katika kutunga sheria yenye dosari inayokinzana na Katiba,

Kwa hiyo basi Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari hiyo ya kukinzana na Masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ili kutatua dosari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari ya kuwa na masharti yanayokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi.

Kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zina dosari ya kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa sheria mama inayohusika;

Na kwa kuwa dosari ya sheria ndogo kukinzana na masharti ya sheria mama au kukinzana na masharti ya sheria nyingine za nchi;

(a) Ni changamoto isiyostahili kuendelea kuwepo kutokana na kutoendana na masharti yaliyowekwa na mamlaka kuu ya kutunga sheria katika sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1;

(b) Ni dosari inayotokana na kukiuka masharti ya madaraka ya Bunge yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na sheria hiyo, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge; na

Na kwa kuwa dosari ya sheria ndogo kukinzana na masharti ya sheria mama au kukinzana na masharti ya sheria nyingine za nchi:-

(a) Ni changamoto isiyostahili kuendelea kuwepo kutokana na kutoendana na masharti yaliyowekwa na mamlaka kuu ya kutunga sheria katika sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza,

(b) Ni dosari inayotokana na kukiuka masharti ya madaraka ya Bunge yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine inayohusika na sheria hiyo, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge,

(c) Ni dosari inayotosha kubatilisha sheria ndogo zinazohusika kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya Kwanza, jambo ambalo ni kinyume na madhumuni ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka nyingine Serikalini,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya sheria mama na sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

Kwa kuwa baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari za kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria, jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya Bunge,

Na kwa kuwa dosari hizo:-

(a) Zinaathiri azma ya Bunge kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera kupitia sheria za Bunge na sheria ndogo,

(b) Zinakwamisha nia ya Bunge kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni wa wadau, wakiwemo watu

wengine ambao ni watekelezaji wa sheria na wanaoguswa sheria hizo,

(c) Ni ukiukaji wa misingi ambayo Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria halipaswi kuikiuka,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wa uandishi wa majedwali wenye dosari.

Kwa kuwa zipo sheria ndogo zilizochambuliwa na kubainika kuwa na dosari ya kuwa na majedwali yenye hitilafu za uandishi, jambo linaloathiri lengo la sheria ndogo inayohusika,

Na kwa kuwa athari ya dosari hiyo:-

(a) Inasababisha changamoto katika utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika katika jambo ambalo halikuwa lengo la Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine,

(b) Ni pamoja na kufifisha madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa kwa ufafanuzi wa sheria ndogo,

(c) Haiwezi kuvumiliwa na Bunge ambalo hukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine Serikalini,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye dosari za uandishi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari zilizobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa maazimio kuhusu sheria ndogo zilizobainika kuwa na dosari.

Kwa kuwa dosari zote zilizobainika katika uchambazi kama inavyoonekana katika Jedwali la Uchambuzi, Kiambatisho Na. 01, zinahitaji kurekebishwa inavyostahili.

Na kwa kuwa:-

(a) Dosari hizo zisiposahihishwa zitaendelea kuwa na madhara ambayo yametokana na matumizi ya madaraka ya kutunga sheria ndogo yaliyokasimiwa kwa mamlaka zinazohusika,

(b) Bunge ambalo ndilo mamlaka kuu ya kutunga sheria ambayo ina dhima ya kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi hazina dosari na wala hazisababishi kero kwa wananchi,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho cha 01 cha Taarifa hii, ziwasilishe taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo tarehe 02 Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokutekelezwa kwa Maazimio.

Kwa kuwa, Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari 19 za sheria ndogo 10 kama ilivyobainika wakati wa uchambuzi ni jambo linalokwamisha azma ya Bunge kuondoa changamoto zitokanazo na dosari hizo,

Na kwa kuwa, kuendelea kuwa na dosari 19 za sheria ndogo 10 zilizobainishwa:-

(a) Ni kukumbatia athari ya dosari hizo katika utekelezaji wa sheria na kuafiki changamoto zinazoweza kutokana na dosari hizo,

(b) Ni kubariki matumizi mabaya ya madaraka ya kufafanua sheria yaliyokabidhiwa na Bunge kwa mamlaka zinazohusika bila kujali madhara yake kwa wananchi,

(c) Ni jambo linalohitaji kuzuiwa na Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze Maazimio hayo na kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wake kwa Katibu wa Bunge, ifikapo tarehe 02 Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchelewaji katika kutekeleza maazimio ya kurekebisha sheria ndogo:-

Kwa kuwa, Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kusababisha kero kwa wananchi.

Na kwa kuwa, kutokutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo ni jambo ambalo:-

(a) Linalocheleweshа utatuzi wa kero za wananchi wanaolitegemea Bunge kusimamia maslahi yao,

(b) Halipaswi kuridhiwa na Bunge ambalo ni chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi chenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma,

Kwa hiyo basi, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizochelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kuwasilisha kwa Katibu wa Bunge, ifikapo tarehe 2 Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, shukrani; napenda kutumia nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Spika na kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua sheria ndogo na Taarifa ya Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Kwa heshima kubwa naomba majina yao yaingie kwenye Taarifa Rasmi ya Shughuli za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa moyo wa dhati nimshukuru Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge, Waziri wa Nchi, Ofisi ya

Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwa uratibu ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati kwa kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushiriki katika vikao vya uchambuzi wa sheria ndogo na vikao vya kupokea taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Nawashukuru pia, watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc,* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja. Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI KUHUSU UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA KUMI NA MKUTANO WA KUMI NA MOJA, PAMOJA NA UCHAMBUZI WA TAARIFA ZA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KWENYE MKUTANO WA NANE NA MKUTANO WA TISA – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, naomba kuwasilisha Taarifa ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge; pamoja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Naanza kwa kukushukuru wewe binafsi kwa kuelekeza Taarifa hii iwekwe kwenye Orodha ya Shughuli za leo za Bunge (*Order Paper*) kwa mujibu wa Kifungu cha 10(3) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Uamuzi huo unaliwezesha Bunge lako tukufu kuangalia namna madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali serikalini yanavyotekelezwa.

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya Taarifa hii ni kubainisha matokeo ya uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni na kuwekwa Mezani wakati wa Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge. Aidha, Taarifa hii inalenga kulijulisha Bunge hatua iliyobainika kufikiwa katika utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari za sheria ndogo zilizowalishwa wakati wa Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa Taarifa hii ni nyenzo ya kulisaidia Bunge kujadilili utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga Sheria, naomba kutanguliza maelezo ya awali kuhusu muundo wa Taarifa hii ili kurahisisha ufuatiliaji wa maudhui. Kwa kufanya hivyo, mawanda na mtiririko utakuwa bayana na rahisi kwa majadiliano ili hatimaye Bunge liamue inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa madhumuni hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza ni ya utangulizi ambayo inatoa maelezo ya jumla. Lengo lake ni kujenga msingi wa maudhui ya Taarifa hii kwa ajili ya majadiliano ya Bunge;

(b) Sehemu ya Pili inahusu ufafanuzi wa shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi kinachohusika. Lengo lake ni kutoa maelezo kuhusu shughuli hizo, msingi wake na mambo yaliyobainika;

(c) Sehemu ya Tatu inafanya majumuisho ya maoni kutokana na shughuli zilizotekelezwa. Lengo lake ni kuweka msingi wa

mapendekezo katika hoja ya Kamati inayojadiliwa Bungeni leo; na

(d) Sehemu ya Nne na ya mwisho inahitimisha hoja ili kuliomba Bunge lifanye uamuzi stahiki. Lengo lake ni kumalizia wasilisho na kutoa fursa kwa Bunge kuanza mjadala.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ajili ya kumbukumbu na rejea inayotokana na majadiliano ya hoja hii ya Kamati ya Sheria Ndogo, naomba Bunge liipokee na kuijadili Taarifa hii pamoja na viambatisho vyake viwili ambavyo navyo vinastahili kuingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Viambatisho hivyo ni:

**Kwanza: Kiambatisho Na. 1** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja; na

**Pili: Kiambatisho Na. 2** ambacho ni Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

**Mheshimiwa Spika**, Viambatisho hivyo, vimetoa ufafanuzi wa kina unaodhihirisha maeneo muhimu yatokanayo na uchambuzi. Hivyo, kubainisha msingi wa mapendekezo yanayolenga kutimiza lengo la Bunge kukabidhi madaraka yake ya kutunga sheria kwa mamlaka nyingine serikalini.

### 1.3 Msingi wa Shughuli za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli zote za Kamati hii zinatokana na masharti yaliyofafanuliwa katika misingi ifuatayo:-

#### 1.3.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977

**Mheshimiwa Spika**, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ni msingi wa kwanza. Ibara ya 4 (1) ya Katiba hiyo imelitambua Bunge kuwa mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma. Aidha, kwa mujibu wa Ibara ya 97 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Bunge halizuiwi kukabidhi kwa mtu yeyote au kwa idara yoyote ya

Serikali madaraka ya kuweka Kanuni zenye nguvu ya kisheria au kuzipa nguvu ya kisheria Kanuni zozote zilizowekwa na mtu yeyote au Idara yoyote ya serikali.

**1.3.2 Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.1*)**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1 (*The Interpretation of Laws Act, Cap.1*) ina lengo la kuzatiti sheria kuhusu muundo wa uandishi, kuweka mwongozo kuhusu tafsiri na matumizi ya sheria zote za nchi pamoja na mambo mbalimbali kuhusiana na hayo. Kwa sababu hiyo, muundo wa uandishi na mchakato wa sheria ndogo unapaswa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

**1.3.3 Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023**

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni za Kudumu za Bunge zinazotokana na Ibara ya 89 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zimeweka mwongozo kuhusu utaratibu, desturi na uendeshaji wa shughuli za Bunge ikiwemo kuainisha majukumu ya Kamati hii na masharti ya utekelezaji wa majukumu hayo. Kifungu cha 10 (1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kimefafanua majukumu ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo ndio kiini cha taarifa hii.

**1.4 Njia na Mbinu Zilizotumika**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 142 (a) ambayo pamoja na mambo mengine inaweka sharti la Taarifa ya Kamati kubainisha njia au mbinu zilizotumika, naomba kulijulisha Bunge kwamba, Kamati ilitumia njia na mbinu zifuatazo: -

(a) Kupitia Magazeti ya Serikali yaliyowasilishwa Mezani kwa lengo la kupata orodha na jumla ya sheria ndogo zote. Mbinu hiyo iliiwezesha Kamati kubaini mwelekeo, wigo wa kazi ya uchambuzi na sekta zinazohusika;

(b) Kufanya uchambuzi wa awali wa sheria ndogo ili kubaini masharti yanayowekwa na Sheria hizo. Mbinu hiyo, ilisaidia maandalizi ya maeneo ya kufanyia udadisi kuhusu uzingatiaji wa masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria zingine za Nchi;

(c) Kuhakiki mtiririko wa maudhui kwa kulinganisha masharti yanayowekwa katika sheria ndogo. Mbinu hii ilifanikisha dhamira ya Kamati kubaini iwapo kuna ukamilifu uliokusudiwa na Bunge wakati wa kukasimu madaraka ya ufafanuzi uliotakiwa kufanywa na sheria ndogo inayohusika;

(d) Kuoanisha masharti ya Sheria Ndogo inayohusika na misingi iliyowekwa katika Katiba na Sheria Nyingine za nchi. Nia ni kujiridhisha na ukubalifu wa Sheria Ndogo kwa misingi ya Sheria za nchi inayopaswa kuzingatiwa;

(e) Kurejea madhumuni ya Sheria Kuu iliyoruhusu kutungwa kwa sheria ndogo na kupima iwapo maudhui ya sheria ndogo yanaweza kufanikisha madhumuni ya Sheria Kuu. Mantiki ya mbinu hii inatokana na umuhimu wa Bunge kujiridhisha iwapo sheria ndogo inafanikisha nia ya Bunge kutunga Sheria Kuu na kukasimu madaraka ya ufafanuzi; na

(f) Kufanya mahojiano na mamlaka zilizotunga sheria ndogo kwa idhini ya Bunge. Mbinu hii ililenga kuiwezesha Kamati kupima uthabiti wa hoja dhidi ya ufafanuzi wa mamlaka zinazohusika na hatimaye kupendekeza maazimio ya Bunge yenye kufaa na yanayotekelezeka.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa mbinu hizo kwa ujumla wake, ziliiwezesha Kamati kubaini mambo mbalimbali yenye misingi na vigezo vya kuthibitisha ukweli au uthabiti wa maoni ya Kamati ambayo ni msingi wa maazimio ya Bunge yanayopendekezwa katika taarifa hii. Niwashukuru Mawaziri waliohusika na sheria ndogo katika kipindi hicho, kwa kutoa ushirikiano mkubwa ambao uliiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ya uchambuzi wa Sheria Ndogo na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inalenga kulijulisha Bunge kuhusu shughuli za Kamati na matokeo yake yanayohitaji uamuzi wa Bunge. Shughuli hizo zilihusu maeneo makuu ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Maeneo hayo ni:-

(a) Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja; na

(b) Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Sheria Ndogo unatokana na Bunge kuwa Mamlaka Kamili ya Kutunga Sheria kama inavyotambulika kwenye Katiba, lakini likaamua kukasimu kwa Mamlaka ya Utendaji (*Executive*), uwezo wa kufafanua sheria linazozitunga. Utaratibu huo wa mabunge duniani kukasimu madaraka ya kutunga sheria (*legislative power*) unatokana na ongezeko la shughuli za serikali katika muktadha wa demokrasia kwa dunia ya leo.

**Mheshimiwa Spika**, Mtazamo huo wa uhusiano kati ya mamlaka za nchi, hauliondoi Bunge ambalo ni wakala wa wananchi kwenye kuhakikisha kuwa, sheria zote za nchi zinawezesha ustawi wao. Nchini Tanzania, kama ambavyo imeelezwa hapo awali, Katiba inaonesha kuwa lengo kuu la Serikali inayopata madaraka na mamlaka kutoka kwa wananchi ni ustawi wa wananchi. Bunge ambalo ni mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia shughuli za umma kwa niaba ya wananchi, linapaswa kujiridhisha na namna sheria zinavyofanikisha ustawi wa wananchi. Wajibu huo unalitaka Bunge kujiridhisha iwapo madaraka ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine, yanatumika inavyostahili. Msingi huo ndio kiini cha shughuli za uchambuzi wa sheria ndogo kila zinapowasilishwa mezani.

**Mheshimiwa Spika**, Katika utaratibu wa utekelezaji bora wa madaraka ya Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria

Ndogo ni karakana ya uchambuzi wa Sheria Nodgo. Aidha, Kamati hii ni nyenzo ya Bunge katika kubaini, iwapo maudhui ya sheria ndogo yanaweka masharti na taratibu zinazowezesha ustawi wa wananchi kwa namna iliyokusudiwa na Bunge. Katika kutimiza azma ya Bunge, uchambuzi unaofanywa na Kamati unalenga kuliwezesha Bunge kuondoa uwezekano wa matumizi yasiyo na mantiki (*arbitrary use of power*) au mabaya (*abuse of power*) ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa Mamlaka ya Utendaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kama ilivyo ada, Bunge hufanyia kazi matokeo ya uchambuzi wa sheria ndogo kwa utaratibu wa hoja kutolewa, kuungwa mkono na kujadiliwa. Utaratibu huo unaliwezesha Bunge kuzingatia mambo yanayohusu sheria ndogo ambayo yameibuliwa na Kamati au yameibuka wakati wa mjadala na kuamua kwa njia ya matamko rasmi yanayotaka utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria kwa namna Bunge linavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba, madaraka yake ya kutunga sheria yanazingatiwa inavyostahili, Bunge linapaswa kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari zinazobainishwa katika sheria ndogo. Lengo la kufanya hivyo ni kuwezesha nafuu baada ya madhara ya dosari zilizobainika.

### 2.1.1 Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 07 Februari, 2023 kwenye Kikao cha Sita, wakati wa Mkutano wa Kumi wa Bunge, Jumla ya Sheria Ndogo mia moja na tisini na mbili (192) zikiwa na Nyongeza ya matoleo ya Magazeti ya Serikali ziliwasilishwa Mezani.[1]Aidha, Tarehe 12 Aprili 2023 kwenye Kikao cha Tano, wakati wa Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge, Serikali iliwasilisha jumla ya sheria ndogo mia mbili thelathini na mbili (232).[2] Nilikumbushe Bunge lako kuwa hati za kuwasilishwa Mezani kwa upande wa sheria ndogo ni desturi inayolipa Bunge fursa ya kusajili sheria ndogo hizo kwa hatua zake muhimu.

---

[1] Taz. Kumbukumbu Rasmi za Majadiliano ya Bunge, tarehe 7 Februari, 2023

[2] Taz. Kumbukumbu Rasmi za Majadiliano ya Bunge, tarehe 12 Aprili, 2023

**Mheshimiwa Spika**, Hatua za Bunge kwa Sheria Ndogo zinazowekwa Mezani ni kuziingiza kwenye karakana yake ya sheria ndogo ambayo ni Kamati hii. Kwa madhumuni ya kufanikisha azma ya Bunge kutunga sheria za nchi zenye misingi sahihi na madhubuti, Kamati ilitekeleza jukumu lake la uchambuzi wa sheria hizo kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Ili kukidhi masharti hayo, Kamati ililenga kujiridhisha na mambo yafuatayo:-

(a) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(b) Iwapo sheria ndogo zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi;

(c) Iwapo sheria ndogo zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi;

(d) Iwapo sheria ndogo zina masharti yasiyo na uhalisia kwa kiasi cha kusababisha changamoto katika utekelezaji wake; na

(e) Iwapo sheria ndogo zina majedwali yenye dosari kwa-

(i) kutofautiana na vifungu vya sheria ndogo vinavyoyaanzisha au:

(ii) kutokamilika ilivyostahili au;

(iii) kutajwa katika sheria ndogo inayohusika lakini yanakosekana; na

(iv) kujitokeza bila kuwa na kifungu cha sheria ndogo inayoyaanzisha.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa hii inaweka wazi mambo yaliyobainika katika maeneo hayo yaliyotajwa. Ufafanuzi wa mambo hayo utaliwezesha Bunge lako kusimamia ipasavyo madaraka yake ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine serikalini.

### 2.1.2 Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo thelathini na moja (31) zilizowasilishwa Bungeni tarehe 20 Septemba 2022 wakati wa Kikao cha Sita kwenye Mkutano wa Nane;[3] na tarehe 07 Novemba 2022 kwenye Kikao cha Sita, Mkutano wa Tisa.[4] Madhumuni ya ufuatiliaji huo ni kubaini hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa uamuzi wa Bunge kuhusu mamlaka yake ya kutunga sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la kuchambua Taarifa za Utekelezaji ni kujiridhisha iwapo hatua stahiki za utekelezaji wa mamlaka ya kutunga sheria zimefikiwa. Mantiki yake inatokana na umuhimu wa Bunge kutekeleza jukumu la kutunga sheria bila kusahau wajibu wake kikatiba kuhusu sheria za nchi. Kamati hii ilikusudia kuliwezesha Bunge kufuatilia utekelezaji wa mamlaka yake katika eneo la sheria ndogo. Hivyo, kuna umuhimu wa kuripoti matokeo ya ufuatiliaji huo.

**Mheshimiwa Spika**, Nilikumbushe Bunge lako tukufu kuwa, Matokeo ya ufuatiliaji wa Maazimio kuhusu sheria ndogo hizo yaliwasilishwa Bungeni tarehe 8 Februari, 2023 wakati wa Kikao cha Sita, kwenye Mkutano wa Kumi wa Bunge.[5] Wasilisho hilo lilibainisha dosari mbalimbali sanjari na kuonesha madhara yake dhidi ya misingi ya sheria na ustawi wa watu uliosisitizwa katika Ibara ya 8 (1) (b) ya Katiba.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa maazimio unalibainishia Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria, hatua iliyofikiwa dhidi ya hatua iliyostahili katika kurekebisha sheria ndogo. Nia ni kuona jinsi madaraka ya Bunge ya kutunga sheria chini ya mamlaka nyingine yanavyozingatia azma ya Bunge lenye dhamana ya sheria za nchi. Maoni ya Kamati kutokana na uchambuzi huo yanaweza kutengeneza msingi wa mjadala na uamuzi wa Bunge kutathmini madaraka yake yanavyotumika.

---

[3] Taz. Kumbukumbu Rasmi za Majadiliano ya Bunge, tarehe 20 Septemba 2022

[4] Taz. Kumbukumbu Rasmi za Majadiliano ya Bunge, tarehe 07 Novemba 2022

[5] Taz. Kumbukumbu Rasmi za Majadiliano ya Bunge, tarehe 7 Februari, 2023

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge yaliyotajwa ulikamilishwa kwa kufuata hatua zifuatazo:-

(a) Kupokea Taarifa za Utekelezaji kabla ya kukutana na mamlaka zilizohusika ili kuoanisha utekelezaji na Maazimio yaliyopitishwa na Bunge, Lengo ni kubaini iwapo kuna mkwamo au kusuasua katika utekelezaji;

(b) Kuoanisha hatua ya utekelezaji na madhara ya dosari au hitilafu yaliyonusurika. Lengo ni kulionesha Bunge iwapo utekelezaji umeendana na matarajio yake; na

(c) Kukutana na mamlaka zinazohusika ili kupata ufafanuzi wa kina kuhusu mashaka ambayo yalipatikana wakati wa uchambuzi wa taarifa hizo. Lengo ni kuzingatia utaratibu mzuri wa misingi ya asili kisheria ili kufikia msimamo wa kutumainiwa juu ya jambo linalohusika.

**Mheshimiwa Spika**, hatua hizo zimechangia uthabiti wa matokeo ya uchambuzi yaliyotolewa taarifa hapo awali na mengine yanayoripotiwa leo hii. Utaratibu huu unaostahili kuendelezwa ili kuwawezesha wananchi kupata tija ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge ambalo, kimsingi ni chombo chao cha uwakilishi.

**2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa sheria ndogo umefanyika ili kufanikisha wajibu wa Bunge kudhibiti mamlaka yake ya kutunga sheria. Kwa desturi za uendeshaji wa Bunge hili, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo imekuwa injini ya Bunge lako katika udhibiti wa sheria ndogo. Nafasi ya Kamati katika dhima hiyo ni kuchambua, kubainisha dosari na kulishauri Bunge juu ya hatua za kuchukua.

**Mheshimiwa Spika,** Maelezo hayo yanaonesha ulazima wa Kamati kuripoti matokeo ya uchambuzi Bungeni. Bila kufanya hivyo haitakuwa rahisi kwa Bunge kudhibiti mamlaka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine nchini. Ikiwa hivyo, Bunge ambalo limepewa mamlaka na majukumu

kwa niaba ya wananchi, litakuwa limeshindwa kutekeleza madaraka yake na kutumia mamlaka lililonayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sheria ndogo zilizochambuliwa, naomba kulihakikishia Bunge lako tukufu kuwa, matokeo ya uchambuzi yanayowasilishwa leo hii, yameainishwa kwa namna rahisi kwa Bunge kuona hatua stahiki dhidi ya dosari. Kwa urahisi wa kufuatilia, Jedwali la Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge linaambatishwa na kuwa **Kiambatisho Na.1**. Naomba Jedwali hilo lisomwe kwa pamoja na taarifa hii na kuingizwa kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* likiwa ni sehemu ya taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, Dosari zinazobainishwa katika Jedwali hilo zinajitokeza sheria ndogo zaidi ya moja. Kwa sababu hiyo, idadi ya dosari na hitilafu haitalingana na jumla ya idadi ya sheria ndogo. Kwa ujumla Sheria ndogo zenye dosari zimechanganuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Sheria ndogo tatu (03) zina masharti yanayokinzana na Katiba;

(b) Sheria ndogo mbili (02) zina masharti yanayokinzana na Sheria Mama na sheria nyingine za nchi;

(c) Sheria ndogo sita (06) zina makosa ya kutoendana na misingi ya uandishi; na

(d) Sheria ndogo mbili (02) zina dosari ya kutokamilika kwa majedwali ambapo, hayajajumuisha baadhi ya mambo muhimu yanayopaswa kujumishwa katika Majedwali hayo.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa kazi ya Sheria Ndogo ni kutoa ufafanuzi wa kina ili kufanikisha utekelezaji wa sheria ya Bunge, dosari au hitilafu zilizobainika zinaweza kuzorotesha utekelezaji wa sheria na hivyo kukwamisha azma ya Bunge. Kwa sababu hiyo, haitarajiwi Bunge kuendelea na utungaji wa sheria nyingine bila kusimamia usahihishaji wa dosari hizo.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kuliwezesha Bunge kuwa katika nafasi nzuri ya kuamua, sehemu hii inafafanua dosari na hitilafu kwa kurejea mifano halisi kama ifuatavyo:-

**2.2.1 Dosari ya Kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba**

**Mheshimiwa Spika,** Nia ya sheria ndogo ni kufanikisha lengo kuu la sheria mama. Aidha, sheria ndogo zinatarajiwa kuendana na masharti ya Katiba ambayo ni msingi mkuu wa sheria za nchi zikiwemo sheria mama. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kuwa, baadhi ya sheria ndogo zina maudhui yanayotofautiana na matakwa ya Katiba. Mfano wa sheria ndogo zenye dosari hiyo ni Kanuni iitwayo ***The Whistleblower and Witness Protection Regulations, 2023.***

**Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 5 (4)** ya Sheria Ndogo hiyo inampa haki ya kukata rufaa mtoa taarifa ambaye maombi yake ya kupatiwa ulinzi yamekataliwa na mamlaka inayohusika. Kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hiyo, mtoa taarifa ambaye hajaridhika na uamuzi wa kutopatiwa ulinzi anapaswa kuwasilisha rufaa yake kwa Waziri ndani ya siku kumi na nne tangu kutolewa kwa uamuzi. Dosari ya Kanuni hii ni kutokuonesha muda ambao Waziri atashughulikia shauri la rufaa lililowasilishwa mbele yake. Dosari hiyo inabeba sura ya kubariki ucheleweshaji wa mashauri ya rufaa, jambo ambalo ni kinyume na masharti ya **Ibara ya 107A** ya Katiba. Kwa masharti ya Ibara hiyo, mamlaka zote zinazojihusisha na utoaji wa haki hazipaswi kuchelewesha haki bila sababu ya msingi.

**Mheshimiwa Spika,** Iwapo Bunge halitasisitiza marekebisho ya dosari hiyo litakuwa limeruhusu madaraka yake ya kutunga sheria yatumike kukiuka masharti ya Katiba kama ilivyo kwa kanuni hii. Hivyo, mjadala wa Bunge kuhusu sheria ndogo unategemewa kuhitimishwa kwa kuitaka mamlaka inayohusika kurekebisha dosari iliyobainishwa kwa kuweka muda mahsusi ambao Waziri atashughulikia shauri la rufaa lililowasilishwa mbele yake.

### 2.2.2 Dosari ya Kuwa na masharti Yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi

**Mheshimiwa Spika,** Kama tunavyofahamu, sheria ndogo zinatokana na mamlaka ya Bunge yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine. Lengo la Bunge kukasimu madaraka yake ni kuwezesha utekelezaji wa Sheria mama. Hivyo, ni muhali kuwa na sheria ndogo inayokiuka masharti ya Sheria ambayo inaipa nguvu. Kwa mantiki hiyo, sheria ndogo yoyote inayokiuka masharti ya sheria mama itakuwa imechupa mipaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 36 (1) cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, kinakataza sheria ndogo kukinzana na sheria mama au sheria nyingine ya nchi. Aidha, kifungu hicho kinabatilisha sheria ndogo inayokinzana na masharti ya sheria mama au ya sheria nyingine ya Bunge. Licha ya masharti hayo ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Kamati imebaini kuwepo kwa sheria ndogo zenye dosari ya kukinzana na sheria mama.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa sheria ndogo zenye dosari ya kuwa na masharti ni *The Law School of Tanzania (Admission, Fees and Conduct of Practical Training) Rules, 2022* ambayo imetungwa chini ya Sheria ya *The Law School of Tanzania Act*. Jedwali la Kwanza la Kanuni hizi pamoja na masuala mengine linaonesha ada ya programu ya mafunzo maalumu kwa Wasaidizi wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika**, uwekaji wa ada kwa ajili ya programu ya mafunzo maalumu kwa Wasaidizi wa Sheria chini ya Kanuni hizi ni kukinzana na sheria mama. Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinaeleza kuwa, sheria hiyo itatumika kwa mtu yoyote mwenye Shahada ya Sheria kutoka chuo kikuu au chuo kinachotambulika, na mwenye nia ya kutumia taaluma hiyo katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama mtumishi wa umma, wakili wa Mahakama Kuu na Mahakama za chini.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Sheria mama ambayo ndio imetengeneza Kanuni hizi, haijatambua masuala ya Wasaidizi wa Sheria, ilitarajiwa pia Kanuni nazo zisiweke maudhui hayo, kwa kuweka masuala ambayo hayapo katika Sheria mama ni kukinzana na masharti ya Kifungu cha 36(1) cha Sheria ya Tafsiri

ya Sheria kinachokataza sheria ndogo kukinzana na sheria mama au sheria nyingine ya nchi.

**Mheshimiwa Spika**, Kama inavyofahamika, Bunge linapokabidhi kwa mamlaka za serikali madaraka ya kutunga kanuni, halikusudii kuruhusu sheria ndogo inayokinzana na masharti yanayowekwa na Bunge kupitia Sheria Mama. Hivyo, sheria ndogo zote zenye masharti yanayokinzana na masharti yaliyowekwa na Bunge kwenye sheria mama hazistahili kuwa sehemu ya sheria za nchi na hazipaswi kutumika.

**2.2.3 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria**

**Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya misingi ya uandishi wa sheria ni kuwezesha sheria za nchi kufanikisha hatua za serikali kisera, sheria kueleweka kwa urahisi miongoni mwa watu au wananchi wanaoguswa pamoja na wanaosimamia au wenye jukumu la kuzitafsiri. Bunge linapotunga sheria huzingatia misingi ya uandishi ambayo huwezesha mawazo ghafi kuwekwa katika ukamilifu unaoeleweka na wenye maana halisi kiutekelezaji. Kazi nzuri ya Mwandishi Mkuu wa Sheria Nchini inaliwezesha Bunge kuzingatia misingi ya Uandishi wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Iwapo Bunge lenye mamlaka kamili ya utungaji wa sheria linazingatia misingi ya uandishi, Sheria Ndogo zinatokana na sheria za Bunge zinapaswa kuandikwa kwa kuzingatia ipasavyo misingi ya uandishi wa sheria nchini. Hata hivyo, uchambuzi umeonesha kwamba, zipo sheria ndogo zenye dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa Sheria Ndogo zenye dosari hiyo ni **Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023**. Katika Kanuni hizo, namna **Kanuni ya 10 (a)** inavyoweka utaratibu wa kusajili laini kwa watoto ina dosari ya kiuandishi. Dosari iliyopo ni kumlazimisha mzazi au mlezi anayetaka kusajili laini ya mtoto, awasilishe kwa pamoja nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto, nakala ya cheti cha kuasili mtoto, hati halali ya kusafiria pamoja picha ya mtoto anayehusika.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa masharti hayo yanayolazimisha uwasilishaji wa nakala zote kwa pamoja yatafuatwa,

yatasababisha watoto wanaokosa moja kati ya nyaraka hizo, kutoruhusiwa kusajili laini za simu. Athari hiyo itazuia kutimia kwa lengo la Sheria Mama ambayo ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 (*Electronic and Postal Communications Act Cap. 306*). Lengo la Sheria hiyo ni kuanzisha daftari kuu la utambulisho wa vifaa kwa ajili ya usajili wa simu zinazoweza kuondolewa na simu za mkononi zenye simu kadi zilizojengewa ndani.

**2.2.4 Dosari za Uandishi wa Majedwali**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kawaida madhumuni ya majedwali katika Sheria yoyote ni kutimiza malengo ya kifungu cha sheria inayohusika. Hivyo, dosari yoyote ya jedwali kwa msingi huo, inakwamisha azma ya sheria inayohusika. Matokeo ya uchambuzi yanaonesha kwamba, sheria ndogo mbili (02) zina dosari ya uandishi wa majedwali. Mfano wa sheria ndogo hizo ni **Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Kuingia Ndani ya Nchi na Kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023.**

**Mheshimiwa Spika,** Jedwali la pili la Kanuni hizo lina dosari katika uandishi wake. Jedwali hilo limewekwa kwa mujibu wa Kanuni ya 6 ambayo inaanzisha vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu yanayosafirishwa kuingia ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi. Uchambuzi umeonesha kuwa maudhui ya jedwali hilo yana hitilafu kwa kutokutaja maeneo mengine ambayo yanatumika kuingia Ndani ya Nchi na kutoka Nje ya nchi. Kwa mfano, bandari zote zilizo katika ziwa Nyasa, ziwa Victoria, vituo vya reli vya Kigoma na Mwanza pamoja na Viwanja vya ndege vyote ni maeneo ambayo hayamo katika orodha inayobainishwa na Jedwali.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokutambuliwa kwa maeneo hayo muhimu katika jedwali ni mwanya unaoweza kutumika kupitisha mazao ya misitu ili kukwepa ukaguzi. Uwezekano huo unafifisha lengo la Sheria ya Misitu ambalo ni usimamizi wa Misitu. Jambo hilo halipaswi kufumbiwa macho na Bunge kwa kuwa nia yake ya kuruhusu sheria ndogo haikuwa kuzuia lengo la Sheria.

## 2.3 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako linao wajibu wa kuhakikisha kwamba, madaraka yake ambayo yamekabidhiwa kwa mamlaka nyingine yanatumika inavyostahili. Wajibu huo unalitaka Bunge kutokuishia kutoa maazimio kuhusu urekebishwaji wa sheria ndogo bali pia kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake. Ili kutimiza wajibu huo ni jukumu la Bunge lenyewe kufuatilia ipasavyo namna madaraka hayo yanavyotumika. Kwa maneno mengine, Bunge halipaswi kuishia kwenye kubainisha dosari katika sheria ndogo na kuamua kwa njia ya maazimio. Kwa kawaida, Bunge linapaswa kujiridhisha iwapo dosari hizo zimerekebishwa kwa namna ilivyoazimiwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Bunge linaituma Kamati ya Sheria Ndogo kusimamia utekelezaji bora wa madaraka ya sheria ndogo yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine, Kamati hii inawajibika kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Bunge. Lengo ni kuona hatua inayofikiwa na kulinganisha na hatua iliyostahili ili kulishauri Bunge uamuzi unaofaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa sheria ndogo ni sehemu ya Sheria za nchi, dosari zinazojitokeza katika Sheria hizo, zinapaswa kufanyiwa kazi kwa utaratibu unaoendana na desturi za Bunge. Bila kufanya hivyo, madhara ya dosari zote yanavyoendelea yanaweza kuliweka Bunge kwenye kulaumiwa na wananchi. Bunge ambalo ni chombo halisi cha wananchi haliwezi kuacha kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari katika sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio uliangalia hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio hayo. Uangaliaji na ufuatiliaji wa hatua hizo za utekelezaji ulidadisi mambo yafuatayo:-

(a) Iwapo hakuna kabisa utekelezaji wa maazimio;

(b) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(c) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya Rasimu ya marekebisho kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(d) Iwapo utekelezaji wa Maazimio umefikia hatua ya marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, udadisi ulioegemea katika vigezo hivyo, uliiwezesha Kamati kutathmini hali ya utekelezaji wa kila azimio lililotolewa na Bunge na hatimaye kupata matokeo halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji. Matokeo hayo yataliwezesha Bunge kuamua kuhusu hatua inayofuata.

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari za sheria ndogo zilizowasilishwa wakati wa Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge, yanafaa kuripotiwa. Nia ni kuonesha hatua iliyofikiwa ili kusahihisha dosari kama ilivyoamuliwa kupitia maazimio ya Bunge. Matokeo hayo yanaonesha kwamba, hatua zilizoripotiwa za kusahihisha dosari ili kutekeleza maazimio ya Bunge, zinagawanyika katika makundi makuu manne yafuatayo:-

(a) Maazimio ya Bunge kutokuwa yametekelezwa;

(b) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho katika ngazi ya Wizara;

(c) Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki; na

(d) Hatua ya Marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Hatua zilizoripotiwa kwenye Kamati ni kwa kipindi cha kuishia tarehe 25 Agosti, 2023. Naomba kufafanua hatua hizo sambamba na kubainisha wizara zinazohusika. Lengo la ufafanuzi huu ni kuliwezesha Bunge kubaini kiwango cha utekelezaji wa maazimio yake na kufanya uamuzi stahiki. Ili kuweka bayana wahusika wa utekelezaji wa maazimio, naomba kubainisha Wizara zinazohusika na utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo. Wizara hizo ni:-

(a) Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliyokuwa na Sheria ndogo ishirini na moja (21) zilizobainika kuwa dosari sitini na moja (61);

(b) Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira iliyokuwa na sheria ndogo tatu (03) zenye dosari saba (07);

(c) Iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi wakati wa uchambuzi ilikuwa na sheria ndogo tatu (03) zilizobainika kuwa na dosari tatu (03);

(d) Wizara ya Madini iliyokuwa na sheria ndogo moja (01) iliyobainika kuwa na dosari tatu (03); na

(e) Wizara ya Fedha iliyokuwa na sheria ndogo tatu (03) zenye dosari tisa (09).

**Mheshimiwa Spika,** hali halisi ya hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge inabainishwa katika **Kiambatisho Na. 2** (Jedwali la Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu sheria ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa). Jedwali hilo linafafanua hatua iliyofikiwa na kila Wizara. Pamoja na hivyo, kwa madhumuni ya kuweka mtiririko huo kwa ajili ya kuwezesha majadiliano juu ya hoja hii, naomba kufafanua hatua hizo kama ifuatavyo:

**2.3.1 Maazimio ya Bunge kutokuwa yametekelezwa**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ulionesha kuwa maazimio kuhusu jumla ya dosari kumi na tisa (19) kati ya themanini na tano (83) ambazo ni sawa na asilimia 22.89 ya dosari zote, hayajatekelezwa. Mchanganuo wa maazimio hayo unaonesha kuwa, maazimio kuhusu dosari kumi na sita (16) yanagusa sheria ndogo zinazosimamiwa na OR-TAMISEMI na maazimio kuhusu dosari tatu (03) ni kuhusu sheria ndogo inayosimamiwa na Wizara ya Madini.

**Mheshimiwa Spika,** Maazimio hayo ambayo hayajatekelezwa yanahusu dosari katika sheria ndogo zifuatazo:-

(a) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022 (TS Na. 216 la tarehe 15/04/2022);

(b) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji Wa Bunda ya Mwaka 2022 (TS Na. 375 la tarehe 27/05/2022);

(c) Sheria Ndogo ya (Ada na Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS Na. 560 la tarehe 16/9/2022);

(d) Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Stendi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS Na. 561 la tarehe 16/9/2022);

(e) Sheria Ndogo ya (Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS NA. 563 la tarehe 16/9/2022);

(f) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ya Mwaka 2022 (TS NA. 567 la tarehe 16/9/2022);

(g) Sheria Ndogo ya (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2022 (TS NA. 588 la tarehe 30/9/2022);

(h) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ya Mwaka 2022 (TS NA. 591 la tarehe 30/9/2022);

(i) Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ya Mwaka 2023; na

(j) *The Mining (State Participation) Regulations, 2022* (TS NA. 574 la tarehe 23/9/2022).

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya kutotekeleza Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira ya kutokuyapa uzito. Hatua ya

kutotekeleza maazimio ni kufifisha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika sheria ndogo zinazohusika, hivyo kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa dosari inayoendelea kutokana na kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge ipo katika **Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ya Mwaka 2023**. **Kifungu cha 22 (2)** cha Sheria Ndogo hizi kinaweka adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayevunja masharti ya sheria ndogo hii, kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki mbili au kifungo cha miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Adhabu hiyo iliyowekwa na **Kifungu cha 22 (2)** inatofautiana na adhabu ya jumla iliyowekwa na kifungu cha 36(1) cha Sheria Ndogo hiyo. Kwa mujibu wa kifungu cha 36 (1) adhabu ya jumla kwa kosa la kukiuka masharti ya sheria ndogo hiyo ni faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja. Mkinzano huo wa adhabu unaendelea kuwepo kutokana na mamlaka inayohusika kutokutekeleza maazimio ya Bunge. Athari yake katika maisha ya watu wanaowakilishwa na Bunge ni kuendelea kupata madhara ya mkanganyiko wa adhabu, jambo ambalo haikuwa dhamira ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi haliwezi na halitaweza kuacha mamlaka yake ya kutunga sheria yatumike kwa namna inayowakanganya wananchi. Athari yoyote ambayo inatokana na kuchelewa kutekeleza uamuzi wa Bunge, haifai kuendelea kuachwa. Hivyo, athari ya kutokutekelezwa kwa maazimio hayo kwa kipindi chote tangu tarehe 8 Februari, 2023 Bunge lilipo azimia mpaka tarehe 9 hadi 14 Agosti, 2023 wakati Kamati ikipokea taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge takriban miezi sita, ni jambo lisilostahili kujirudia.

### 2.3.2 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho katika ngazi ya Wizara

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuandaliwa na kuwepo katika ngazi ya Wizara inaonesha kuwa nyuma ya hatua mbili katika utekelezaji uliokamilika wa maazimio ya Bunge.

Kwa maneno mengine hatua hiyo inaendeleza dosari zilizobainishwa na madhara yake yanaendelea kuwepo bila kuwa yamefanyiwa kazi. Jambo hili linaleta mashaka makubwa kwa Kamati kuhusu tija ya madaraka ya Bunge yaliyokasimiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibaini maazimio ya Bunge kuhusu dosari tatu (03) za sheria ndogo inayosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, kuwa yapo katika hatua Rasimu ambayo bado inapitia michakato ya ndani ya Wizara. Maazimio hayo ambayo yametekelezwa hadi hatua ya kuwa na Rasimu ya Marekebisho iliyo katika ngazi ya Wizara, yanahusu dosari katika sheria ndogo ya *The Environmental Management (Control and Management of Carbon Trading) Regulations, 2022.*

**Mheshimiwa Spika**, Kuendelea kuwa Rasimu ya Marekebisho ya Sheria Ndogo baada ya Maazimio ya Bunge inaweza kuwa na taswira ya kuchelewesha azma ya Bunge ambalo ndilo mamlaka kuu ya utungaji wa sheria za nchi. Ikumbukwe kuwa Maazimio ya Bunge yanalenga kusimamia madaraka yake yaliyokabidhiwa kwa mamlaka nyingine, hivyo utekelezaji wa maazimio unapochelewa, unazorotesha dhamira ya Bunge ya kuondoa dosari katika sheria ndogo zinazohusika. Hivyo, kuendeleza dosari hizo ambazo zinasababisha changamoto mbalimbali miongoni mwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa changamoto inayoendelea kwa sababu ya kutokamilika kwa Rasimu ya Marekebisho ya sheria ndogo ni athari ya dosari iliyokuwa imebainika katika Sehemu C ya Jedwali la kwanza la sheria ndogo hiyo. Dosari hiyo ni kuweka kiwango cha gharama za mradi ikiwemo, gharama za maandalizi, gharama za uanzishaji na gharama nyingine pamoja na gharama ya jumla kuwa zinapimwa kwa thamani ya kuanzia dola za kimarekani milioni moja. Changamoto yake ni kwamba, masharti hayo yanaendelea kuwaacha au kutowajumuisha watu wenye mitaji iliyo chini ya dola milioni moja za marekani.

**Mheshimiwa Spika,** Masharti hayo yonaashiria kwamba waombaji wote, watatakiwa kujaza miradi iliyo na thamani ya kuanzia dola milioni moja za kimarekani kwa kila hatua ya mradi, hivyo masharti

hayo yanazuia waombaji ambao gharama za uwekezaji wa miradi yao hazijafikia thamani hiyo.

**2.3.3 Hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Uhakiki**

**Mheshimiwa Spika,** Hatua ya Rasimu ya Marekebisho iliyowasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ni kiashiria muhimu. Hatua hiyo inaonesha mwelekeo wa kutimiza azma ya Maazimio ya Bunge kutatua changamoto zitokanazo na dosari za sheria ndogo zilizobainishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji ulibainisha kuwepo kwa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari Kumi na tano (15) katika sheria ndogo Sita (06) uliofikia hatua ya Rasimu ya Marekebisho kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki. Mchanganuo wa dosari zilizotolewa maazimio na kufikia hatua hiyo ni kama ifuatavyo:-

(a) dosari nane (08) za sheria ndogo tatu (03) zinazosimamiwa na Ofisi ya Rais -TAMISEMI,

(b) dosari nne (04) zinahusu sheria ndogo mbili (02) zinazosimamiwa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; na

(c) dosari tatu (03) zinahusu sheria ndogo moja (01) inayosimamiwa na Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika**, Sheria ndogo zilizoanza kufanyiwa marekebisho katika hatua hii ni:

(a) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji Wa Bunda ya Mwaka 2023;

(b) Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ya Mwaka 2023;

(c) Sheria Ndogo ya (Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi ya Mwaka 2023;

(d) *The Environmental Management (Prohibition of Plastic Carrier Bags and Plastic Bottle Cap Regulations, 2022* (TS NA. 291 la tarehe 6/05/2022);

(e) *The Environmental Management (Control of Ozone Depleting Substances and Hydrofluorocarbons) Regulations, 2022* (TS NA. 291 la tarehe 6/05/2022); na

(f) *The Foreign Exchange Regulation, 2022* (TS NA. 294 13/05/2022).

**Mheshimiwa Spika**, Hatua hiyo inaelekea kuondoa changamoto. Kwa mfano, marekebisho ya **Kanuni ya 27(b)** ya Sheria Ndogo ya ***The Environmental Management (Control of Ozone Depleting Substances and Hydrofluorocarbons) Regulations, 2022*** yanaondoa changamoto ya sheria kutokuonesha namna mamlaka ya Afisa Fordha yanavyotekelezwa ili kukagua atakavyokagua na kutambua mzigo ulioingizwa nchini ambao una chembechembe za kikemikali zenye athari kwa Ozoni.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa reja ya Bunge lako tukufu, Kanuni hii inampa Afisa Forodha mamlaka ya kukagua na kutambua ikiwa mzigo ulioingizwa nchini una chembechembe za kikemikali zenye athari kwa Ozoni. Dosari iliyobainishwa ni kutokuonesha namna atakavyokagua kwa kuwa si mtaalamu wa masuala ya kemikali jambo linalokanganya katika utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika**, Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hii liliitaka mamlaka inayohusika kufanya marekebisho ya **Kanuni ya 27(b)**. Lengo ilikuwa ni kuonesha namna ambavyo Afisa Forodha atawezeshwa kufanya ukaguzi wa mizigo inayoinga nchini kwa lengo la kubaini iwapo ina chembechembe za kemikali zenye athari kwa Ozoni.

**Mheshimiwa Spika,** Hatua iliyofikiwa katika kutekeleza azimio la Bunge ikikamilika, itasaidia utambuzi wa kemikali zinazohusika kama ilivyokusudiwa na Kanuni hizi. Itakapofikia hatua ya mwisho ya kuanza kutumika kwa marekebisho hayo, mamlaka ya kutunga kanuni yaliyokasimiwa na Bunge yatakuwa yametumika

kufanikisha malengo ya Sheria ya usimamizi wa Mazingira ambayo ni sheria mama.

**2.3.4 Hatua ya Marekebisho Kutangazwa katika Gazeti la Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Marekebisho ya sheria ndogo Kutangazwa katika Gazeti la Serikali ni hatua inayostahili kupongezwa. Kwa ujumla hatua hii ni ya juu ya uzingatiaji wa maazimio ya Bunge. Katika hatua hii, mamlaka zinazohusika zimeweka juhudi ya kusahihisha dosari zilizobainishwa. Kwa kufanya hivyo madhara ya dosari hizo yameondoshwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge zilizowasilishwa na kujadiliwa na Kamati zinaonesha kuwa, sheria ndogo zilizofikia hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali ni ishirini na tatu (23). Kati ya sheria ndogo hizo, kumi na nane (18) zinasimamiwa na Ofisi Rais TAMISEMI, mbili (02) zinasimamiwa na Wizara ya Fedha na tatu (03) zilisimamiwa na iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Maazimio uliofikia hatua ya Marekebisho kutangazwa katika Gazeti la Serikali unahusu dosari katika sheria ndogo zifuatazo:-

(a) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022 (TS Na. 216 la tarehe 15/04/2022);

(b) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya Mwaka 2022 (TS Na. 217 la tarehe 15/04/2022);

(c) Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi ya 2022 (TS Na. 219 la tarehe 15/04/2022);

(d) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ya Mwaka 2022 (TS Na. 224 la tarehe 15/04/2022);

(e) Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale ya Mwaka 2022 (TS Na. 324 la tarehe 13/05/2022);

(f) Sheria Ndogo ya (Afya na Usafi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Mji Wa Bunda ya Mwaka 2022 (TS Na. 375 la tarehe 27/05/2022);

(g) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Songea ya Mwaka 2022 (TS Na. 376 la tarehe 27/05/2022);

(h) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo ya Mwaka 2022 (TS Na. 480 la tarehe 8/07/2022);

(i) Sheria Ndogo ya (Ada na Vibali vya Burudani) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS Na.560 la tarehe 16/9/2022);

(j) Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Stendi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS Na. 561 la tarehe 16/9/2022);

(k) Sheria Ndogo ya (Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala ya Mwaka 2022 (TS NA. 563 la tarehe 16/9/2022);

(l) Sheria Ndogo ya (Udhibiti wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalalaya Mwaka 2022 (TS NA. 564 la tarehe 16/9/2022);

(m) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero ya Mwaka 2022 (TS NA. 567 la tarehe 16/9/2022);

(n) Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2022 (TS NA. 586 la tarehe 30/9/2022);

(o) Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2022 (TS NA. 587 la tarehe 30/9/2022);

(p) Sheria Ndogo ya (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke ya Mwaka 2022 (TS NA. 588 la tarehe 30/9/2022);

(q) Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ya Mwaka 2022 (TS NA. 589 la tarehe 30/9/2022);

(r) Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ya Mwaka 2022 (TS NA. 590 la tarehe 30/9/2022);

(s) *The Merchant Shipping (Maritime Labour) Regulations* 2022 (TS NA. 228 la tarehe 22/04/2022);

(t) *The Merchant Shipping (Seafarers' Identity Document) Regulations, 2022*(TS NA. 229 la tarehe 22/04/2022);

(u) *The Merchant Shipping (Continous Discharge Certificate) Regulations, 2022* (TS NA 230 22/04/2022);

(v) *The Banking and Financial Institutions (Mortgage Refinance Companies) Regulations, 2022*(TS NA. 559 la tarehe 16/09/2022)*;* na

(w) *The Banking and Financial Institutions (Financial Leasing) Regulations, 2022* (TS NA. 575 23/09/2022).

**Mheshimiwa Spika,** Mfano wa dosari iliyorekebishwa kufikia hatua hiyo ipo katika Sheria Ndogo ya *The Merchant Shipping (Continous Discharge Certificate) Regulations, 2022* (TS NA 230 22/04/2022). Azimio la Bunge katika Sheria Ndogo hii, lililenga kuondoa dosari ya kuweka adhabu inayokinzana na Sheria mama. **Kanuni ya 21** ya sheria ndogo hii, iliweka adhabu kwa mtu yeyote atakayekiuka masharti yoyote ya Kanuni na kanuni mahsusi inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, kuwa atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 200 na isiyozidi shilingi za kitanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote kwa pamoja, ilhali kwa kosa hilo hilo, **kifungu cha 401** cha Sheria

Mama kimeweka adhabu ya kulipa faini ya shilingi za Tanzania zenye thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara imetekeleza azimio la Bunge kwa kufuta adhabu iliyowekwa na chini ya Kanuni ya 21 na badala yake kuweka adhabu inayofanana na iliyowekwa chini ya Kifungu cha 401 cha Sheria Mama. Marekebisho haya yanafanikisha malengo ya sheria mama.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti ambayo imefikiwa na Wizara zinazohusika ni mwitikio mzuri wa maazimio ya Bunge yaliyolenga kuondoa changamoto zilizobainishwa katika sheria ndogo.

**2.4 Majumuisho kuhusu yatokanayo na Shughuli zilizotekelezwa**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla shughuli zilizotekelezwa na Kamati zilitokana na misingi ya majukumu ya Kamati kuanzia masharti ya Katiba, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Kanuni za Bunge. Shughuli hizo zililenga kulisaidia Bunge katika wajibu wake wa Udhibiti wa Kibunge wa sheria ndogo. Mambo yaliyobainika kutokana na Shughuli hizo ni pamoja na dosari katika maeneo manne ya sheria ndogo. Maeneo hayo yanahusu kutokuendana na masharti ya Katiba, kukinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za nchi, Kutozingatia misingi ya Uandishi wa Sheria na dosari za uandishi wa majedwali.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo hayo ni athari hasi katika matumizi ya sehemu ya madaraka ya Bunge ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa kwa mtu au mamlaka nyingine kwa utaratibu wa kukasimu kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 97 (5) ya Katiba. Aidha, hatua za utekelezaji wa maazimio ya Bunge zinadhihirisha umuhimu wa Bunge kuendelea kuwa makini na kufuatilia utekelezaji wa maazimio yake kuhusu dosari hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla hatua nzuri na ya kupongezwa ni ile ya kukamilisha marekebisho na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kwa sababu hatua hiyo inaondoa dosari zilizobainishwa. Kundi hili linahusu baadhi ya sheria ndogo zinazosimamiwa na

Ofisi ya Rais (TAMISEMI), iliyokuwa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Kundi lingine linajumuisha hatua za Utekelezaji uliochelewa ambayo nayo inarekebisha dosari zilizobainika lakini kwa kuchelewa. Hatua hizo si mbaya ingawa ingelifaa kukamilisha mapema ili kupunguza muda wa athari hasi za dosari zilizobainishwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kundi la mwisho linahusu Wizara ambazo hazijatekeleza Maazimio ya Bunge katika baadhi ya sheria ndogo. Kutokutekelezwa kwa maazimio kunaendeleza changamoto ambazo Bunge limeziona katika sheria ndogo mbalimbali, hivyo kushindwa kutatua kero ambazo Bunge lililenga kuziondoa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuwa Kamati hii imepewa majukumu ya kuchambua Sheria Ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria inayotekelezwa na sheria ndogo inayohusika pamoja na sheria nyingine za nchi Kamati imechambua kwa kuzingatia vigezo hivyo. Uchambuzi huu hutumika kama nyenzo ya Bunge kusimamia matumizi ya madaraka ya Bunge ya kutunga sheria iliyoyakasimu kwa mamlaka nyingine. Mjadala wa taarifa hii unahitaji umakini wa hali ya juu ili kufanikisha lengo lililokusudiwa na Bunge wakati linakasimisha madaraka yake kwa mamlaka nyingine.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake, ninaliomba Bunge lako lipokee mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na kuyafanyia kazi. Kwa madhumuni hayo, naomba kudhihirisha mtazamo wa Kamati unaotokana na uchambuzi kama ifuatavyo:-

### 3.1.1 Dosari ya kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**Mheshimiwa Spika,** Dosari ya sheria ndogo kukinzana na Katiba ya Nchi ni dosari inayoitoa Sheria hiyo nje ya Misingi ya Utungaji wa Sheria. Kamati ina maoni kwamba, Bunge ambalo ni Mamlaka ya kutunga Sheria, haliwezi kuruhusu matumizi ya sheria ndogo zenye dosari hiyo kwa kuwa Bunge lenyewe halipaswi kutunga sheria inayokinzana na masharti ya Katiba.

### 3.1.2 Dosari ya kuwa na Masharti yanayokinzana na Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi

**Mheshimiwa Spika,** Dosari ya sheria ndogo kukinzana na Masharti ya Sheria Mama ni changamoto isiyostahili kuendelea kuwepo. Dosari hiyo inakaidi masharti yanayowekwa na Bunge kupitia Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1. Aidha, dosari ya aina hiyo inakiuka masharti ya madaraka ya Bunge yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na sheria hiyo, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge.

### 3.1.3 Dosari ya kutoendana na misingi ya uandishi wa Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Dosari za uandishi wa Sheria ndogo ni kinyume na matarajio ya Bunge. Dosari hizo zinaathiri azma ya kuwezesha na kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera au sheria kueleweka kwa urahisi miongoni wa watu. Bunge linapotunga sheria halipaswi kukiuka misingi ya uandishi yenye madhumuni hayo.

### 3.1.4 Dosari za uandishi wa Majedwali

**Mheshimiwa Spika**, Majedwali ya sheria ndogo yanapokuwa na hitilafu za uandishi, yanaathiri lengo la sheria ndogo inayohusika. Athari hiyo inafifisha madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa kwa ufafanuzi wa sheria ndogo. Bunge ambalo hukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine serikalini, hupaswa kuzingatia misingi ya uandishi wa majedwali katika Sheria. Kwa msingi huo, Kamati ina maoni kuwa Kuruhusu sheria ndogo yenye hitilafu ya uandishi wa majedwali iendelee kutumika ni suala lisilotarajiwa kwa Bunge.

### 3.1.5 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio yanayohusu Kurekebisha Sheria Ndogo

**Mheshimimiwa Spika**, Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kero kwa wananchi. Bunge ambalo ni sauti ya wananchi halipaswi kutokusema chochote inapotokea dosari hiyo. Ni maoni ya Kamati kuwa, kuchelewa kutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo, ni jambo ambalo linachelewesha utatuzi wa kero za wananchi. Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria, halipaswi kuruhusu mamlaka serikalini zichelewe kusahihisha dosari ilhali zimekabidhiwa mamlaka ya kutunga sheria ndogo.

### 3.1.6 Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge

**Mheshimiwa Spika,** Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari 19 za sheria ndogo 10 ni jambo linalokwamisha azma ya Bunge kuondoa changamoto zitokanazo na dosari hizo. Ni maoni ya Kamati kwamba, kuendelea na dosari 19 za sheria ndogo kumi zilizobainishwa, ni jambo linalohitaji kuzuiwa na Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi.

### 3.2 Majumuisho ya Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kujumuisha maoni ya Kamati, naomba kulikumbusha Bunge hili kuwa dosari zilizobainika zinaathiri tija ya Bunge kukasimu madaraka ya kuweka kanuni kwa mamlaka nyingine. Athari za dosari hizo ni pamoja na kusababisha ugumu wa kueleweka kwa sheria na kuzalisha kero kwa wananchi kutokana na hitilafu kwenye sheria ndogo.

**Mheshimiwa Spika**, Madhara mengine ya dosari hizo ni uwezekano hafifu wa kutimia kwa lengo la baadhi ya Sheria zilizotungwa na Bunge na kuendelea kwa desturi isiyofaa katika utaratibu wa Sheria za nchi. Mambo hayo yanahitaji hatua za haraka za marekebisho na hasa kwa kuwa sheria ndogo zinagusa moja kwa moja maslahi ya wananchi katika utekelezaji wa shughuli za umma. Hali hiyo ndio hasa msingi wa mapendekezo ya maazimio ya Bunge katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile kuchelewa kutekeleza Maazimio ya Bunge yanayohusu marekebisho ya dosari za sheria ndogo ni

jambo lenye madhara kwenye nia ya Bunge kukasimu kwa mamlaka nyingine uwezo wa kufafanua sheria mama kupitia sheria ndogo. Madhara hayo ni pamoja na kuendeleza kero kwa wananchi licha ya kuwa zimebainishwa na chombo chao cha Uwakilishi. Aidha, hali hiyo inasababisha kuendeleza hitilafu ambazo chombo kikuu cha utungaji wa sheria nchini kamwe hakitaweza kudumisha hitilafu hizo pale zinapobainika. Kwa sababu hiyo Taarifa hii inajumuisha Mapendekezo ya Maazimio ya Bunge kwa lengo la kuondoa hitilafu hizo.

### 3.3 Mapendekezo

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Mapendekezo ya Kamati ni maoni yake yaliyotokana na shughuli kubwa mbili. Shughuli hizo zimetajwa kuwa ni **uchambuzi wa sheria ndogo** na **uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge**. Uchambuzi huo umekuwa msingi wa maoni ya Kamati kutokana na dosari zilizobainika katika sheria ndogo. Kwa kuzingatia maoni hayo, Kamati inapendekeza mambo saba kwa njia ya hoja kama inavyoelekeza Kanuni ya 61 ya Kanuni za Bunge. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:-

#### 3.3.1 Sheria Ndogo kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Katiba

**KWA KUWA**, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya katiba, suala ambalo ni kinyume na misingi ya sheria inayotambua ukuu wa Katiba,

**NA KWA KUWA**,

(a) ukiukwaji wa msingi wa masharti ya Katiba kwa sheria yoyote ni kinyume na Ibara ya 64 (5) ya Katiba;

(b) Bunge haliwezi kutunga sheria iliyo kinyume na Katiba na wala kukubali madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka nyingine, yatumike katika kutunga sheria yenye dosari inayokinzana na Katiba,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zote zilizobainika kuwa na dosari ya kukinzana na masharti ya Katiba ya nchi zifanyiwe marekebisho ili kutatua dosari hiyo.

**3.3.2 Dosari ya kuwa na Masharti yanayokinzana na Masharti ya Sheria Mama na Sheria Nyingine za Nchi**

**KWA KUWA,** Baadhi ya sheria ndogo zilizochambuliwa zina dosari ya kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi, jambo linaloweza kuathiri tija ya utekelezaji wa Sheria Mama inayohusika,

**NA KWA KUWA,** Dosari ya sheria ndogo kukinzana na Masharti ya Sheria Mama au kukinzana na masharti ya sheria nyingine za nchi:

(a) ni changamoto isiyostahili kuendelea kuwepo kutokana na kutoendana na masharti yaliyowekwa na mamlaka kuu ya kutunga sheria katika sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1,

(b) ni dosari inayotokana na kukiuka masharti ya madaraka ya Bunge yaliyokabidhiwa kwa mamlaka inayohusika na sheria hiyo, jambo ambalo halipaswi kuruhusiwa na Bunge; na

(c) ni dosari inayotosha kubatilisha sheria ndogo zinazohusika kwa mujibu wa kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1, jambo ambalo ni kinyume na madhumuni ya Bunge kukasimu madaraka yake kwa mamlaka nyingine serikalini;

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizotunga sheria ndogo zenye kukinzana na masharti ya Sheria mama na Sheria nyingine za nchi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari hiyo.

**3.3.3 Dosari ya Kutoendana na Misingi ya Uandishi wa Sheria**

**KWA KUWA**, baadhi ya sheria ndogo zimebainika kuwa na dosari za kutokuendana na misingi ya uandishi wa Sheria, jambo ambalo ni kinyume na matarajio ya Bunge,

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo:

(a) zinaathiri azma ya Bunge kufanikisha utekelezaji wa hatua za serikali kisera kupitia sheria za Bunge na Sheria ndogo;

(b) Zinakwamisha nia ya Bunge kuwezesha sheria kueleweka kwa urahisi miongoni wa wadau, wakiwemo watu wengine

ambao ni watekelezaji wa sheria au wanaoguswa na masharti ya sheria inayohusika; na

(c) Ni ukiukaji wa misingi ambayo Bunge ambalo ni mamlaka kuu ya utungaji wa sheria halipaswi kuikiuka,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zimebainika kuwa na dosari ya kutozingatia misingi ya uandishi wa sheria, zirekebishe dosari hiyo ili kuleta tija kwa watumiaji wa sheria hizo.

### 3.3.4 Dosari za Uandishi wa Majedwali

**KWA KUWA**, Zipo sheria ndogo zilizochambuliwa na kubainika kuwa na dosari ya kuwa na majedwali yenye hitilafu za uandishi, jambo linaloathiri lengo la sheria ndogo inayohusika;

**NA KWA KUWA,** Athari ya dosari hiyo;

(a) Inasababisha changamoto katika utekelezaji wa sheria ndogo inayohusika jambo ambalo haikuwa lengo la Bunge kukasimu madaraka ya kutunga sheria kwa mamlaka zinazohusika;

(b) Ni pamoja na kufifisha madhumuni ya Bunge kutunga sheria inayotekelezwa kwa ufafanuzi wa sheria ndogo; na

(c) Haiwezi kuvumiliwa na Bunge ambalo hukasimu madaraka ya kufafanua sheria kwa mamlaka nyingine serikalini,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zinazohusika na sheria ndogo ambazo zilibainika kuwa na majedwali yenye dosari za uandishi, zifanye marekebisho ili kuondoa dosari zilizobainika.

### 3.3.5 Kuwasilisha Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio kuhusu Sheria Ndogo zilizobainika kuwa na Dosari

**KWA KUWA,** Dosari zote zilizobainika katika uchambazi kama inavyoonekana katika Jedwali la Uchambuzi, Kiambatisho Na. 01 zinahitaji kurekebishwa inavyostahili,

**NA KWA KUWA,**

(a) Dosari hizo zisiposahihishwa zitaendelea kuwa na madhara ambayo yametokana na matumizi ya madaraka ya kutunga sheria ndogo yaliyokasimiwa kwa mamlaka zinazohusika;

(b) Bunge ambalo ndilo mamlaka kuu ya kutunga sheria ambayo ina dhima ya kuhakikisha kuwa sheria zote za nchi hazina dosari na wala hazisababishi kero kwa wananchi,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zote zinazohusika na sheria ndogo zenye dosari kama zilivyotajwa katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii, ziwasilishe Taarifa ya utekelezaji wa maazimio yote kuhusu dosari za sheria ndogo kwa Katibu wa Bunge ifikapo tarehe 02 Oktoba, 2023.

**3.3.6 Kutokutekelezwa kwa Maazimio**

**KWA KUWA** Kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge kuhusu dosari 19 za sheria ndogo 10 kama ilivyobainika wakati wa uchambuzi ni jambo linalokwamisha azma ya Bunge kuondoa changamoto zitokanazo na dosari hizo,

**NA KWA KUWA**, kuendelea kuwa na dosari 19 za sheria ndogo 10 zilizobainishwa:-

(a) ni kukumbatia athari ya dosari hizo katika utekelezaji wa sheria na kuafiki changamoto zinazoweza kutokana na dosari hizo;

(b) ni kubariki matumizi mabaya ya madaraka ya kufafanua sheria yaliyokabidhiwa na Bunge kwa mamlaka zinazohusika bila kujali madhara yake kwa wananchi

(c) Ni jambo linalohitaji kuzuiwa na Bunge ambalo ni chombo cha uwakilishi wa wananchi,

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, mamlaka zilizobainika kutotekeleza maazimio ya Bunge zitekeleze Maazimio hayo na kuwasilisha Taarifa za utekelezaji wake kwa Katibu wa Bunge, ifikapo tarehe 02 Oktoba, 2023.

### 3.3.7 Uchelewaji katika Kutekeleza Maazimio ya Kurekebisha Sheria Ndogo

**KWA KUWA,** Maazimio ya Bunge yaliyohusu kurekebisha dosari katika sheria ndogo, yalilenga kuondoa madhara ya dosari hizo, ikiwemo uwezekano wa kusababisha kero kwa wananchi;

**NA KWA KUWA**, kutokutekeleza maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa dosari za sheria ndogo ni jambo ambalo;

(a) Linalochelewesha utatuzi wa kero za wananchi wanaolitegemea Bunge kusimamia maslahi yao.

(b) halipaswi kuridhiwa na Bunge ambalo ni chombo halisi cha uwakilishi wa wananchi chenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma,

**KWA HIYO BASI**, Bunge linaazimia kwamba, Mamlaka zilizochelewa katika utekelezaji wa Maazimio ya Bunge, zikamilishe mchakato wa marekebisho na kuwasilisha kwa Katibu wa Bunge, ifikapo tarehe 02 Oktoba, 2023.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi kwa kuweka utaratibu wa Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuwasilishwa katika vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni katika Mkutano wa Kumi na Mkutano Kumi na Moja na Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge hatimaye kufanikisha taarifa hii. Kwa heshima kubwa naomba kuwatambua majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, (Mb) – Mwenyekiti;
2. Mhe. Ramadhan Suleiman Ramadhan, (Mb) M/ Mwenyekiti;
3. Mhe. Ally Yahya Mhata, Mb Mjumbe;
4. Mhe. Amour Khamis Mbarouk, (Mb) Mjumbe;
5. Mhe. Jacob Tarimo Priscus, (Mb) Mjumbe;

6. Mhe. Khamis Ali Vuai, (Mb) Mjumbe;
7. Mhe.Eng.Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho,(Mb) Mjumbe;
8. Mhe. Simai Hassan Sadiki, (Mb) Mjumbe;
9. Mhe. Askofu Josephat Mathias Gwajima, (Mb) Mjumbe;
10. Mhe. Balozi. Liberata Rutageruka Mulamula, (Mb) Mjumbe;
11. Mhe. Godwin Emmanuel Kunambi, (Mb) Mjumbe;
12. Mhe. Jacqueline Andrew Kainja, (Mb) Mjumbe;
13. Mhe. Abdallah Dadi Chikota, (Mb) Mjumbe;
14. Mhe. Aloyce Andrew Kwezi, (Mb) Mjumbe;
15. Mhe. Hamida Mohammed Abdallah, (Mb) Mjumbe;
16. Mhe. Ally Mohamed Kassinge, (Mb) Mjumbe;
17. Mhe. Dkt. Paulina Daniel Nahato, (Mb) Mjumbe;
18. Mhe. Mariam Omar Said, (Mb) Mjumbe;
19. Mhe. Zulfa Mmaka Omar, (Mb) Mjumbe;
20. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, (Mb) Mjumbe;
21. Mhe. Amina Bakar Yusuf, (Mb) Mjumbe; na
22. Mhe Latifa Khamis Juakali, (Mb) Mjumbe.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa moyo wa dhati kabisa nimshukuru Mhe. Jenista Muhagama, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kwa uratibu ambao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri wa sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushiriki wao katika Vikao vya Uchambuzi wa Sheria Ndogo na Vikao vya kupokea Taarifa za Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile napenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi mahiri wa Katibu wa Bunge Bi. Nenelwa J. Mwihambi, *ndc* kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

### 4.2 Hoja

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kutoa hoja kwamba, Bunge liipokee na kuikubali Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya

Sheria Ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Dkt. Jasson S. Rweikiza (Mb)
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo**
5 Septemba, 2023

**KIAMBATISHO NA. 1**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

**JEDWALI LA UCHAMBUZI WA SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MKUTANO WA KUMI NA MOJA WA BUNGE**

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI WA BUNGE** | | | | | | |
| 1. | **(TS. Na 660)**<br><br>25/11/2022 | *The Law School of Tanzania (Admission, Fees and Conduct of Practical Training) Rules, 2022*<br><br>*(Imetungwa chini ya kifungu cha 20(1)(a)(b)* | *The Law School of Tanzania Act, CAP 425* | Wizara ya Katiba na Sheria | 1. **Kanuni ya 4** inaweka utaratibu wa namna ya kuwasilisha maombi ya kujiunga na masomo katika Shule ya Sheria.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>a) Kanuni haijaweka bayana Fomu maalumu inayozungumziwa na Kanuni hiyo.<br><br>b) Kanuni hazioneshi iwapo namna ya kuwasilisha Maombi ya kujiunga na Chuo.<br><br>2. **Kanuni ya 8** inaanzisha jedwali la | 1. Marekebisho yafanyike kwa kuweka bayana Fomu maalumu inayozungumzwa na kanuni hizi. Pia kanuni zifanyiwe marekebisho kwa kuonesha njia ya kuwasilisha maombi hayo.<br><br>2. Marekebisho yafanyike kwa kuweka |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Ada linalohusu ada kwa walengwa wanaotambuliwa kama "*Tanzanian Students*".<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Neno "*Tanzanian Students*" linaleta mkanganyiko katika kutimiza lengo lililotarajiwa.<br><br>3. **Kanuni ya 9** inaanzisha Jedwali la Ada linalohusu ada kwa walengwa wanaotambuliwa kama "*Non-Tanzanians*".<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Neno "*Non-Tanzanian Students*" linaleta | tafsiri ya maneno "Tanzanian *Applicant* pamoja na *Non Tanzanian Applicant*.<br><br>3. Marekebisho yafanyike kwa kuweka tafsiri ya maneno "Tanzanian *Applicant* pamoja na *Non Tanzanian Applicant*. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mkanganyiko katika kutimiza lengo lililotarajiwa<br>Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko kwa Walengwa.<br><br>4. **Kanuni ya 11** inaipa Bodi uwezo pale itakapoona inafaa kufanya mapitio ya ada ya kujiunga na Shule ya Sheria na iwapo kutakuwa na mabadiliko ya ada wanafunzi wanapewa sharti la lazima kulipa ada hiyo kama itakavyoelekezwa na Bodi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Masharti ya **Kanuni ya** | 4. Marekebisho yafanyike katika **Kanuni ya 11** kwa kuonesha iwapo mabadiliko hayo yatakuwa ni kwa ajili ya wanafunzi ambao wanatarajia kujiunga na Shule ya Sheria au wanafunzi ambao tayari wamejiunga na wanaendelea na masomo katika Shule ya Sheria. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **11** hayaoneshi iwapo mabadiliko hayo yatakuwa ni kwa ajili ya wanafunzi ambao wanatarajia kujiunga na Shule ya Sheria au yatawahusu pia wanafunzi ambao tayari wamejiunga na wanaendelea na masomo katika Shule ya Sheria.<br>Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko kuhusu namna ya utekelezaji wa masharti hayo.<br><br>5. **Kanuni ya 13** inaweka ulazima kwa wanafunzi kutii miongozo, utaratibu na maelekezo yaliyowekwa na Mkuu | 5. **Kanuni ya 13** ifanyiwe marekebisho kwa kuonesha miongozo mingine itakayotumika kutambua ujuzi na bidii ya mwanafunzi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wa Chuo.<br>**Kanuni ndogo ya (2)** inaelezea hatua ambazo Mkuu wa Chuo atachukua endapo hatoridhishwa na Mahudhurio, bidii na Ujuzi wa Mwanafunzi ikiwemo kuitaarifu Kamati ambayo Itashauri Bodi kuchukua hatua stahiki dhidi ya Mwanafunzi anayehusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>a) Kanuni haioneshi vigezo ambavyo Mkuu wa Chuo atatumia Kujiridhisha na bidii na Ujuzi wa | Pamoja na hatua stahiki zinazotakiwa kufuatwa endapo Bodi haitaridhishwa na Mahudhurio, bidii na ujuzi wa mwanafunzi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Mwanafunzi.<br><br>b) Kanuni haijaweka bayana hatua stahiki zinazoweza kuchukuliwa na Bodi.<br><br>c) Kanuni haioneshi utaratibu wa kutoa taarifa kwa Mwanafunzi juu ya mchakato unaoendelezwa na Mkuu wa Chuo dhidi yake.<br><br>6. **Jedwali la Kwanza** la Kanuni linaonesha ada mbalimbali zinazopaswa kulipwa na Wanafunzi wa Shule ya Sheria na Wasaidizi wa Sheria | 6. Marekebisho yafanyike katika **Jedwali la Kwanza** kwa kuonesha kiwango cha ada ya maombi ya kujiunga na mafunzo katika |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | (*Paralegals*).<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Jedwali halioneshi iwapo wasaidizi hao wanapaswa kulipa ada ya maombi ya kujiunga na mafunzo katika Shule ya Sheria.<br><br>Kutokuwekwa bayana kwa kiwango cha ada kunasababisha kutokufahamika kwa kiwango kinachostahili kulipwa, hivyo kuleta mkanganyiko miongoni mwa waombaji.<br><br>7. Kanuni imeanzisha programu ya | Shule ya Sheria kwa wasaidizi wa Sheria (*paralegals*).<br><br>7. Marekebisho yafanyike ili kuendana |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | mafunzo maalumu kwa Wasaidizi wa Sheria na kuwatambua kwenye Jedwali la Kwanza linalobainisha ada mbalimbali zitakazotozwa na Shule ya Sheria.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Uanzishwaji wa programu hii unakinzana na matakwa ya **Kifungu cha 2 cha sheria mama** kinachotambua matumizi ya sheria hiyo pamoja na kanuni zake kwa mtu yoyote mwenye Shahada ya Sheria kutoka chuo kikuu au | na masharti ya Sheria Mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | chuo kinachotambulika, na mwenye nia ya kutumia taaluma hiyo.<br>Hali hii inaondoa uhalali wa programu ya mafunzo ya wasaidizi wa sheria.<br><br>8. **Jedwali la pili** linaainisha gharama mbalimbali zinazotakiwa kulipiwa ada katika shule hiyo ikiwemo gharama kwa ajili ya mapitio ya NACTE ambayo ni shilingi 20,000.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Jedwali limerejea mamlaka ambayo haitambuliki kisheria. | <br><br><br><br><br><br><br><br><br>8. Marekebisho yafanyike katika **Jedwali la Pili** kwa kurejea Mamlaka sahihi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA KATIKA MKUTANO WA KUMI NA MOJA WA BUNGE** | | | | | | |
| 2. | **(TS. Na. 59)**<br><br>10/02/2023 | The Whistleblower and Witness Protection Regulations, 2023<br><br>(Zimetungwa chini ya kifungu cha 15) | The Whistleblower And Witness Protection Act, (Sura ya 446) | Wizara ya Katiba na Sheria | 1. **Kanuni ya 5 (1) (a)** inaweka utaratibu wa Mamlaka ya utoaji Ulinzi kwa Mtoa Taarifa ama shahidi kutoa Notisi ya kuthibitisha kupokea ombi la ulinzi kwa Mtoa Taarifa na Shahidi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haijaweka mfumo wa Notisi ambao unaweza kutumika kama uthibitisho wa kupokea maombi ya ulinzi kwa mtoa taarifa kutoka kwa Mamlaka inayohusika. | 1. Kanuni ifanyiwe Marekebisho kuweka Fomu maalumu ya Notisi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Hali hii itasababisha kila Mamlaka inayohusika kuandaa notisi kwa namna yake, hali inayoweza kuleta mkanganyiko wa maudhui katika Notisi inayohusika.<br><br>2. **Kanuni ya 5 (4)** inazungumzia utaratibu wa Mtoa Taarifa kukata rufaa endapo hajaridhishwa na uamuzi kukataliwa kwa maombi yake ya kupatiwa Ulinzi. Kanuni inamtaka kukata Rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ndani ya siku 14 tangu | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha muda wa siku 21 ambao Waziri atashughulikia shauri la rufaa. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kutolewa kwa uamuzi huo.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi muda ambao Waziri atashughulikia shauri la Rufaa lililowasilishwa mbele yake.<br>Kukosekana kwa muda mahsusi kunaweza kusababisha Waziri ashughulikie shauri la rufaa kwa muda atakaoona unafaa, hali inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa haki ya mrufani.<br><br>3. **Kanuni ya 10 (1) (a) hadi (g)** inaainisha | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | sababu ambazo zinaweza kusababisha Makubaliano ya Ulinzi kuvunjwa na Mamlaka inayohusika. **Kanuni ya 10 (2)** inazungumzia sababu zinazoweza sababisha Makubaliano Maalumu ya Ulinzi kwa mtoto mdogo ama mtu asiye na utimamu wa akili kusitishwa kwa kuzingatia sababu zilizoainishwa katika **aya (a), (c), (g)** na **(h)** ya **Kanuni ya 10(1)** | kuondoa **aya ndogo ya (h)**. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | <u>**Tatizo**</u><br>**Aya (h)** iilyorejewa haipo katika Kanuni.<br><br>Kukosekana kwa aya hiyo inaweza kuwa ni:-<br>a) makosa ya kiuandishi ambayo yamepelekea kurejea aya isiyo sahihi; au<br><br>b) Kusahaulika kwa **aya (h)** ambayo ilipaswa kuwepo kwenye Kanuni.<br><br>Hali inaweza kusababisha kutotimia kwa malengo ya Kanuni katika eneo hilo na | |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | hivyo pia kuathiri malengo ya Sheria Mama. | |
| 3. | **(TS Na. 60)** 10/02/2023 | Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta Kuhusu Usajili wa Laini za Simu, 2023<br><br>(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 165) | Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, (Sura ya 306) | Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari | 1. **Kanuni ya 3** inahusu tafsiri ya maneno mbalimbali.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 3** imetoa tafsiri ya neno "**Mdiplomasia**" ambalo halipo katika maneno rasmi ya lugha ya Kiswahili.<br><br>Matumizi ya neno hilo ni kinyume na misingi ya uandishi na matumizi ya lugha fasaha ya Kiswahili. Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wa tafsiri iliyokusudiwa. | 1. Marekebisho yafanyike kwenye Kanuni kwa kutumia neno sahihi la Kiswahili "**mwanadiplomasia**". |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. **Kanuni ya 10** inahusu utaratibu wa kusajili laini kwa Watoto. **Aya (a)** ya Kanuni hii, inamtaka mzazi au mlezi kuwasilisha kwa pamoja nakala ya cheti cha kuzaliwa cha mtoto, nakala ya cheti cha kuasili mtoto, Hati halali ya kusafiria pamoja na picha ya pasipoti ya mtoto anayehusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imeweka ulazima wa kuwasilisha viambitisho vinne kwa pamoja ili kusajili laini ya simu ya mtoto. Kwa mantiki hiyo, masharti ya | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuruhusu usajili wa laini za simu kwa watoto ambao wana kiambatisho kimoja kati ya vinne vilivyotajwa na **Kanuni ya 10**. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kanuni hii yatawazesha usajili wa laini za simu kwa watoto walio na nyaraka hizo zote kwa pamoja.<br>Hali hiyo itasababisha watoto wengine wakose fursa ya kusajili laini za simu kwa kukosa moja kati ya nyaraka hizo, hivyo kuathiri lengo la Sheria Mama la usajili laini za simu.<br><br>3. **Kanuni ya 37 (6)** inatoa adhabu kwa yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni hizi. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuendana na adhabu iliyowekwa chini ya Kifungu cha 152 cha Sheria Mama. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Tatizo**<br>Adhabu zilizotolewa kwa mtu binafsi na taasisi zinakinzana na adhabu zilizowekwa na sheria mama katika kifungu cha 152 kifungu kidogo cha pili, hali inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa kanuni hizi kutokana na kuwepo kwa adhabu mbili tofauti. | |
| 4. | **(TS Na. 172)** 17/03/2023 | Kanuni za Uteuzi, Malipo na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka za Mwaka, 2023 | Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi, (Sura ya 216) | Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi | 1. **Kanuni ya 3(4)** inaonesha sababu nafasi ya Mjumbe wa Kamati kuwa wazi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haioneshi sababu ya kubaki | 1. **Kanuni ya 3(4) (d)** ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza maneno **uwezo** mara baada ya neno sifa |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | (Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 28C) | | | wazi kwa nafasi ya Ujumbe kama vile kutokana na ugonjwa utakaosababisha Mjumbe wa Kamati kushindwa kutekeleza Majukumu yake.<br><br>Hali hiyo inaacha ombwe na inaweza kusababisha nafasi hiyo ya Mjumbe kuonekana imejazwa ilhali si hivyo, jambo linaloweza kudumaza utendaji wa Kamati hivyo kutofanikisha lengo la Sheria Mama. | |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. **Kanuni 6(2)** inazungumzia sifa zitakazozingatiwa wakati wa uteuzi wa madalali wa Baraza au Wasambaza nyaraka<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imechanganya sifa za uteuzi wa Madalali na Wasambaza Nyaraka kwa pamoja ilhali, wahusika waliotajwa wana sifa zinazotofautina.<br><br>3. **Kanuni ya 6** inahusu uteuzi na sifa za kuteuliwa kuwa dalali wa Baraza au | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kutenganisha sifa za madalali na wasamabaza nyaraka<br><br>3. **Kanuni 6(5)** ifanyiwe marekebisho kwa kuweka sharti la lazima kwa msajili |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | | | | msambaza nyaraka. **Kanuni 6 (5)** inampa mamlaka msajili ya kuweza kubainisha idadi ya madalali wa mabaraza na wasambaza nyaraka.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 6(5)** imempa nafasi msajili kuamua kutangaza ama kutokutangaza idadi ya madalali na wasambaza nyaraka.<br><br>Hali hii inaweza ikaleta ugumu wa kuwatambua madalali na wasambaza nyaraka wanaohusika ikiwa | kubainisha idadi ya madalali wa mabaraza na wasambaza nyaraka ndani ya kipindi fulani. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | msajili hataweka wazi taarifa zao. Kutotambuliwa kwao na umma, kunaweza kusababisha athari kwa watumiaji wa huduma zitolewazo na madalali na wasambaza nyaraka.<br><br>4. **Kanuni ya 27 (4) (a)** inazungumzia hatua zitazakochukuliwa endapo mtu aliyetangazwa mshindi katika mnada ambaye atashindwa kuweka kwenye akaunti ya Baraza asilimia 25 ya bei ya manunuzi ndani ya muda uliotajwa kwenye | 4. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti linalomtaka mshindi wa mnada kuweka kwenye akaunti ya Baraza 25% ya jumla ya fedha ambayo ni bei ya mali iliyouzwa kwa mnada ndani ya siku moja ya kazi. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | **Kanuni ya 27(1).**<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 27(1)** haijaweka muda mahsusi ambao mshindi wa mnada atatakiwa kulipa asilimia 25 ya bei ya manunuzi.<br>Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko kuhusu wakati muafaka wa kufanya malipo yanayohusika.<br><br>5. **Kanuni ya 27 (4) (c)** inazungumzia utaratibu wa kurudisha kiwango cha asilimia 25 ya bei ya manunuzi ya tuzo kwa mshindi | <br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br><br>5. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha utaratibu wa kurejesha malipo yaliyozidi 25%. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | aliyeshindwa kumalizia malipo yote ya tuzo kama inavyoelekezwa na kanuni hizi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br><br>Kanuni haijabainisha utaratibu wa marejesho kwa mshindi aliyeshinda tuzo na kulipa kiwango cha juu zaidi ya asilimia 25 na kushindwa kumalizia kiasi kilichobaki.<br><br>Hali hii inaweza kusababisha kukosekana kwa mwongozo wa urejeshwaji wa kiwango cha fedha | |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kilichozidi asilimia 25, hivyo kusabibisha kero kwa wanaopaswa kurejeshewa fedha zao.<br><br>6. Kanuni haijabainisha utaratibu wa akidi ya vikao vya Kamati ya Uteuzi na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka wakati wa kufanya uamuzi. Hali hiyo inaacha ombwe na uwezekano wa uamuzi kufikiwa na Wajumbe wachache, hivyo kuathiri haki za Madalali wa Baraza | 6. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuonesha akidi ya vikao vya Kamati ya Uteuzi na Nidhamu kwa Madalali wa Baraza na Wasambaza Nyaraka. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | na Wasambaza Nyaraka. | |
| 5. | **(TS Na. 211)** 24/03/2023 | The Copyright and Neighbouring Rights (Royalty Collection and Distribution) (Collective Management Organisations) Regulations, 2023<br><br>(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 54G) | The Copyright and Neighbouring Rights Act, (Sura ya 218) | Wizara ya Utamaduni, sanaa na Michezo | 1. **Kanuni ya 3(1) na (2)(a)(b)** inaweka katazo la kuendesha CMO bila ya kuwa na leseni iliyotolewa kwa mujibu wa masharti yaliyowekwa na Kanuni.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni inaweka sharti la lazima kwa Mwenyekiti wa Bodi kuchaguliwa kutoka nje ya wanaounda CMO inayohusika. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta sharti la kulazimisha Mwenyekiti wa Bodi kuchaguliwa kutoka nje ya wanaounda CMO |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | 2. **Kanuni ya 16** inaipa uwezo CMO kupitia Mkutano Mkuu kuamua kuhusu kiwango cha ada ya kujiunga na uanachama.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imeweka utaratibu wa Mkutano Mkuu kuhusu kiwango cha ada ya kujiunga na uanachama kupata ithbati ya COSOTA. | 2. **Kanuni ya 16** ifanyiwe marekebisho ili kuondoa sharti la COSOTA kutoa ithbati kuhusu kiwango cha ada ya kujiunga na uanachama |
| | | | | | 3. **Kanuni ya 27** inazungumzia wajibu wa CMO kutoa taarifa kwa watumiaji wa haki miliki ambao wataomba Taarifa | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuweka fursa kwa CMO ilitakayoshindwa kutoa taarifa kwa sababu za msingi kusikilizwa kabla ya |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | za CMO inayohusika.<br><br>**Kanuni ya 27(4)** inaitaka CMO yeyote iliyoshindwa kutoa Taarifa ya kusahihisha makosa ya kutokutoa taarifa ndani ya muda maalum uliotolewa kulipa faini ya shilingi milioni mbili.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imetoa adhabu ya moja kwa moja pasipo kuonesha mbadala kwa CMO ambazo zinaweza kuwa na sababu za msingi kushindwa kuwasilisha Taarifa. Kulipishwa faini kwa | kuadhibiwa kwa mujibu wa masharti ya **Kanuni ya 27(4).** |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | CMO zilizo na sababu za msingi za kutowasilisha taarifa kunaweza kuwa na sura ya kudumaza ari na utendaji wa CMO zinazohusika. | |
| 6. | **(TS Na. 266)** 31/03/2023 | Kanuni za Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Kuingia Ndani ya Nchi na Kutoka Nje ya Nchi za Mwaka 2023<br><br>(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 106(1)(aa)) | Forest Act, (Sura ya 323) | Wizara ya Maliasili na Utalii | 1. **Sehemu (b) ya Jedwali la Pili** inazungumzia vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu kuingia na kutoka nchini kwa njia ya Reli.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sehemu hii haijaweka baadhi ya vituo vya kuingia na kutoka nchini kwa njia ya reli.<br>Hali hii inaweza kuwa kufifisha dhamira ya | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuonda orodha ya maeneo ya kuingia ndani ya nchi na nje na badala yake Kanuni itambue kutambua kwa ujumla maeneno hayo pasipo kuyataja. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Sheria Mama kuweka ulinzi wa maliasili za nchi.<br><br>2. **Sehemu (c) ya Jedwali la Pili** inazitaja Bandari ambazo zinatumika kama vituo vya kuingia na kutoka nchini.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haijazitaja bandari nyingine ambazo zinatumika kama vituo vya kutoka na kuingia nchini, Mfano Ziwa Nyasa na Ziwa Victoria.<br>Hali hii inaweza kuwa kufifisha dhamira ya Sheria Mama | 2. Ufafanuzi wa Waziri unahitajika kuhusu kutokutajwa bandari zinazotumika kama vituo vya kutoka na kuingia nchini. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kuweka ulinzi wa maliasili za nchi.<br><br>3. **Jedwali la Pili** linatambua vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu yanayosafirishwa ndani na nje ya nchi.<br><br>**Tatizo**<br>Jedwali halijatambua maeneo ya Viwanja vya Ndege kama maeneo yanayotambulika kuwa na vituo vya ukaguzi.<br><br>Kutokutajwa maeneo ya Viwanja vya Ndege kama maeneo ya ukaguzi | 3. Ufafanuzi wa Waziri unahitajika kuhusu kutokutajwa bandari zinazotumika kama vituo vya kutoka na kuingia nchini. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | wa mazao ya misitu, kunasabisha kutotambulika kisheria kwa maeneno hayo, hali inayoweza kutatiza malengo la sheria mama.<br><br>4. **Kanuni ya 14** inampa mamlaka Kamishna wa Uhifadhi kusitisha kibali chochote kilichotolewa chini ya Kanuni hizi. **Kanuni ya 14 (a) (b)** inaonesha sababu mojawapo kusitisha kibali ni iwapo mwenye kibali amekiuka masharti ya kanuni hizi. | <br><br><br><br><br><br><br><br>4. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu unaoruhusu mwenye kibali kurejeshewa kibali chake iwapo amefanya masahihisho kwenye jambo lililopekea leseni yake kusitishwa. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | <u>**Tatizo**</u><br>Kanuni haioneshi kama kuna uwezekano wa kibali kurejeshwa ikiwa aliyesitishiwa kibali amesahihisha makosa.<br><br>5. **Kanuni ya 16** inazungumzia kuhusu Rufaa dhidi ya uamuzi wowote uliofikiwa chini ya Kanuni hizi kuwa, itapelekwa kwa Waziri ndani ya siku 30 tangu kutolewa kwa uamuzi unaohusika.<br><br><u>**Tatizo**</u><br>Kanuni haitaji utaratibu wa namna | 5. Marekebisho yafanyike kuweka muda maalum ambao utatumiwa na Waziri kushughulikia Rufaa hizo. |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | ya kushughulikia rufaa ikiwemo *format* ya rufaa na muda ambao Waziri atapewa kufanyia kazi Rufaa inayohusika. Kukosekana kwa muda mahsusi kunaweza kusababisha Waziri ashughulikie shauri la rufaa kwa muda atakaoona unafaa, hali inayoweza kusababisha ucheleweshaji wa haki ya mrufani.<br><br>6. Kanuni hazitambui utaratibu wa kielektroniki wa kuwasilisha maombi ya vibali vya | 6. Marekebisho yafanyike katika Kanuni ili kuweka utaratibu wa kuwasilisha maombi |

| Na | Tangazo la Serikali | Jina la Sheria Ndogo | Sheria inayotoa madaraka | Mamlaka inayohusika | Yatokanayo na Uchambuzi | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | kusafirisha mazao ndani na je ya nchi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kukosekana kwa utaratibu wa kuwasilisha maombi ya vibali kwa njia ya kielektroniki kunaongeza urasimu, hivyo kuchelewesha uchakataji wa vibali vinavyohusika. | ya leseni kwa njia ya kielektroniki |

**KIAMBATISHO NA. 2**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**BUNGE LA TANZANIA**

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO**

**JEDWALI LA UTEKEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE KUHUSU SHERIA NDOGO ZILIZOWASILISHWA BUNGENI KATIKA MKUTANO WA NANE NA MKUTANO WA TISA.**

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI YA RAIS TAMISEMI** | | | | | |
| 1. | Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022<br><br>**(TS Na. 555)** | 1. **Kifungu cha 14(3)** kinaeleza kwamba, iwapo abiria atatupa taka nje ya chombo cha usafiri, kosa litachukuliwa kuwa limetendwa na mmiliki wa gari au dereva au kondakta. Aidha, kinaelekeza kuwa watu hao watalazimika kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushitakiwa mahakamani.<br><br>__**Tatizo**__<br>**Kifungu cha 14 (3)** kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine. Wanaodhibiwa | 1. **Kifungu cha 14(3)** kifanyiwe Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kumtaka mkosaji mwenyewe aweze kuadhibiwa kwa kosa alilolifanya. | 1. Marekebisho **ya Kifungu cha 14(3)** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya kwa mumuondoa mmiliki na dereva katika makosa yaliyotendwa na abiria. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 565 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | 1. Hatua iliyofikiwa ya kufanya marekebisho kwa kuwaondaoa mmiliki na dereva katika adhabu inayotokana na makosa ambayo hawajatenda ina akisi misingi ya haki ya mtu kuadhibiwa iwapo ametenda kosa na si vinginevyo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi na wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa. | | | |
| | | 2. **Kifungu cha 14** kinaweka adhabu kwa mmiliki wa gari au dereva au kondakta kulipa kiasi kisichozidi shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushtakiwa mahakamani ikiwa abiria anayesarifi katika chombo chao cha usafiri atatupa takataka.<br><br>Aidha, kifungu cha 23 kinatoa adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayetiwa hatiani | 2. **Kifungu cha 14** kifanyiwe marekebisho kwa kubainisha adhabu mahususi kwa kosa mahususi chini ya kanuni hii ili kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa kanuni hizi. | 2. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 2. Tatizo la Sheria Ndogo kuwa na adhabu za aina mbili linaendelea kuwepo hivyo linaweza kuleta mkanganyiko katika utekelezaji |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii kulipa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote viwili kwa pamoja.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria Ndogo imeweka adhabu mahsusi kwa makosa, lakini pia inaweka adhabu ya jumla kwa kosa lolote lililotendwa chini ya Sheria Ndogo hizi.<br><br>Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji kuhusu adhabu inayostahili kuadhibiwa mtu aliyekiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi. | | | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| 2. | Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022 | **Kifungu cha 8** kinachohusu muda wa kusafirisha mazao kinaonesha mtu yeyote, kikundi cha watu, kampuni au taasisi kusafirisha mazao kuanzia saa 1:00 jioni hadi saa 12:00 asubuhi.<br><br>**Tatizo**<br>Kifungu kimekosa ukamilifu wa sentensi, hivyo hakipo wazi kuhusu muda uliotajwa iwapo ni wa kusafirisha au unaokataza kusafirisha.<br><br>Kutokukamilika kwa sentensi na maelezo kuhusu muda wa kusafirisha mazao kunatatanisha masharti hayo kuhusu muda. | **Kifungu cha 8** kifanyiwe Marekebisho ili kubainisha muda mahsusi uliokusudiwa na kanuni hizi wakati wa usafirishaji wa mazao. | Marekebisho ya **Kifungu cha 8** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya ili kuonesha muda unakususiwa kusafirisha mazao.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 206 la tarehe 17 Machi, 2023).** | Hatua ya marekebisho iliyofikiwa itaondoa mkanganyiko kuhusu maudhui ya kifungu, vilevile mkanganyiko kuhusu muda unaoruhusiwa kusafirisha mazao. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| 3. | Sheria Ndogo ya Hifadhi ya Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, 2022 | 1. **Kifungu cha 3(1) (a)** kinaweka sharti kuwa mfugaji anayefuga ndani ya Halmashauri atapaswa kufuga mifugo kwa idadi itakayoamuliwa na Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Kigezo cha idadi ya mifugo kuamuliwa na Halmashauri hakina uhalisia.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Masharti ya Kifungu hiki yanaweza kuwa na tafsiri kwamba, Halmashauri inawapangia wananchi kiwango cha mali wanachopaswa kumiliki jambo ambalo linaacha ukakasi. | 1. **Kifungu cha 3(1) (a)** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mamlaka ya Halmashauri kuamua kuhusu idadi ya mifugo itakayofugwa na mtu anayeishi ndani ya eneo la Halmashauri hiyo. | 1. Marekebisho ya **Kifungu cha 3(1) (a)** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 203 la tarehe 17 Machi, 2023).** | 1. Hatua iliyofikiwa katika Marekebisho itasaidia kuondoa mtazamo wa halmashauri kuwapangia wananchi kiwango cha umiliki wa mali, aidha yataifanya sheria ndogo kuwa na vifungu vilivyo na uhalisia katika utekelezaji wake. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 2. **Kifungu cha 4(1) (a)** pamoja na mambo mengine kinaweka sharti kwa mtu anayetaka kufanya shughuli ya kilimo ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Sheria Ndogo haioneshi bayana nini maana ya kalenda ya Halmashauri. Hali hiyo, inasababisha kutokueleweka vizuri kwa sheria, jambo linaloweza kuwaathiri wananchi wakati wa utekelezaji.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Masharti yaliyowekwa yana muonekano | 2. **Kifungu cha 4(1) (a)** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa sharti la mtu anayetaka kufanya shughuli ndani ya Halmashauri kufuata kalenda ya Kilimo ya Halmashauri. | 2. Marekebisho ya **Kifungu cha 4(1) (a)** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 203 la tarehe 17 Machi, 2023).** | 2. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa mkanganyiko uliowekwa na kifungu hicho kuhusu kalenda ya kilimo iliyokusudiwa. Vilevile yanaondoa matazamo wa kuonekana kana kwamba, inawabana wananchi kutekeleza shughuli za kilimo kwa kuzingatia majira wanayoona yanayaafa. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | usiofaa kwa umma kwa kuondoa mnyumbuko wa shughuli za kilimo. Hii ni kutokana na kuwabana wananchi ili watekeleze shughuli za kilimo zilizopangwa na halmashauri. Hali hiyo, inaweza kufifiza juhudi za uzalishaji zinazofanywa na wananchi. | | | |
| 4. | Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2022 | **Sehemu H ya Jedwali la Kwanza** inabainisha viwango vya ushuru wa kituo cha mabasi kwa mchanganuo ufuatao:-<br>(i) Basi la abiria zaidi ya 40 (basi kubwa) litalipiwa shilingi 1000/-;<br><br>(ii) Basi la abiria ya zaidi ya 20 chini ya 40 (coaster) litalipiwa shilingi 1,000/-; | **Sehemu H ya Jedwali la Kwanza** ifanyiwe marekebisho ili kubainisha muda wa malipo ya ushuru wa kituo cha mabasi uliokusudiwa na kanuni hizi. | Marekebisho ya **Sehemu H ya Jedwali la Kwanza** yamefanyika kwa kufuta maneno ushuru wa **kituo cha mabasi** na bdala yake kuandika upya maneno hayo kama **ushuru wa kituo cha mabasi kwa siku**. Marekebisho yametangazwa | Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa uwezekano wa utozaji wa ada na ushuru pasipo kufuata miongozo ya kisheria. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Basi la abiria chini ya 20 (Hiace) litalipiwa shilingi 500/-; na<br><br>(iv) Magari madogo kama Taksi, Noah na mengine yatlipiwa shilingi 500/-.<br><br>**Tatizo**<br>Sheria ndogo haijabainisha iwapo viwango vya ushuru vitalipwa kwa siku au kwa tripu au vinginevyo. Kutokubainishwa kwa muda mahsusi wa malipo ya ushuru huo kunaweza kusababisha utozaji usiokuwa na mwongozo. | | kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 205 la tarehe 17 Machi, 2023).** | |
| 5. | Sheria Ndogo ya (Hifadhi ya Mazingira) ya Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale, 2022 | 1. **Kifungu cha 3** kinatafsiri neno "Taka hatari" kuwa ni taka ngumu, miminika na hewa ambazo zina kiwango kibubwa cha kemikali ambazo | 1. **Kifungu cha 3 k**ifanyiwe marekebisho ili kuendana tafsiri iliyopo kwenye **kifungu cha 3** cha Sheria Usimamizi wa | 1. Marekebisho **Kifungu cha 3** yamefanyika kwa kufuta **tafsiri ya neno taka hatari** na badala yake kuingiza tafsiri mpya | 1. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa ukinzani wa tafsiri ya neno **taka hatarishi** kati ya Sheria Ndogo hizi na Sheria ya Usimamizi |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | husababisha sumu na kuathiri maisha ya binadamu, viumbe wengine pamoja na mazingira kwa ujumla wake.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 3** ya Sheria Ndogo itoa tafsiri isiyojitosheleza ya maneno "taka hatarishi" Ikilinganishwa na tafsiri pana ya maneno hayo iliyo katika **Kifungu cha 3** cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. | Mazingira. | kama inayosomeka katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 202 la tarehe 17 Machi, 2023).** | wa Mazingira. |
| | | 2. Kifungu cha 3 kimetoa ufafanuzi kuhusu maana ya ardhi hatari ikihusisha maeneo ya vyanzo vya maji, maeneo ya barabara, | 2. **Kanuni ya 3** ifanyiwe marekebisho kwa kutoa tafsiri inayojitoshelea ya neno Hatarishi kama inavobainishwa katika | 2. Marekebisho **Kifungu cha 3** yamefanyika kwa kufuta tafsiri ya neno **ardhi hatari** Marekebisho | 2. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa ukinzani wa tafsiri ya neno taka hatarishi kati ya Sheria Ndogo hizi na |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | maeneo ya miteremko au maeneo yaliyotengwa na halmashauri kwa madhumuni yoyote yale.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimetumia neno hatari ambalo linaweza kuleta tafsiri isiyokusudiwa. | **Kifungu cha 3** cha Shria mama **(Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**) | yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 202 la tarehe 17 Machi, 2023).** | Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. |
| 6. | Sheria Ndogo za (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Mji Wa Bunda, 2022 | 1. Mtiririko wa vifungu vya Sehemu ya Tano vinaanzia **Kifungu cha 41** hadi **Kifungu cha 54**.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Katika mpangilio huo, Kifungu cha 43 kinakosekana. Hii inaweza kuwa, imetokana na makosa ya kiuchapaji au kusahaulika kwa kifungu | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo kwa kuweka mtiririko unaofaa/mzuri | 1. Azimio la Bunge limetekelezwa kwa kuweka upya mpangilio wa vifungu.<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika | 1. Hatua iliyofikiwa katika marekebisho iwapo itakamilika hadi kufikia hatua ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali itaondoa dosari ya mpangilio wa vifungu vya sheria hivyo kurahisisha usomaji wake. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | hicho. Hali inasababisha kutokuwepo kwa ukamilifu wa Sheria Ndogo hii. | | Gazeti la Serikali | |
| | | 2. **Kifungu cha 15** kinaweka sharti kwa wauzaji wa chakula kutumia masanduku ya mbao yaliyo na vioo kuhifadhia chakula.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimeweka sharti la matumizi ya masanduku ya mbao yenye vioo kuhifadhia chakula pasipo kuzingatia pia yapo masanduku ya aina nyingine. | 2. Marekebisho yafanyike ili kutambua aina nyingine za masanduku ya kuhifadhia vyakula. | 2. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 2. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza dosari ya Sheria Ndogo kutotambua aina nyingine za masunduku ya kuhifadhia chakula, hali inayoweza kuendeleza kero kwa wauza chakula wanaotumia wa masunduku ya kuhifadhia ya chakula yasiyo ya mbao na vioo. |
| | | 3. **Jedwali la Kwanza** linaloonesha kuwa limetokana na **Kifungu** | 3. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa | 3. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 3. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuna taswira ya |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **cha 25** linahusu ada ya ukaguzi wa afya. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.<br><br>__**Tatizo**__<br>**Jedwali la Kwanza** linarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 25** ambacho maudhui yake hayahusiani **Jedwali** hilo.<br><br>4. **Jedwali la Pili** linaloonesha kuwa limetokana na **Kifungu cha 31(1)** linahusu ada ya uzoaji taka kwa kaya, biashara na taasisi. Kwa kawaida | kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali husika.<br><br>4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali husika. | 4. Azimio la Bunge halijatekelezwa | kuendeleza matumizi ya Sheria iliyo na dosari katika uandishi wa majedwali, hali inayotatiza usomaji mzuri wa sheria ndogo.<br><br>4. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuna taswira ya |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Jedwali la Pili** linarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 31(1)** ambacho maudhui yake hayahusiani na **Jedwali** hilo.<br><br>5. **Jedwali la Tatu** linaloonesha kuwa limetokana na **Kifungu cha 45** linahusu ilani ya kuijenga choo. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha | 5. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali husika. | 5. Azimio la Bunge halijatekelezwa | kuendeleza matumizi ya Sheria iliyo na dosari katika uandishi wa majedwali, hali inayotatiza usomaji mzuri.<br><br>5. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuna taswira ya kuendeleza matumizi ya Sheria iliyo na |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | msomaji kwenye Jedwali linalohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Jedwali la Tatu** linarejea kuanzishwa chini ya Kifungu **cha 45** ambacho maudhui yake hayahusiani na **Jedwali** hilo.<br><br>6. **Jedwali la Nne** linaonesha kuwa limetokana na **Kifungu cha 47(1)** linahusu ilani yakuondoa kero. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika. | 6. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha Jedwali linalohusika. | 6. Azimio la Bunge halijatekelezwa | dosari katika uandishi wa majedwali, hali inayotatiza usomaji mzuri.<br><br>6. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuna taswira ya kuendeleza matumizi ya Sheria iliyo na dosari katika uandishi wa majedwali, hali inayotatiza usomaji mzuri. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tatizo**<br>**Jedwali la Nne** linarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 47(1)** ambacho maudhui yake hayahusiani **Jedwali** hilo.<br><br>7. **Jedwali la Tano** linaonesha kuwa limetokana na **Kifungu cha 52** linahusu hati ya kukiri kosa. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.<br><br>**Tatizo**<br>**Jedwali la Tano** linarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 52** | 7. Marekebisho yafanyike kwenye sheria ndogo hii kwa kuainisha kifungu kinachoanzisha hati/Jedwali husika la kukiri kosa. | 7. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 7. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuna taswira ya kuendeleza matumizi ya Sheria iliyo na dosari katika uandishi wa majedwali, hali inayotatiza usomaji mzuri. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ambacho maudhui yake hayahusiani **Jedwali** hilo. | | | |
| 7. | Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya Ya Songea, 2022 **(TS Na. 216)** | 1. **Kifungu cha 6 (6)** kimetumia neno "afisa masuuli" kuwa ndiye atakayetoa idhini ya kukamata na kuuza bidhaa au mali iliyokamatwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Neno "afisa masuuli" ni mamlaka ya Mkurugenzi wa Halmashauri katika masuala ya fedha na si jina la cheo kinachotambuliwa kwa mujibu wa Sheria.<br><br>2. **Sehemu T ya Jedwali la Kwanza** inabainisha viwango ushuru wa maegesho magari | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kufuta neno "afisa masuuli" na badala yake kuandika neno Mkurugenzi ili kuondoa mkanganyiko kati ya mamlaka na cheo cha ukurugenzi kinachotambulika kisheria.<br><br>2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kubainisha muda wa | 1. Marekebisho **ya Kifungu cha 6 (6)** yamefanyika kwa kufuta neno **Afisa masuuli** na badala yake kuandika neno **Mkurugenzi**. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 200 la tarehe 17 Machi, 2023).**<br><br>2. Marekebisho **ya Sehemu T ya Jedwali la Kwanza** yamefanyika kwa | 1. Marekebisho yaliyofanyika katika Kifungu cha 6(6) yanaondoa mkanganyiko kati ya mamlaka na cheo cha ukurugenzi kinachotambulika kisheria.<br><br>2. Hatua iliyofikiwa katika Marekebisho inaondoa uwezekano wa utozaji wa ada na |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | yanayobeba makaa ya mawe katika maeneo ya halmashauri kwa mchanganuo ufuatao:-<br>(i) Kuanzia tani 1 hadi tani 10 shilingi 1,000/-; na<br>(ii) Tani 10 nakuendelea shilingi 30,000/-.<br><br>**<u>Tatizo kwanza</u>**<br>Sheria ndogo haijabainisha iwapo viwango vya ushuru vitalipwa kwa siku au kwa kuegesha gari kwa mara moja au vinginevyo.<br>Kutobainishwa wa muda mahsusi wa malipo ya ushuru huo kunaweza kusababisha utozaji usiokuwa na muongozo. | ulipaji wa viwango vya ushuru na uzito wa gari ili kuondoa mkanganyiko utakaoleta changamoto katika utekelezaji wa sheria hii. | kuongeza maneno **kwa siku** mara baada ya maneno **kiwango cha ushuru**.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 200 la tarehe 17 Machi, 2023).** | ushuru pasipo kufuata miongozo ya kisheria. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Gari lenye uzito wa tani kumi linatajwa katika ushuru wa shilingi 1000/- halikadhalika katika ushuru wa shilingi 30,000/-. Hali inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji kuhusu ulipaji wa ushuru wa Gari lenye uzito wa tani 10. | | | |
| 8. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo, 2022 | **Sehemu (c) (ii) ya Jedwali la Kwanza** imeainisha viwango vya ada za kusafirisha mifugo kwa mchanganuo ufuatao:-<br>(i) Kusafirisha Mbuzi nje ya Halmashauri shilingi 1500/-;<br><br>(ii) Kusafirisha nguruwe nje ya Halmashauri shilingi 1500/-; | Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kubainisha idadi ya mifugo Iliyokusudiwa kutozwa ili kuweza kupata muongozo wa namna ya utozaji ushuru kwa usafirishaji wa mifugo. | Marekebisho ya **Sehemu (c) (ii) ya Jedwali la Kwanza** yamefanyika kwa kuweka maneno **kwa kila mmoja** katika safu ya mwisho ya vipengele Na. 4 na Na. 6.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 556 la** | Marekebisho yaliyofanywa yanaondoa uwezekano wa utozaji wa ada na ushuru pasipo kufuata miongozo ya kisheria |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (iii) Kusafirisha kuku/bata/kanga wakubwa nje ya Halmashauri shilingi 200/-; na<br><br>(iv) Kusafirisha vifaranga vya kuku/bata/kanga shilingi 1,000/-.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Viwango vya ada vilivyoainishwa havijaonesha iwapo vimekusudiwa kutozwa kwa mfugo mmoja mmoja au kwa idadi yoyote ya mifugo itakayosafirishwa nje ya Halmashauri.<br>Kutowekwa vema kwa namna ya ulipaji wa ada hizo kunasababisha kukosekana kwa muongozo wa utozaji, hali inayoweza kupunguza | | **tarehe 4 Agosti, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mapato ya halmashauri yatokanayo na ada ya mifugo inayohusika.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Uwezekano wa kukosekana kwa uhalisia wa namna ya ulipaji wa wa ada ya kusafirisha mifugo ndani ya Halmashauri | | | |
| 9. | Sheria Ndogo za Ada na Vibali vya Burudani za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 | 1. **Kifungu cha 4(4)** ya Sheria Ndogo hizi kinaweka utaratibu wa kuwasilisha Nakala ya kibali cha kufanya burudani katika eneo la halmashauri kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ikiwa na viambatisho vyote vinavyohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria Ndogo hii haijataja viambatisho | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha viambatisho vilivyolengwa ili kuondoa usumbufu kwa wananchi katika kutimiza takwa hili. | 1. **Kifungu cha 4(4)** kimefanyiwa marekebisho kwa kutaja kimbatisho kinachohusika kuwa **ni stakabadhi ya malipo ya ada ya kibali.**<br>Marekebisho haya yamefikia yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 566 la tarehe 4 Agosti,** | 1. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa mkanganyiko kuhusu kiambatisho kilichokusudiwa kuwasilishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 4(4). |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | vinavyotakiwa kuwasilishwa pamoja na nakala kwa mkuu wa polisi wa Wilaya. Kushindwa kutaja aina ya viambatisho vinavyotakiwa kuwasilishwa pamoja na kibali hiko kunaweza kusababisha usumbufu kwa wananchi katika kutimiza takwa hili. | | **2023).** | |
| | | 2. **Kanuni ya 8** inatoa wajibu kwa mtu yeyote au kikundi cha watu kinachotaka kufanya sherehe kwa kufunga barabara katika mtaa, kuomba na kupewa kibali cha kufunga barabara inayohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Tofauti na vibali vingine | 2. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza fomu maalum ya maombi ya kibali cha kufanya sherehe kwa kufunga barabara katika mtaa. | 2. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 2. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kunaendeleza changamoto iliyopo katika sheria ndogo ya kutoonesha aina ya fomu na gharama za kibali cha kufunga barabara, hali inaweza kusababisha ugumu katika utekekezaji. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ndani ya kanuni hizi, maombi ya kibali cha kufunga barabara hayajawekewa utaratibu wa kuwa na fomu maalumu pamoja na gharama zake. Hali hii inasababisha kutokukamilika kwa kanuni hii na kutatiza madhumuni yaliowekwa na sheria mama. Hali inayoleta changamoto wakati wa uombaji wa kibali na malipo ya kibali hicho. | | | |
| | | 3. **Jedwali la Kwanza** linaloonesha kuwa limetokana na **Kifungu cha 4(2)**, linahusu maombi ya burudani/sherehe/maonesho. Kwa kawaida Kifungu kinachotajwa | 3. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kufuta rejea ya **Kifungu cha 4 (2)** na kufanya rejea sahihi ya kifungu kinachoanzisha | 3. Kifungu cha 4 kimefanyiwa marekebisho kwa kufuta rejea ya **Jedwali la Kwanza** katika kifungu kidogo cha (2) na badala yake | 3. Hatua ya marekebisho iliyofikiwa inaondoa changamoto ya uandishi, hivyo kurahisisha usomaji mzuri wa Sheria Ndogo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuanzishwa kwa Jedwali huwa na maudhui yanayomrejesha msomaji kwenye Jedwali linalohusika.<br><br>__Tatizo__<br>**Jedwali la Kwanza** linarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 4(2)** ambayo maudhui yake hayahusiani na **Jedwali** hilo.<br>Urejeaji wa kanuni isiyoendana kimaudhui unakiuka matakwa yaliyowekwa na sheria ya utafsiri wa sheria inayoelekeza kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kujitosheleza kimadhumuni.<br>Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa | Jedwali. | kuweka rejea ya **Jedwali la Pili**.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 566 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | masharti ya kanuni na utekelezaji wa sheria mama.<br><br>4. **Jedwali la pili** la kanuni hizi linaainisha Ada za Burudani/ Sherehe/ Maonesho zitakazotozwa kulingana na viwango vya halmashauri hii.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>(i) **Kipengele cha 11,** hakitaji muda wa kutoza makusanyo ya asilimia 10% yatokanayo na Bahati nasibu. Kutokubainishwa kwa muda mahsusi wa malipo ya ya asilimia 10% kunaweza kusababisha utozaji | 4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha muda wa kutoza makusanyo ya asilimia 10 yatokanayo na bahati nasibu pamoja na kuweka viwango halisi vinavyo akisi uhalisia wa shughuli zilizokusudiwa. | 4. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 4. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge linaendeleza dosari ya Sheria Ndogo kutobainisha muda wa kutoza makusanyo ya asilimia 10 yatokanayo na bahati nasibu pamoja na pia, inaendeleza dosari ya kutoweka viwango halisi vinavyo akisi uhalisia wa shughuli zilizokusudiwa. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | usiokuwa na mwongozo na usiotabirika, jambo ambalo ni kunyume na kanuni za utekelezaji bora wa sheria.<br><br>(ii) Viwango vya ada ya vibali vya burudani vilivyoainishwa haviakisi uhalisia wa shughuli zilizokusudiwa.<br>Hali hii inaweza kusababisha kero kwa walengwa. | | | |
| 10. | Sheria Ndogo za Ushuru wa Stendi za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 | 1. **Kifungu cha 4(3)** kinaweka masharti kwa Mabasi na daladala zinazojishughulisha na shughuli za usafirishaji wa abiria ndani na nje ya Halmashauri kuanzia safari zake katika vituo | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kurekebisha **Kifungu cha 4 (3)** ili kubainisha kituo mahsusi cha daladala kinachotakiwa kuwa | 1. Marekebisho yamefanyika katika **Kifungu cha 4(3)** kwa kufuta na kukiandika upya kwa kutaja vituo vikuu vya mabasi na daladala | 1. Hatua iliyofikiwa ya kutaja vituo inaondoa mkanganyiko kuhusu vituo vya kuanzia mabasi na daladala ambapo ada na ushuru wa stendi utatozwa. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | vikuu vya mabasi au katika kituo cha daladala na si vinginevyo.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hii haijataja kituo mahususi cha daladala kinachotakiwa kuwa kituo cha kuanzia safari. Hali hii itasababisha Kukosekana kwa mwongozo sahihi katika maeneo ya kuanzia safari na kupelekea mkanganyiko kuhusu kituo kinachohusika na kutozwa kwa ada na ushuru wa stendi. | kituo cha kuanzia safari. | vitakavyohusika. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 565 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |
| | | 2. **Kifungu cha 8** kinaweka kosa kutembeza chakula katika eneo la Stendi. | 2. Marekebisho yafanyike Katika Sheria Ndogo hii kwa kuondoa **Kifungu cha 8** kinachozuia | 2. Marekebisho yamefanyika katika **Kifungu cha 8** kwa kufuta aya ndogo (b) ili kuondoa | 2. Hatua iliyofikiwa inaweza kupunguza changamoto ya utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tatizo**<br>Kifungu hakifafanui ni aina gani au namna ya utembezaji wa chakula unaokusudiwa. Hali hii inaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo hizi. | wananchi kutembeza chakula eneo la stendi. | katazo la kutemebza vyakula katika maeneo ya stendi.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 565 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |
| 11. | Sheria Ndogo za Ada ya Ukusanyaji na Uzoaji Taka za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 | 1. **Kifungu cha 4** kinaanzisha Jedwali la Kwanza linalohusu ada/tozo zitakazotozwa kwa ukusanyaji na uzoaji wa taka.<br><br>**Tatizo**<br>Jedwali hilo linataja viwango vya Tozo na ada zinazotakiwa kutozwa katika kata tano (5) tu kati ya kata kumi na nne (14) za halmashauri hii kama | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi ili kujumuisha Kata zote za Halmashauri zinazopaswa kulipa tozo ya ukusanyaji na uzoaji wa taka. | 1. Marekebisho yamefanyika katika **Jedwali la Kwanza** kwa kufuta kichwa cha habari na badala yake kuweka kichwa cha habari chenye maneno **maeneo ya kata zote za halmashauri**<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 565** | 1. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa tatizo la kutotambuliwa kwa kata zote za Wilaya ya Msalala katika ukusanyaji wa ada/tozo za ukusanyaji wa taka, hivyo kukidhi malengo ya sheria ndogo kukusanya ada na ushuru ya uzoaji taka kwa kata zote zilizopo katika |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ambavyo imeoneshwa kwenye kichwa cha habari cha jedwali.<br>Kwa kutokutaja kata nyingine zinazopatikana ndani ya halmashauri hiyo inamaanisha kwamba kaya ambazo zipo kwenye kata zisizo tajwa haziguswi na tozo/ ada zinazohusika.<br><br>Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kama ina kinzana na dhamira ya Bunge ya kuruhusu Sheria Ndogo zinazoweka mfumo sahihi na uliokamilika, wa kukusanya na kusimamia mapato ya ndani ya halmashauri. Aidha inaweza kusababisha hisia za wananchi ndani ya | | **la tarehe 4 Agosti, 2023).** | Halmashauri. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | halmashauri moja kuona wanabebeshwa mzigo Zaidi ya sehemu nyingine kutokana na kata nyingine kupendelewa. | | | |
| | | 2. **Kifungu cha 5** inaweka ulazima kwa kila kaya au kila mtu kuwa na chombo cha kutunzia taka ambacho kitakuwa na mfuniko na ukubwa ambao unakubalika na Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria hizi hazijabainisha ukubwa unaotakiwa kwa chombo cha kuwekea taka, jambo linaloweza kusababisha kutokueleweka kwa masharti kuhusu | 2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi kwa kubainisha vipimo na aina ya vyombo vinavyokusudiwa kwa ajili ya kutunzia taka ili kulinda afya ya wananchi. | 2. Marekebisho yamefanyika katika **Kifungu cha 5** kwa kufuta maneno **na ukubwa ambao unakubalika na Halmashauri** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 564 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | 2. Hatua ya Marekebisho inaweza kusaidia kurahisisha utekelezaji wa masharti ya sheria kuhusu vyombo vya kutunzia taka. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | chombo cha kuhifadhia taka.<br>Hali hii inaweka mkanganyiko katika utekelezaji wa Sheria Ndogo hizo. Jambo ambalo halina tija katika utungaji wa sheria. | | | |
| | | 3. **Kifungu cha 12** kinaweka adhabu ya jumla iwapo mtu atakiuka masharti yoyote yaliyowekwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa inajumuisha makosa ambayo tayari yana adhabu mahsusi kwa mujibu wa Sheria Mama na adhabu hizo ni | 3. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kurekebisha **Kifungu cha 12** ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo hayajawekewa adhabu mahsusi. | 3. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 3. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kunaendeleza doasri iliyopo katika Sheria Ndogo ya kujumuisha makosa ambayo tayari yana adhabu mahsusi kwa mujibu wa Sheria Mama na adhabu hizo ni ndogo ikilinganishwa na adhabu iliyopo katika Sheria Ndogo hizi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | ndogo ikilinganishwa na adhabu iliyopo katika Sheria Ndogo hizi. | | | |
| 12. | Sheria Ndogo za Udhibiti wa Uchimbaji wa Madini ya Ujenzi) za Halmashauri ya Wilaya ya Msalala, 2022 | 1. **Kifungu cha 7(1)** inazungumzia kuwa malipo ya ushuru wa madini ya ujenzi utalipwa kwa kuzingatia uzito wa madini yanayohusika.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Jedwali la Pili** lililotajwa na Kifungu cha 7(1) linaonesha viwango vya ushuru wa madini ya ujenzi kwa kuzingatia ujazo na si uzito.<br><br>Hali hiyo inaweza kuleta changamoto ya utekelezaji wa masharti ya Sheria Ndogo kuhusu kipimo kinachokusudiwa.<br><br>2. **Kifungu cha 8(4)** kinaweka sharti | 1. Kifungu kifanyiwe marekbisho ili kufuta neno **"uzito"** na badala yake kuandika neno **"ujazo"** ili kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa changamoto wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi<br><br>2. **Kifungu cha 8(4)** kifanyiwe | 1. Marekebisho **Kifungu cha 7(1)** yamefanyika kwa kufuta neno **uzito** na badala yake kuweka neno **ujazo.**<br><br>Marekebisho haya yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 563 la tarehe 4 Agosti, 2023).**<br><br>2. Marekebisho **Kifungu cha 8(4)** | 1. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa changamoto kuhusu tafsiri ya kipimo kilichokusudiwa na Sheria Ndogo hii<br><br>2. Marekebisho haya yanaondoa uwezo |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kwamba, ikiwa chombo kilichokamatwa kitakaa zaidi ya siku 30 bila mmiliki wake kukichukua, kitauzwa kwa njia ya mnada na baada ya mauzo, Halmashauri itakata fedha za faini na ushuru na gharama za ulinzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, na fedha zitakiazo baki baada ya makato atarudishiwa mmiliki wa chombo hicho.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria Ndogo haioneshi sharti la kupata idhini ya mahakama kabla ya kufanya mnada wa kuuza chombo kilichokamatwa.<br>Hali hiyo inaweza kusababisha kuuzwa kwa vyombo vya watu pasipo kufuata utaratibu wa kisheria. | marekebisho ili kuonesha sharti la kupata idhini ya Mahakama kabla ya kufanya mnada. | yamefanyika kwa kuongeza maneno **baada ya kupata idhini ya mahakama** mara baada ya neno **mnada.**<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 563 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | wa halmashauri kuuza mali za wananchi pasipo kufuata utaratibu wa kisheria wa kupata amri ya mahakama. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Jambo ambalo litakua kero kwa wananchi. | | | |
| 13. | Sheria Ndogo (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero, 2022 | 1. **Kifungu cha 9 (6)** na pamoja na **13 (iii)** cha Sheria Ndogo hizi kinaondoa/hakitoi uwajibikaji au wajibu wa Halmashauri kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kifungu cha 9(6)** kinaiondoa Halmashauri katika uwajibikaji kutokana na kupotea kwa mali iliyokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri hiyo. Kuondoa wajibu wa | 1. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kuweka sharti la Halmashauri kuwajibika iwapo hasara itatokana na uzembe wakati wa ukusanyaji madeni au mali. | 1. Marekebisho **ya Kifungu cha 9(6) na 13(iii)** yamefanyika kwa kuongeza maneno yanayoweka sharti la Halmashauri kuwajibika kwa hasara itakayosababishwa na Halmashauri. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 562 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | 1. Marekebisho yatasaidia kuongeza umakini kwa watumishi wa Halmashauri wakati wa kutekeleza majukumu yao. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Halmashauri kwa hasara ambayo inaweza kutokea kwa uzembe wa watumishi wake kunaweza kupunguza umakini wa kutokufuata utaratibu wa ukamataji na kuleta hasara kwa jamii ambayo ni kero isiyotakiwa.<br>Hili hiyo inaweza kuwakatisha tamaa wananchi katika kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kukiuka lengo la serikali la kuwezesha ustawi wa watu. | | | |
| | | 2. **Kifungu cha 15 (1)** kinaweka muda kupakia na kushusha abiria na mizigo stendi. | 2. **Kifungu cha 15 (1)** kifanyiwe marekebisho ili kuainisha muda uliokusudiwa kwa lengo la kuondoa | 2. Marekebisho **ya Kifungu cha 15 (1)** yamefanyika kwa kufuta maneno **saa alfajiri na** badala | 2. Hatua ya Marekebisho iliyofikiwa inaondoa mkanganyiko wa muda uliokusudiwa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimekosa ukamilifu kwa kutokuainisha muda mahsusi wa alfajiri uliokusudiwa.<br>Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji wa masharti yaliyokusudiwa na Sheria Ndogo hizi. | mkanganyiko unaoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi. | yake kuweka maneno **saa kumi na moja alfajiri.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 562 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | hivyo kurahisisha utekelezaji wa kifungu hiki. |
| | | 3. **Kifungu cha 15(2)** kinakataza gari la abiria kuendelea kuwepo stendi baada ya muda uliopangwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria Ndogo haijabainisha muda mahsusi uliopangwa kwa gari kuendelea kuwepo stendi.<br>Athari ya jambo hili ni | 3. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 15 (2)** kwa kubainisha muda uliopangwa kwa gari kuendelea kuwepo stendi. | 3. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 3. Kutokutekelezwa kwa azimio ni kuendeleza dosari ya Sheria Ndogo kutobainisha muda mahsusi uliopangwa kwa gari kuendelea kuwepo stendi.<br>Athari ya jambo hili ni kuendeleza uwezekano wa mkanganyiko kuhusu kueleweka kwa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | uwezekano wa mkanganyiko kuhusu kueleweka kwa muda uliopangwa miongoni mwa walengwa wa Sheria Ndogo hizi. | | | muda uliopangwa miongoni mwa walengwa wa Sheria Ndogo hizi. |
| | | 4. **Jedwali namba xix** lililotungwa chini ya **kifungu cha 4 (1**) na lenye kichwa cha habari "ADA YA KIBALI CA UPIMAJI WA AFYA", orodha ya nne ndani ya jedwali hilo iazungumzia ada ya kibali cha unyunyuziaji wa viatilifu kutolewakwa gharama ya shilingi 1,000,000/=<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Gharama iliyowekwa kwa kibali husika haiakisi uhalisia wa hali ya wananchi ambao ndio | 4. Marekebisho yafanyike katika **Jedwali namba xix** kwa kuandika gharama ya kibali inayo akisi uhalisia wa hali ya wananchi ambao ndio wanufaika wa zoezi la unyunyiziwaji. | 4. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 4. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza dosari ya Sheria Ndogo kuweka vifungu visivyo na uhalisia katika utekelezaji wake |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wanufaika wakubwa wa zoezi la unyunyiziwaji.<br>Hali hii inaweza kuleta shida katika utimilifu wa sheria hii katika matumizi yake.<br><br>5. Sheria Ndogo imeweka Majedwali ishirini na tatu yanayoonesha viwango mbalimbali vya ada na ushuru.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Majedwali yote yana dosari mbalimbali kama vile:-<br>(i) Viwango vya ada kutoakisi uhalisia wa mazingira ya walengwa;<br>(ii) Kukosa mtiririko mzuri mfano, kuchanganya | 5. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho kwa kupitia upya Majedwali yote ili kuondoa kasoro zilizobainika. | 5. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 5. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuhusu kufanya marekebisho katika katika Majedwali ya Sheria Ndogo ni kuendeleza dosari hizo hali inayoweza kusababisha ugumu wa utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa na sheria Mama ambayo imeanzisha Sheria Ndogo hizi |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | huduma na bidhaa, mpangilio wa namba; na<br><br>(iii) Kutokuainishwa kwa ukomo wa muda wa malipo ya ada na ushuru mbalimbali (mfano iwapo utozaji ni kwa siku, mwezi, wiki au mwaka) na kipimo cha ukubwa wa eneo (Mfano matumizi ya maneno ukumbi mkubwa na ukumbi mdogo).<br>Makosa ya Majedwali katika Sheria Ndogo hizi, yanaweza kuleta changamoto wakati wa utekelezaji na kusababisha kutotimia kwa malengo yaliyokusudiwa. | | | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 | 1. **Kifungu cha 5 (5)** cha Sheria Ndogo hizi kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo lolote na muda wowote kwa lengo la kukusanya ada au Ushuru.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Mamlaka anayopewa afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo muda wowote yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha.<br>Hali hiyo inasababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.<br><br>2. **Kifungu cha 5 (9)** cha Sheria Ndogo hizi kinaondoa/ hakitoi | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hizi kwa kubainisha muda ambao afisa muhidhiniwa anaruhusiwa kuingia katika jengo. Muda unaokusudiwa ni muda wowote ndani ya masaa ya kazi.<br><br>2. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuweka sharti la | 1. Marekebisho **ya Kifungu cha 5(5)** yamefanyika kwa kufuta maneno **wakati wowote** na badala yake kuweka maneno **kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jioni.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 561 la tarehe 4 Agosti, 2023).**<br><br>2. Marekebisho **ya Kifungu cha 5(9)** yamefanyika kwa | 1. Marekebisho yaliyofanyika yatondoa uwezekano uliokuwepo wa kukiukwa kwa haki za faragha.<br><br>2. Hatua ya Marekebisho iliyofikiwa itasaidia |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | uwajibikaji au wajibu wa Halmashauri kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kifungu cha 5(9)** kinaiondoa Halmashauri katika uwajibikaji kutokana na kupotea kwa mali iliyokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri hiyo. Kuondoa wajibu wa Halmashauri kwa hasara ambayo inaweza kutokea kwa uzembe wa watumishi wake kunaweza kupunguza umakini wa | Halmashauri kuwajibika kwa hasara itakayosababishwa na Halmashauri kwa mali iliyokamatwa au wakati wa ukusanyaji wa madeni. | kuongeza maneno yanayoweka sharti la halmashauri kuwajibika kwa hasara itakayosababishwa na Halmashauri. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 561 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | kuongeza umakini kwa watumishi wa Halmashauri wakati wa kutekeleza majukumu yao |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kutokufuata utaratibu wa ukamataji na kuleta hasara kwa jamii ambayo ni kero isiyotakiwa.<br>Hili hiyo inaweza kuwakatisha tamaa wananchi katika kufanya shughuli za kiuchumi na hivyo kukiuka lengo la serikali la kuwezesha ustawi wa watu. | | | |
| 15. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Nyumba za Kulala Wageni) za Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 | 1. **Kifungu cha 6 kinachoweka** masharti kwa mmiliki/mtunza Hoteli, kuzuia kitanda kimoja kutumika na wageni wawili au zaidi wa jinsia moja.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Masharti hayo yanaweza kukiuka uhalisia kama vile | 1. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kutoa ufafanuzi zaidi kuhusu wageni wa jinsia moja wanaoruhusiwa kutumia kitanda kimoja kama vile mama na mwanae au mama na Watoto wawili wa jinsia tofauti | 1. Marekebisho yamefanyika kwa kufuta **Kifungu cha 6.**<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 560 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | 1. Marekebisho haya yanaondoa uwezekano wa kusababisha ugumu katika utekelezaji na kati ya wananchi na wasimamizi wa nyumba hizo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | mahitaji ya mama kutumia kitanda kimoja na mtoto wake mdogo au mama na Watoto wadogo wawili wa jinsia tofauti hata kama ni wa jinsia moja.<br>Hali hiyo inaweza kusababisha ugumu katika utekelezaji wake kati ya wateja na wasimamizi wa nyumba hizo. | au mtu mzima anayemuuguza mtoto au mtu mzima wa jinsia moja lakini ni mgonjwa anayehitaji uangalizi na kuainisha watu wazima wa jinsia moja wasioruhusiwa kutumia kitanda kimoja. | | |
| | | 2. **Kifungu cha 7(b)** kinaweka jukumu kwa kila mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni kuhakikisha kuwa anaweka mahitaji ya msingi kwa wageni.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimeweka jukumu kwa mmiliki wa | 2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii katika **Kifungu cha 7(b)** ili kubainisha mahitaji ya msingi yanayotakiwa kuwekwa na mmiliki wa hoteli au nyumba ya kulala wageni ili kurahisisha utekelezaji wa masharti ya sheria | 2. Marekebisho ya **Kifungu cha 7** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho na kuandika upya kwa kuainisha mahitaji muhimu yanayopaswa kuwekwa na mmiliki wa hoteli.<br>Marekebisho | 2. Marekebisho yanaondoa mkanganyiko kuhusu mahitaji muhimu yaliyokusudiwa na kifungu hiki. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | hoteli au nyumba ya kulala wageni kuweka mahitaji mengine muhimu kwa wageni pasipo kuyaainisha au kuyataja. Kutoainishwa kwa mahitaji hayo kunaweza kusababisha mkanganyiko kwa walengwa kuhusu mahitaji yanayokusudiwa. | ndogo hizi na kuondoa mkanganyiko wakati wa utekelezaji. | yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 560 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |
| 16. | Sheria Ndogo za (Afya, Usafi na Usimamizi wa Mazingira) Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, 2022 | 1. **Kifungu cha 3** kinatafsiri neno "taka ngumu" kuwa ni kitu chochote ambacho baada ya kukitumia hakina thamani yoyote kwa jamii inayohusika, uwepo katika eneo husika unaweza kusababisha machukizo ya kiafya na kuhatarisha afya ya | 1. Tafsiri ya maneno "taka ngumu" ifanyiwe marekebisho ili kuendana na tafsiri iliyopo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. | 1. Marekebisho katika **Kifungu cha 3** yamefanyika kwa kufuta **tafsiri ya neno taka ngumu** na badala yake kuingiza tafsiri mpya kama inayosomeka katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Marekebisho | 1. Marekebisho yaliyofanywa yanaondoa ukinzani wa tafsiri ya neno taka ngumu kati ya Sheria Ndogo hizi na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, jambo ambalo ni utimizaji wa masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | jamii.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 3** ya Sheria Ndogo inatoa tafsiri isiyojitosheleza ya maneno "taka ngumu" Ikilinganishwa na tafsiri pana ya maneno hayo kama ilivyo katika **Kifungu cha 3** cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Hali hiyo inaweza kusababisha kutokutimia kwa masharti yanayokusudiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. | | yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 559 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | Sheria, Sura 1. |
| | | 2. **Kifungu cha 4(1)** kinaipa Halmashauri mamlaka ya kukagua nyumba yoyote, barabara, njia au uchochoro, mfereji | 2. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii ili kubainisha ukomo wa muda wa ukaguzi na | 2. Marekebisho yamefanyika katika **Kifungu cha 4(1)** kwa kufuta na kukiandika upya | 2. Marekebisho yanaondoa uwezekano uliokuwepo wa kusababisha matumizi |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wa maji ya mvua au ardhi yoyote katika eneno la Halmashauri kwa muda wowote na kuchukua hatua zozote itakazoona zinafaa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria Ndogo:-<br>(i) Haiweki ukomo wa muda kwa Halmashauri kukagua maeneo yanayohusika;<br><br>(ii) Haiweki ukomo wa hatua zitakazochukuliwa<br>Hali hiyo inaweza kusababisha matumizi mabaya ya mamlaka na kuleta kero kwa wananchi. | ukomo wa hatua zitakazochukuliwa mara baada ya ukaguzi kufanyika. | Kifungu hicho kwa kuweka muda maalum wa ukaguzi utakaoanzia **kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 559 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | mabaya ya mamlaka na kuleta kero kwa wananchi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 3. **Kifungu cha 17(1)** kinaweka sharti kuwa taka zote zitapaswa kuchambuliwa sehemu zinapotoka, katika makundi ya taka zenye madhara na zisizo na madhara.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu hakijaeleza muhusika anayepaswa kufanya uchambuzi wa taka. Hali hiyo inaweza kuleta mkanganyiko wa kimajukumu katika utekelezaji wa sharti hili. | 3. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 17 (1) cha Sheria Ndogo** hii kwa kubainisha muhusika anayepaswa kufanya uchambuzi wa taka. | 3. Marekebisho **Kifungu cha 17(1)** yamefanyika kwa kufuta na kukiandika upya Kifungu hicho kwa kuonesha kuwa anayepaswa kuchambua taka ngumu ni mzalishaji wa taka. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 559 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | 3. Hatua ya Marekebisho iliyofikiwa inaondoa mkanganyiko kuhusu mhusika anayepaswa kuchambua taka hivyo kurahisisha utekelezaji wa kifungu hiki. |
| | | 4. **Kifungu cha 20** kinaweka jukumu kwa kila mkazi kuhakikisha kuwa maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na salama kwa | 4. Marekebisho yanyike katika **Kifungu cha 20** kwa kubainisha jukumu la kila mkazi kuhakikisha kuwa maji yote yanayotumika kwa kunywa ni safi na | 4. Marekebisho **Kifungu cha 20** yamefanyika kwa kufuta maneno **kwa kuyachemsha bila kujali yametoka katika chanzo gani** | 4. Marekebisho haya yatasaidia kuleta maana iliyokusudiwa na kifungu kinachohusika. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuyachemsha bila kujali yametoka kwenye chanzo gani.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimetaja njia moja tu ya kuyafanya maji yawe safi na salama. Hali inayosababisha kutokutambua aina nyingine za kutibu maji ili kuwa safi na salama kwa kunywa. | salama. | **cha maji.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 559 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |
| | | 5. **Kifungu cha 23** cha sheria hii kinazungumzia uuzaji vyakula vilivyopikwa ambapo kinaweka amri ya kuhifadhi vyakula hivyo kwenye sanduku lililotengenezwa kwa mbao safi na kuwekewa kioo ili kuzuia | 5. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 23** cha Sheria Ndogo hii kwa kuongeza matumizi ya malighafi nyingine katika kuhifadhia chakula ikiwemo aluminiamu (alminium) na malighafi zingine | 5. Marekebisho **Kifungu cha 23** yamefanyika kwa kuongeza maneno **au kutumia malighafi nyingine katika kuhifadhi chakula** baada ya neno **binadamu** Marekebisho | 5. Marekebisho haya yatasaidia kuleta maana iliyokusudiwa na kifungu kinachohusika. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | inzi, vumbi na wadudu waletao madhara kwa afya ya binadamu.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Takwa la lazima la kuhifadhi vyakula hivyo kwenye sanduku la mbao na kuwekewa kioo linaweza kuleta changamoto hasa katika upatikanaji wa malighafi ya mbao ambayo kwa sasa kazi yake inaweza kufanywa na malighafi nyingine kama aluminiamu (*aluminium*). | zinazoweza kupatikana kwa kwa urahisi. | yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 559 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | |
| | | 6. **Kifungu cha 40 (1)** kinaweka kosa kwa mtu yoyote kufuga mfugo wa aina yoyote bila kuwa na kibali cha halmashauri. | 6. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 40 (1)** cha Sheria ndogo hii kwa kuonyesha sharti la idadi ya mifugo | 6. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 6. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza tatizo la mkanganyiko juu ya idadi ya mifugo inayopaswa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Tatizo**<br>Kifungu hakijaonesha sharti la idadi ya mifugo inayopaswa kuombewa kibali cha halmashauri.<br>Kutokuoneshwa kwa idadi ya mifugo kunaleta ugumu katika utekelezaji kwa watumiaji wa Sheria Ndogo hizi | inayopaswa kuombewa kibali cha Halmashauri. | | kuombewa kibali kwa mtu anayetaka kufuga ndani ya Halmashauri. |
| 17. | Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao) za Halmashauri ya Wilaya Nsimbo, 2022 | **Kifungu cha 10 (2)** cha sheria hii kinazungumzia fomu maalum ya kibali cha ununuzi wa Mazao.<br><br>**Tatizo**<br>Fomu maalumu inayotajwa na kifungu hiki haijawekwa ndani ya sheria hizi.<br>Hali hii inasababisha kutokukamilika kwa Sheria hii na kutatiza madhumuni yaliowekwa na sheria mama. | Marekebisho yafanyike kwa kuongeza Nyongeza ya fomu maalum ya maombi ya kibali cha ununuzi wa mazao. | Marekebisho yamefanyika kwa kuweka fomu maalumu katika Jedwali la Tatu inayotajwa katika **Kifungu cha 10(2).** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 558 la tarehe 4 Agosti, 2023).** | Marekebisho yaliyofanyika yanaleta ukamilifu wa Sheria Ndogo hivyo kukidhi madhumuni yaliyokusudiwa na Sheria Mama. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| 18. | Sheria Ndogo (Hifadhi ya Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, 2022 | 1. **Kifungu cha 7** cha sheria kinampa uwezo afisa mwidhiniwa kuingia katika nyumba au jengo lolote kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Mamlaka anayopewa afisa mwidhiniwa kuingia katika jengo muda wowote yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha.<br>Hali hiyo inaweza kusababisha kero kwa wananchi wanaowakilishwa na Bunge.<br><br>2. **Kifungu cha 9(2)** kimeweka katazo la | 1. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 7** cha Sheria Ndogo hii ili kubainisha ukomo wa muda wa ukaguzi unaofanywa na afisa mwidhiniwa kufanyika muda wa saa za kazi.<br><br>2. Sheria ndogo ifanyiwe marekebisho ili | 1. Rasimu ya Marekebisho imeandaliwa kwa kufuta maneno **wakati wowote** na badala yake kuweka maneno **kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri.**<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali<br><br>2. Rasimu ya Marekebisho | 1. Iwapo mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika utafika hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali, itaondoa uwezekano uliokuwepo wa kukiukwa kwa haki za faragha.<br><br>2. Iwapo mchakato wa Marekebisho |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | kuchinja mifugo mahali ambapo si machinjio. Aidha, kimeweka gharama za machinjio.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu:-<br>(i) Kimeweka ada ya machinjio kwa mbuzi na ng'ombe pekee; na<br>(ii) Kimeweka ada ya machinjio badala ya kuweka katika Jedwali. | kuweka Jedwali litakaloainisha viwango vya ada ya machinjio na kuongeza idadi ya mifugo inayokusudiwa. | imeandaliwa kwa kukifuta kifungu cha 9(2) na kukiandika upya kwa kuweka utaratibu unaoruhusu kuchinja mifugo sehemu ambayo si machinjio ni baada ya kutoa taarifa. Vilevile marekebisho yamefanyika kwa kuanzisha Jedwali jipya la Nne linaloonesha gharama za uchinjaji na limeanzishwa. | yaliyofanyika utafika hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali yataondoa mkanganyiko kuhusu gharama za uchinjaji wa mifugo na pia yataondoa dosari za uandishi. |
| 19. | Sheria Ndogo (Afya na Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, 2022 | 1. **Kifungu cha 6(5)** kinatoa wajibu kwa dereva na mmiliki wa chombo cha usafiri kuweka chombo cha kutupia taka ndani ya gari na kuhakikisha | 1. **Kifungu cha 6(5)** kifanyiwe marekebisho ili kutenganisha wajibu wa dereva na mmiliki wa gari kuwajibika na kosa linalotokana na kutoweka chombo cha | 1. Marekebisho **ya Kifungu cha 6 (5)** yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya ili kutenganisha wajibu wa dereva | 1. Marekebisho yaliyofanyika yatondoa mkanganyiko kuhusu anayepaswa kuadhibiwa kwa kosa la utupaji wa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zinatupwa katika sehemu maalumu iliyotengwa na Halmashauri.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimeweka wajibu wa jumla kwa mmiliki na dereva kuwajibika na kosa linalotokana na kutoweka chombo cha kutupa taka ndani ya gari pasipo kutenganisha wajibu huo.<br>Hali hiyo inaweza kusababisha mmiliki kuwajibika kwa kosa lililotendwa na dereva. | kutupa taka ndani ya gari. | na mmiliki wa gari kuwajibika na kosa linalotokana na kutoweka chombo cha kutupa taka ndani ya gari.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 553 la tarehe 17 Machi, 2023).** | takataka nje ya vyombo vya usafiri. |
| | | 2. **Kifungu cha 14** cha sheria hizi kinazungumzia wajibu na jukumu la afisa | 2. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 14** cha Sheria Ndogo hii ili | 2. Marekebisho ya **Kifungu cha 14** yamefanyika kwa kufuta maneno | 2. Marekebisho yatondoa uwezekano uliokuwepo wa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | mwidhiniwa wa Halmashauri ikiwemo jukumu la ukaguzi wa majengo au maeneo.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Katika Kifungu hicho, afisa mwidhiniwa amepewa mamlaka ya kuingia eneo lolote wakati wowote bila kuwekewa kikomo cha muda wa kutimiza jukumu hilo.<br>Mamlaka anayopewa afisa muhidhiniwa kuingia katika jengo muda wowote yanaweza kusababisha ukiukwaji wa haki ya msingi ya faragha. | kuweka ukomo wa muda wa ukaguzi unaofanywa na afisa mwidhiniwa. Sheria ndogo itasisitiza Ukaguzi huo kufanyika wakati wa saa za kazi ili kulinda haki ya msingi ya faragha. | **wakati wowote** na badala yake kuweka maneno **kuanzia saa 1:30 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 553 la tarehe 17 Machi, 2023).** | kukiukwa kwa haki za faragha kama ingelikuwa hakuna ukomo wa muda wa ukaguzi wa majengo na maeneo ya halmashauri. |
| | | 3. **Kifungu cha 20 (1)** kinaweka sharti kwa wauza vyakula katika | 3. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 20 (1)** | 3. Marekebisho **ya Kifungu cha 20(1)** yamefanyika kwa | 3. Marekebisho yatondoa uwezekano wa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | magenge, jengo lolote la chakula au vinywaji kupimwa afya zao mara moja kila mwezi na kuwa na sare wakati wote akiwa kazini.<br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu kimeweka sharti la upimaji wa afya kila mwezi. Hali inaweza kuchochea kero kwa walengwa. | **cha Sheria Ndogo** kwa kubadilisha muda wa upimaji wa afya kutoka kila mwezi na kuwa kila baada ya miezi sita. | kufuta maneno **kila mwezi** na badala yake kuweka maneno **kila baada ya miezi sita.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 553 la tarehe 17 Machi, 2023).** | kusababisha kero kwa walengwa wa kupima afya kila baada ya mwezi mmoja. |
| | | 4. **Kifungu cha 21 (2)** kinatoa sharti kwa kila mmiliki wa Nyumba kuweka madirirsha yasiyopungua 1/8 ya ukubwa wa chumba.<br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kipimo kilichowekwa cha 1/8 ya ukubwa wa chumba kinakinzana na vipimo vya kawaida | 4. Marekebisho yafanyike katika Sheria Ndogo hii kwa kuweka vipimo sahihi vya uwiano wa madirisha kwa ukuta au sakafu. | 4. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 4. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza dosari ya kukosekana kwa uhalisia wa vipimo vya ukubwa wa madirisha vilivyowekwa na Sheria Ndogo ikilinganishwa na uhalisia wa ukubwa wa majengo ambayo |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | vya ukubwa wa madirisha ambavyo hutegemea ukubwa wa ukuta ama ukubwa wa sakafu.<br><br>5. **Kifungu cha 22 (6)** cha sheria hii kinaorodhesha makosa mbalimbali ambayo yataadhibiwa ndani ya sheria hiyo. Kifungu kidogo cha sita cha kifungu 22 (6) kinataja kosa kwa mtu yeyote kuuza vyakula kwa kubeba katika ndoo, sufuria au beseni hata kama vimefunikwa.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria hii haijaweka mwongozo wa vibebeo ambavyo halmashauri inaruhusu kutumika. | 5. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 22 (6)** cha Sheria Ndogo hii kwa kuweka bayana mwongozo wa aina ya vibebeo vinavyoruhusiwa kutumika kwa ajili ya kubebea vyakula vya kuuza. | 5. Marekebisho **ya Kifungu cha 22(6)** yamefanyika kwa kufuta maneno **hata kama vimefunikwa** na badala yake kuweka maneno **tofauti na muongozo au maelekezo yaliyotolewa na halmashauri.** Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 553 la tarehe 17 Machi, 2023).** | kimsingi hutofautiana.<br><br>5. Marekebisho yatondoa utata kuhusu vyombo vingine zaidi ya kabati vilivyotajwa, na hivyo kusababisha ugumu wa utekelezaji wa sheria. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hali hii inaleta utata kuhusu vyombo vingine zaidi ya kabati la kioo vilivyotajwa katika kifungu cha 22(1), na hivyo kusababisha ugumu wa utekelezaji wa sheria. | | | |
| 20. | Sheria Ndogo za (Usafi wa Mazingira) za Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi, 2022 | 1. Kifungu cha 3 kinatoa Tafsiri ya neno "Taka ngumu'' <br>**<u>Tatizo</u>**<br>Tafsiri iliyowekwa kwenye kanuni hii inatofautiana na Tafsiri iliyopo kwenye sheria ya usimamizi wa Mazingira. | 1. Tafsiri ya maneno "**taka ngumu**" ifanyiwe marekebisho ili kuendana tafsiri iliyopo Sheria Usimamizi wa Mazingira. | 1. Rasimu ya Marekebisho ya **Kifungu cha 3** imeandaliwa kwa kufuta tafsiri ya neno **taka ngumu** na badala yake kuingiza tafsiri mpya kama inayosomeka katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 1. Ikiwa mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika ukikamilika yanaondoa ukinzani wa tafsiri ya neno **taka hatarishi** kati ya Sheria Ndogo hizi na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali | |
| | | 2. **Kifungu cha 8 (2)** kinaeleza kwamba itakuwa ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au stendi. Aidha **kifungu kidogo cha 3** kinaeleza kuwa Mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu hamsini baada ya kujaziwa fomu ya ilani na afisa mwidhiniwa wa Mji endapo abiria aliyeko ndani ya gari lake atatupa uchafu | 2. Marekebisho yafanyike ili kuweka adhabu kwa abiria aliyeko ndani atakayetupa taka au kitu chochote stendi au barabarani badala ya mwenye basi au dereva. Aidha sheria ndogo itaweka wajibu wa Kondakta au Dereva kuhakikisha anaweka chombo ndani ya gari kwa ajili ya abiria kutupa taka na kuwapatia elimu abiria ya umuhimu wa kutupa taka kwenye chombo hicho. | 2. **Rasimu ya** Marekebisho **ya Kifungu cha 8 (2)** imeandaliwa kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya na kuweka adhabu kwa abiria kwa kosa la kutupa takataka barabarani au stendi.<br><br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika | 2. Marekebisho yakitangazwa katika Gazeti la Serikali yatawaondoa mmiliki na dereva katika adhabu inayotokana na makosa ambayo hawajatenda ina akisi misingi ya haki ya mtu kuadhibiwa iwapo ametenda kosa na si vinginevyo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | katika barabara au kituo cha mabasi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kifungu hiki kinawapa adhabu watu kwa makosa ya wengine. Wanaoadhibiwa hawana namna ya kumzuia mkosaji halisi na wala sio waliomshawishi mkosaji kutenda kosa.<br><br>Hali hiyo haizuii kosa kurudiwa na mfanyaji wa kosa wala mtu mwingine kwasababu atakayeadhibiwa siye mtenda kosa. | | Gazeti la Serikali | |
| | | 3. **Kifungu cha 22 (2)** kinaweka adhabu ya jumla kwa mtu yeyote atakayevunja Sheria | 3. Marekebisho yafanyike kwa kuweka kifungu kimoja tu chenye adhabu ya | 3. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 3. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge kuendeleza mkanganyiko kuhusu |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndogo hizi ambapo kinatamka Mtu atakayevunja masharti ya Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichozidi shilingi laki mbili au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyotolewa na kifungu hicho inatofautiana na adhabu ya jumla iliyo katika kifungu cha 36(1) ambayo ni faini isiyopungua shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja. Hali hii inaleta mkanganyiko kuhusu adhabu ya jumla iliyokusudiwa na Sheria | jumla. | | adhabu ya jumla iliyokusudiwa na Sheria Ndogo hizi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Ndogo hizi.<br><br>4. **Kifungu cha 39 (3)** kinatoa sharti kwa kila mmiliki wa Nyumba kuweka madirirsha yasiyopungua 1/8 ya ukubwa wa chumba.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kipimo kilichowekwa cha 1/8 ya ukubwa wa chumba kinakinzana na vipimo vya kawaida vya ukubwa wa madirisha ambavyo hutegemea ukubwa wa ukuta ama ukubwa wa sakafu**.** | 4. Marekebisho yafanyike kwa kuweka sharti la mmiliki wa nyumba kutumia vipimo vya madirisha kutegemeana na ukubwa wa ukuta ama sakafu. | 4. **Rasimu ya** Marekebisho **ya Kifungu cha 39 (3)** imeandaliwa kwa kufuta **kipimo cha 1/8** na badala yake kuweka maneno **vipimo vya madirisha kutegemeana na ukubwa wa madirisha au sakafu**.<br><br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali | 4. Ikiwa mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika ukikamilika utaondoa changamoto ya utekelezaji wa sharti la kipimo cha 1/8. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 5. **Kifungu cha 40 (ii)** kinazungumzia muda uliopangwa kwa siku ya usafi ya jumamosi ya mwisho wa mwezi na kutaja muda wa kuanzia saa 12:00 asubuhi mpaka saa 4:00 asubuhi na kuweka sitisho la shughuli yeyote kufanyika ndani ya muda huo.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Muda uliotengwa kwa shughuli za usafi katika jumamosi ya mwisho wa mwezi na kuweka zuio la shughuli zote za kijamii na kiuchumi ni muda mrefu.<br>Hali hii itaathiri uendeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwa kiwango cha kuwa | 5. Marekebisho yafanyike katika **Kifungu cha 40 (ii**) cha Sheria Ndogo hii kwa kuweka masharti ya kushiriki katika shughuli za usafi pasipo kuathiri shughuli za kijamii na kiuchumi siku ya usafi. | 5. **Rasimu ya Marekebisho ya Kifungu cha 40 (ii) kwa kuondoa zuio la kufanyika shughuli za kijamii, kibiashara na kiuchumi siku ya usafi**<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali | 5. Ikiwa mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika ukikamilika utaondoa kero katika uendeshaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi kwa wananchi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kero kwa wananchi.<br><br>6. **Jedwali la Kwanza** linahusu ada za huduma za usafi na uzoaji taka.<br><br><u>**Tatizo**</u><br>Jedwali lina makosa katika:-<br>(i) **Kipengele cha 9** kimetaja mitandao kwa majina na kuacha mitandao mingine;<br><br>(ii) Mpangilio wa namba za vipengele vya majedwali hazina mtiririko;<br><br>(iii) **Kipengele cha 39** kwa kuweka gharama zisizoakisi uhalisia wa shughuli | 6. Sheria Ndogo ifanyiwe marekebisho ili kuondoa dosari zilizobainishwa. | 6. **Rasimu ya** Marekebisho **ya Jedwali la Kwanza** imeandaliwa kwa kuondoa maneno **tigo pesa na m-pesa** na badala yake kuandika neno **fedha mtandao.** Aidha, marekebisho yamefanyika **kwa kupunguza ada na ushuru wa huduma za usafi na uzoaji taka kwa mashine ya mbao.**<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na | 6. Ikiwa mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika ukikamilika utaondoa mkanganyiko kuhusu maduka ya fedha yaliyokusudiwa, uhalisia wa masharti ya sheria wakati wa utekelezaji na viwango vya ada vinavyopaswa kulipwa. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zinazotekelezwa; na<br><br>(iv) **Kipengele cha 42** hakina maelezo yoyote kuhusu kiwango cha ada.<br>Dosari hizo zinaweza kusababisha mkanganyiko wa usomaji na utekelezaji wa Sheria Ndogo. | | kutangazwa katika Gazeti la Serikali | |
| 21. | Sheria Ndogo (Ushuru wa Madini ya Ujenzi na Shughuli za madini ya vito) za Halmashauri ya wilaya ya Misungwi 2022. | 1. **Kifungu cha 4(1)** kinatoa wajibu kwa mtu anayekusudia kuanzisha machimbo ya madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri kutoa taarifa kwa Halmashauri ili eneo hilo likaguliwe.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Sheria hiyo imetumia maneno "**utaenda kinyume**". Maneno hayo hayaleti maana | 1. **Kifungu cha 4(1)** kifanyiwe marekebisho kwa kuondoa maneno "**utaenda kinyume**" na badala yake kuweka maneno yenye maana iliyokusudiwa na Kifungu hiki. | 1. **Kifungu cha 4(1)** kimefanyiwa marekebisho kwa kufuta maneno **"utaenda kinyume"** na badala yake kuweka maneno **"utaenda sawa"**<br><br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu | 1. Ikiwa mchakato wa Marekebisho yaliyofanyika yatakamilika yataondoa dosari ya uandishi hivyo kuleta maana iliyokusudiwa na Sheria |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | iliyokusudiwa na Kifungu hiki. | | wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali | |
| | | 2. **Kifungu cha 6(2)** kimefanya rejea ya Jedwali la Pili linalohusu viwango vya ushuru wa kusafirisha madini ya ujenzi.<br>**<u>Tatizo</u>**<br>Jedwali la Pili linalorejewa halipo katika Sheria Ndogo hizi. Kutokuwepo kwa Jedwali hili kunaondoa ukamilifu wa Sheria Ndogo, hali inayoweza kuathiri malengo yaliyokusudiwa. | 2. Marekebisho yafanyike katika Kifungu cha 6 (2) kwa kuweka Jedwali la Pili lenye kuonesha viwango vya ushuru wa kusafirishia madini ya ujenzi. | 2. Marekebisho yamefanyika katika **Kifungu cha 6(2)** kwa kufuta maneno **"katika Jedwali la Pili"** na badala kuweka maneno **"Katika Jedwali la Kwanza"**<br><br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali | 2. Mchakato wa marekbisho ukifika hatua ya kutangazwa utaondoa makosa ya rejea ya majedwali hivyo kurahisisha usomaji wa Sheria Ndogo hii |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 3. **Jedwali Kwanza B** linahusu ada ya kibali cha kuchimba madini.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Jedwali halijaonesha viwango vya ada vitalipwa kwa muda gani au utaratibu upi (Siku, Mwezi, Mwaka au kwa tripu).<br>Kutokuainishwa kwa muda au utaratibu wa utozaji kunaweza kusababisha utozaji wa ada usio na muongozo. | 3. Jedwali lifanyiwe marekebisho katika Jedwali ili kuonesha muda wa ulipaji wa viwango na utaratibu wa ulipaji wake. | 3. Marekebisho ya **Jedwali la Kwanza B** yamefanyika kwa kuongeza maneno **"kwa mwaka mmoja"**<br>Rasimu ya marekebisho imewasilishwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki na kutangazwa katika Gazeti la Serikali. | 3. Ikiwa marekebisho yatafika katika hatua ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali yataondoa uwezekano wa utozaji wa ada usio na muongozo |
| **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI** | | | | | |
| 22. | The Merchant Shipping (Maritime Labour) Regulations, 2022 | **Kanuni ya 83** inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusi inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu | **Kanuni ya 83** inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla iliyowekwa na sheria mama. | **Kanuni ya 83** imefanyiwa marekebisho kwa:-<br>(i) Kufuta adhabu ya Dola za Marekani 500 na kuweka adhabu ya Dola za | Utekelezaji wa azimio hili utawezesha kanuni kutekeleza malengo ya sheria mama kama yalivyolengwa na Bunge wakati wa utunzi wake |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | huyo atapaswa kulipa faini kwa shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.<br><br>Vilevile **Kifungu cha 401** cha sheria mama, kimeweka kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusi kinachoweka adhabu. Mhusika aliyekiuka sheria mama atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenye thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja. | | Marekani 1000; na<br><br>(ii) Kufuta kifungo kinachozidi miezi (6) na badala yake kuweka adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita (6).<br><br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 161 la tarehe 10, Machi, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyoowekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni kwenye:-<br>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama; na<br>(ii) Adhabu ya kifungo inayowekwa na Sheria Ndogo ni kubwa kuliko iliyowekwa katika Sheria Mama. | | | |
| 23. | *The Merchant Shipping (Seafarers' Identity Document) Regulations, 2022* | **Kanuni ya 26** inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusi inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu | **Kanuni ya 26** inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla iliyowekwa na sheria mama. | **Kanuni ya 26** imefanyiwa marekebisho kwa:-<br>(i) Kufuta adhabu ya Dola za Marekani 200 na isiyozidi Dola za Marekani 500 na | Utekelezaji wa azimio hili utawezesha kanuni kutekeleza malengo ya sheria mama kama yalivyolengwa na Bunge wakati wa utunzi wake |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | huyo atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 200 na isiyozidi shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.<br>**Kifungu cha 401** cha sheria mama, kimeweka kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusi kinachoweka adhabu. Mhusika aliyekiuka sheria mama atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania zenye thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiozidi miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja. | | adhabu ya kuweka ya Dola za Marekani 1000; na<br>(ii) Kufuta kifungo cha miezi (6) na badala yake kuweka adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita (6).<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 162 la tarehe 10, Machi, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyoowekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni kwenye:-<br>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama; na<br><br>(ii) Sheria Ndogo imelazimisha adhabu ya miezi sita ili hali Sheria Mama imeruhusu busara ya kuamua adhabu kifungo chini ya miezi sita. | | | |
| 24. | *The Merchant Shipping (Continous Discharge Certificate)* | **Kanuni ya 21** inaweka adhabu ya jumla, iwapo mtu amekiuka masharti yoyote ya Kanuni ambapo hakuna kanuni mahsusi | **Kanuni ya 21** inayotoa adhabu ya jumla ifanyiwe marekebisho ili kuendana na matakwa ya adhabu ya jumla | **Kanuni ya 21** imefanyiwa marekebisho kwa:-<br>(i) Kufuta adhabu ya Dola za Marekani | Utekelezaji wa azimio hili utawezesha kanuni kutekeleza malengo ya sheria mama kama yalivyolengwa na Bunge |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | *Regulations, 2022* | inayoweka adhabu ya kukiuka masharti hayo, mtu huyo atapaswa kulipa faini isiyopungua shilingi za Tanzania ambazo ni sawa na dola 200 na isiyozidi shilingi za kitanzania ambazo ni sawa na dola 500 au kifungo cha miezi sita au adhabu zote kwa pamoja.<br><br>**Kifungu cha 401** cha sheria mama, kimeweka kifungu cha jumla cha adhabu iwapo mtu atakiuka masharti ya sheria hiyo na hakuna kifungu mahsusi kinachoweka adhabu. Mhusika aliyekiuka sheria mama atapaswa kulipa faini ya shilingi za Tanzania zenye thamani ya dola 1000 za kimarekani au kifungo cha muda usiozidi | iliyowekwa na sheria mama. | 200 na isiyozidi Dola za Marekani 500 na kuweka adhabu ya Dola za Marekani 1000; na<br><br>(ii) Kufuta kifungo kinachozidi miezi (6) na badala yake kuweka adhabu ya kifungo kisichozidi miezi sita (6).<br><br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 160 la tarehe 10, Machi, 2023).** | wakati wa utunzi wake |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa katika Kanuni inakinzana na adhabu iliyoowekwa na Sheria Mama. Kukinzana huko ni kwenye:-<br>(i) Kiasi cha faini kilichotajwa kwenye Sheria Ndogo ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichotajwa katika sheria Mama; na<br><br>(ii) Sheria Ndogo imelazimisha adhabu ya miezi sita ili hali Sheria Mama imeruhusu busara ya kuamua adhabu ya kifungo chini ya miezi sita. | | | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| **OFISI YA MAKAMU WA RAIS , MUUNGANO NA MAZINGIRA** | | | | | |
| 25. | *The Environmental Management (Prohibition of Plastic Carrier Bags and Plastic Bottle Cap Regulations , 2022* | **Kanuni ya 32** inatoa fursa kwa mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wowote uliotolewa chini ya Kanuni hizi ya kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku thelathini baada ya uamuzi.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Kanuni haijaweka muda mahsusi ambao Waziri atashughulikia shauri la rufaa.<br>Hali hiyo inaweza kutoa mwanya wa ucheleweshaji wa mashauri ya rufani.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Kanuni hazijaonesha muundo wa hati ya kukata rufaa, jambo linaloacha utatanishi katika ukataji wa | **Kanuni ya 32** ifanyiwe marekebisho kwa kubainisha muda mahsusi ambao Waziri atautumia kushughulikia shauri la rufaa. | Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo, Rasimu ya marekebisho ya **Kanuni ya 32** imeandaliwa kwa kuweka muda wa Waziri kushughulikia rufaa kuwa ni siku 14.<br><br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki. | Iwapo Marekebisho haya yatakamilika, yataondoa hatari ya matumizi ya mamlaka ya kikanuni yasiyo na ukomo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | rufaa. Hali hiyo inasababisha kutoeleweka kwa namna ya kutumia fursa ya kukata rufaa. | | | |
| 26. | *The Environmental Management (Control of Ozone Depleting Substances and Hydrofluorocarbons) Regulations, 2022* | 1. **Jedwali la Nne** linalohusu Muundo wa Taarifa ya Nusu Mwaka, na limerejea kuanzishwa chini ya **Kanuni ya 20(2) na 21 (2)**.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kanuni ya 20(2)** inayorejewa haihusiani na Jedwali la Nne. Urejeaji wa kanuni isiyoendana kimaudhui unakiuka matakwa yaliyowekwa na Sheria ya Tafsiri ya Sheria (Sura ya kwanza) inayoelekeza kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kijitosheleze | 1. **Jedwali la Nne** lifanyiwe marekebisho kwa kurejea Kanuni sahihi inayolianzisha. | 1. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya marekebisho ya **Jedwali la Nne** imeandaliwa kwa kufuta Kanuni ya 20(2) na kurejea Kanuni sahihi ya 21(2) iliyotengeneza jedwali hilo.<br><br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki. | 1. Ikiwa Marekebisho yatakamilika, yataondoa changamoto ya ukiukwaji wa matakwa yaliyowekwa na kifungu cha 11 sheria ya Tafsiri ya sheria inayoelekeza kuwa sheria au kifungu kinachorejewa kijitosheleze kimadhumuni. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kimadhumuni.<br>Hali hii inaleta ugumu wa kueleweka kwa masharti ya kanuni na utekelezaji wa sheria mama.<br><br>2. **Kanuni ya 27 (b)** kinampa mamlaka Afisa Forodha kukagua na kutambua ikiwa mzigo ulioingizwa nchini una chembechembe za kikemikali zenye athari kwa Ozoni.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hazioneshi kwa namna gani Afisa Forodha ataweza kutambua uwepo wa kemikali hizo. | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuonesha namna ambavyo Afisa Forodha ataweza kutambua uwepo wa kemikali wakati wa ukaguzi wa mizigo inayoingizwa nchini. | 2. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya **Kanuni ya 27(b)** imeandaliwa kwa kuonesha kuwa afisa forodha atatambua bidhaa zenye Kemikali zenye athari kwa Tabaka la Ozone kwa kutumia kifaa maalum.<br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni | 2. Ikiwa marekebisho yatakamilika, yatasaidia kutambua kemikali zinazohusika kama ilivyokusudiwa na Kanuni hizi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 3. **Jedwali la kwanza** la linataja bidhaa zenye viwango fulani vya kemikali hatarishi kwa Ozoni na haidroflorokaboni.<br>**Tatizo**<br>Kipengele cha kwanza kinataja (Automobile and truck conditioning units) kikiacha neno Air kabla ya neno *Conditioning*.<br>Hali hii inaleta mkanganyiko wa kanuni katika kueleweka kwake. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho ili kuleta ukamilifu wa maudhui, Kipengele cha kwanza kinataja katika neno (Automobile and truck conditioning units) kwa kuongeza neno "*Air*" kabla ya neno "*Conditioning*" | imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki.<br>3. Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo, Rasimu ya Marekebisho ya Jedwali la Kwanza imeandaliwa kwa kuongeza Neno "*Air*" kabla ya Neno *Conditioning*.<br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki. | 3. Iwapo Marekebisho yatakamilika yataondoa mkanganyiko wa kueleweka kwa Kanuni. |
| 27. | *The Environmental Management* | 1. Kanuni inarejea kuanzishwa chini ya **Kifungu cha 75 na** | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta rejea ya | 1. Utekelzaji wa azimio la Bunge haujakamilika | 1. Kutokamilika kwa azimio la Bunge ni kuendeleza doasri ya |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | *(Control and Management Of Carbon Trading) Regulations, 2022* | **Kifungu namba 230(2)** cha Sheria Mama.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kifungu cha 230(2) na 75** vinavyorejewa kama vifungu wezeshi havihusiani na mamlaka ya Waziri kutunga Kanuni, badala yake vinahusu mambo mengine mangineyo ambayo Waziri atayatungia Kanuni na hatua za kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa. Katika uandishi wa Sheria Ndogo, rejea ya kifungu wezeshi inaonesha chimbuko la madaraka ya kutungwa kwa Sheria Ndogo hiyo. Changamoto ya kuweka rejea kifungu cha 75 ambayo | Kifungu cha 75 na 230 (2) na badala yake kurejea Kifungu cha 230(1). | **<u>Maelezo ya Wizara</u>**<br>Wizara imetoa maelezo kwamba, mchakato wa marekebisho ya kufuta rejea ya Kifungu cha 75 cha Sheria Mama kinachoanzisha Kanuni utafanyika. Aidha, Wizara imefafanua kwamba kutokutekelezwa kwa Azimio kunatokana na Kanuni hii kuwa na msukumo kitaifa na Kimataifa hivyo kupelekea kuitisha Mkutano wa Wadau kupata maoni ya wadau wengi, hali iliyosababisha | Sheria kurejea Kifungu wezeshi kisicho sahihi. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | haihusiani na mamlaka ya utungwaji wake inaweza kusababisha mashaka kuhusu uhalali wa Sheria Ndogo hiyo.<br><br>2. **Fomu C** katika Jedwali la Kwanza inahusu maombi ya biashara ya kaboni.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Imeweka viwango fedha za kimarekani kwa thamani ya milioni. Hali inayoashiria waombaji wote, kuwa watatakiwa kujaza viwango vya mradi vilivyo na thamani ya milioni, hivyo kutotambua waombaji ambao miradi yao haijafikia thamani hiyo. | 2. **Fomu C** ifanyiwe marekebisho kwa kufuta viwango vya dola vyenye thamani ya milioni vilivyoandikwa ndani ya fomu na badala yake ioneshe malipo yatakuwa kwa dola za marekani pasipo kuonesha thamani ya mradi. | kutokukamilika kwa marekebisho kwa wakati.<br><br>2. Utekelezaji wa azimio haujakamilika<br><br>**<u>Maelezo ya Wizara</u>**<br>Wizara imetoa maelezo kwamba, mchakato wa marekebisho ya Fomu C utafanyika kwa kufuta neno "*million*".<br>Wizara pia ilitoa maelezo mbelel ya Kamati kwamba, kutokutekelezwa kwa Azimio kunatokana na Kanuni hii kuwa na | 2. Kutokamilika kwa azimio la Bunge kunaendeleza mkanganyiko kuhusu thamani inayopaswa kujazwa waombaji wanaotaka kufanya biashara ya Kaboni. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | msukumo kitaifa na Kimataifa hivyo kupelekea kuitisha Mkutano wa Wadau kupata maoni ya wadau wengi, hali iliyosababisha kutokukamilika kwa marekebisho kwa wakati. | |
| | | 3. **Jedwali la Pili** linahusu viwango vya ada na gharama ya maombi ya kusajili wazo la mradi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Viwango vya ada ya maombi ya usajili inayopaswa kulipa na muombaji mzawa imewekwa kwa viwango vya dola za | 3. **Jedwali la Pili** lifanyiwe marekebisho kwa kubadilisha viwango vya ada ya maombi ya kusajili mradi kwa raia wa Tanzania kutoka dola za kimarekani na kuwa shilingi za kitanzania. | 3. Utekelezaji wa azimio la Bunge haujakamilika<br><br>**<u>Maelezo ya Wizara</u>**<br>Wizara imetoa maelezo kwamba, marekebisho yatafanyika katika Jedwali la Pili kwa kubadilisha viwango vya ada ya maombi ya kusajili mradi kwa | 3. Kutokamilika kwa azimio la Bunge ni kuendeleza kutokutabilika kwa viwango vya ada vinavyopaswa kulipwa na wazawa. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | marekani. | | raia wa Tanzania kutoka dola za kimarekani na kuwa shilingi za kitanzania. | |
| | | | **WIZARA YA FEDHA** | | |
| 28. | *The Foreign Exchange Regulation, 2022* | 1. **Kanuni ya 3** inahusu miamala ya fedha za kigeni, ambapo inazungumzia utaratibu wa kuuza na kununua fedha za kigeni kutoka katika benki, taasisi za fedha na maduka ya kubadilisha fedha.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni inaweka utaratibu wa aina mbili kuhusu namna ya kununua na kuuza fedha za kigeni katika benki, taasisi za kifedha na maduka ya kubadilisha fedha:- | 1. **Kanuni ya 3 (1) (b)** ifanyiwe marekebisho na kuongezwa maneno "*except an exporter*" baada ya maneno "*any person*" ili kuondoa mkanganyiko na kuleta uhusiano wa kimaana na sehemu nyingine za kanuni hii. | 1. Rasimu ya marekebisho ya **Kanuni ya 3** imeandaliwa kwa kufuta Kanuni ndogo ya **(7).** Marekebisho yapo katika hatua ya kuzingatiwa ambapo Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ili itangazwe katika Gazeti la Serikali. | 1. Ikiwa Marekebisho yatakamilika yataondoa mkanganyiko kuhusu utaratibu wa namna ya kununua na kuuza fedha za kigeni katika benki, taasisi za kifedha na maduka ya kubadilisha fedha. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | (i) **Kanuni ya 3(1) (b)** inampa mtu yeyote uhiari wa kuuza au kununua kiasi chochote cha fedha za kigeni kutoka kwenye benki, taasisi ya fedha au maduka ya kubadilisha fedha;<br><br>(ii) **Kanuni ya 3(7)** inaweka ulazima kwa msafirishaji wa bidhaa nje ya nchi, kuuza fedha za kigeni katika benki ambayo ana uhusiano wa kiakaunti.<br>Masharti yaliyowekwa katika **Kanuni ya 3(7)** yanakinzana na **Kifungu cha 4 (b)** cha Sheria | | | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
| --- | --- | --- | --- | --- | --- |
| | | Mama ambacho kinaweka uhiari wa kufungua akaunti ya benki ya fedha za kigeni.<br><br>2. **Kanuni ya 25(7)** inatoa adhabu ya malipo ya shilingi milioni moja kwa siku kutokana na kushindwa kuwasilisha nyaraka za mkopo kutoka nje ya nchi baada ya kuisha kipindi cha siku 14.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Adhabu iliyowekwa na Kanuni ya 25(7) haionekani kwa mujibu wa adhabu zinazowekwa na Sheria Mama. | 2. **Kanuni ya 25 (7)** ifanyiwe marekebisho ya adhabu iliyotajwa na kanuni hii ili kuendana na adhabu zilizoainishwa na sheria mama. | 2. Rasimu ya marekebisho ya **Kanuni ya 25** imeandaliwa kwa kufuta Kanuni ndogo **(7).**<br><br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ili itangazwe katika Gazeti la Serikali. | 2. Ikiwa Marekebisho yatakamilika yataondoa ukinzani wa Kanuni na Sheria Mama, ambao ulikuwa ni kinyume na masharti ya Kifungu cha 36 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 3. **Kanuni ya 26** inaweka utaratibu wa namna ya kusajili mikopo kutoka nje ya nchi. Ambapo pia imeweka vigezo vitakavyozingatiwa ili kuisajili au kutoisajili mikopo hiyo.<br><br>**Aidha, Kanuni ya 26** imeandikwa kwa mpangilio unaoanza kwa kutaja vigezo vitakavyozingatiwa wakati wa kusajili mkopo kutoka nje ya nchi. Ikifuatiwa na maelezo ya jumla ambayo yanaweka katazo kwa benki kutokusajili mikopo ambayo haijakidhi masharti yaliyotajwa na **Kanuni 26 (1) (2).** | 3. **Kanuni ya 26 (3)** ifanyiwe marekebisho kwa:<br>(i) kuondoa utashi wa kuongeza vigezo vingine vitakavyozingatiwa wakati wa kusajili wa mikopo ya nje na kuitaka mamlaka inayohusika kutangaza vingezo vingine vilivyotumika katika kukataa usajili wa mikopo ya nje kwenye gazeti; na<br><br>(ii) kuwekwa katika mpangilio unaoanza na kanuni ndogo ya tatu, ikifuatiwa na kanuni ndogo ya | 3. Rasimu ya marekebisho imeandaliwa kwa kufuta **Kanuni ya 26** na kuiandika upya ili kuondoa sharti la utashi wa kuongeza vigezo vya ziada vitakavyozingatiwa wakati wa kusajili wa mikopo ya nje na vilevile kuweka mpangilio mpya wa Kanuni<br><br>Rasimu ya Marekebisho ya Kanuni imewasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki ili itangazwe katika Gazeti la Serikali. | 3. Ikiwa Marekebisho yatakamilika yataondoa changamoto ya kutotabirika kwa vigezo vya kusajili mikopo ya nje hali inayoweza kusababisha mkwamo katika usajili wa mikopo ya nje. Aidha, marekebisho haya yataondoa changamoto ya kiuandishi hivyo kurahisisha usomaji mzuri wa Kanuni. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Kanuni imetoa utashi wa kuongeza vigezo vingine vitavyozingatiwa wakati wa kusajili mkopo pasipo kuviainisha.<br><br>**<u>Tatizo la pili</u>**<br>Kanuni hiyo haijaandikwa kwa mpangilio. Hali inayoweza kuleta changamoto katika usomaji wake. | kwanza na ya pili | | |
| 29. | *The Banking and Financial Institutions (Mortgage Refinance Companies) Regulations, 2022* | 1. **Kanuni ya 6(3) (b)** inaweka kiwango cha ada ya usajili ya shilingi milioni tano au kiwango kingine kitakachoamuliwa na Benki Kuu, kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya *mortgage re –financing*. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mwanya wa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. | 1. Marekebisho **Kanuni ya 6(3)** yamefanyika kwa kufuta utashi Benki Kuu kuongeza ada ya usajili pale itakapoona inafaa. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la** | 1. Marekebisho haya yanaondoa hali ya kutokutabirika kwa ada halisi za usajili kwa mtu anayetaka kuanza biashara ya *Mortgage re- finance*. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imetoa mwanya kwa Benki Kuu kutoza ada ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua. Kiasi hicho kilichotajwa hakifafanui ukomo wa chini wala wa juu.<br>Hali hiyo inaweza kusababisha kutoeleweka kwa ada halisi ya usajili, uwezekano wa kuwepo wa viwango mbalimbali vya ada ya usajili na kuleta mkanganyiko kwa watekelezaji wa kanuni hizi. | | **Serikali (TS Na. 456 la tarehe 14, Julai, 2023).** | |
| | | 2. **Kanuni ya 10(1) (2)** inaweka vigezo na uzoefu wa Wajumbe watakaopendekezwa kuwa katika Bodi ya | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka utaratibu wa kikanuni utakaofuatwa baada | 2. Marekebisho **Kanuni ya 10** yamefanyika kwa kuongeza Kanuni ndogo ya (3) inayoanzisha | 2. Marekebisho yaliyofanywa yanaweka bayana utaratibu wa Benki Kuu kuelekeza MRC |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wakurugenzi.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni haioneshi endapo hatua itakayochukuliwa na Benki Kuu ikiwa Mjumbe aliyependekezwa atakosa sifa zilizotajwa kwa mujibu wa Kanuni. | ya Benki Kuu kutoridhishwa na sifa za mjumbe/ wajumbe watakaopendekezwa na kampuni kuwa sehemu ya Bodi ya Wakurugenzi. | utaratibu wa Benki Kuu kuelekeza MRC kupendekeza Mjumbe wa Bodi mwingine pale inapotokea aliyependekezwa awali hajakidhi vigezo. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 456 la tarehe 14, Julai, 2023).** | kupendekeza Mjumbe wa Bodi mwingine pale inapotokea aliyependekezwa awali hajakidhi vigezo. |
| | | 3. **Kanuni ya 31** inaonesha uwezo wa Benki kuu kutoa adhabu mbalimbali inapotokea masharti ya Kanuni hizi yamevunjwa. Masharti hayo yametajwa katika aya ya (c), (d), (e), (f) na (g) ambayo ni | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa zuio la muda pamoja na mazingira yatakayopelekea kusitishwa na adhabu. | 3. Marekebisho **Kanuni ya 31** yamefanyika kwa kuongeza kanuni ndogo (2) inayoweka mazingira ambayo wahusika au kampuni iliyositishiwa leseni | 3. Marekebisho yaliyofanyika yanaakisi lengo lililokusudiwa kuhusu zuio la muda. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuzuiwa kwa muda kupata huduma za mikopo kutoka Benki Kuu, (*Suspension of capital expenditure)*, fursa ya kutoa mikopo na kuzuia kwa muda mkurugenzi, afisa au mwajiriwa aliyekiuka masharti ya kanuni hizi asitekeleze majukumu yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni hazioneshi ukomo wa muda wa zuio na wala hazioneshi mazingira yanayoweza kuruhusu wahusika au kampuni kuendelea na majukumu au kazi ikiwa marekebisho au maboresho yatafanyika kuondoa kasoro | | kwa muda kuendelea na majukumu au shughuli zao, ikiwa watafanya marekebisho au maboresho yakuondoa kasoro zilizosababisha kuzuiwa leseni zao kwa muda. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 456 la tarehe 14, Julai, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | zilizosababisha kuwekwa kwa zuio la muda.<br>Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kwa kampuni au wahusika waliosahihisha kasoro au dosari hizo.<br><br>4. **Jedwali la Tatu** linataja sifa na uzoefu za Wajumbe wanotakiwa kuwa katika Bodi ya Wakurugenzi.<br><br>**<u>Tatizo la kwanza</u>**<br>Kipengele cha 1 (b) kinataja sifa mojawapo kuwa wasifu wa jumla wa mjumbe au Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi bila kuhusisha taaluma ya wajumbe hao. | 4. **Jedwali la Tatu** lifanyiwe marekebisho katika: -<br>(i) kipengele cha 1 (b) kwa kuonesha kuwa wasifu wa mjumbe utakaozingatiwa na Benki Kuu utakua ni ule uliotokana na taaluma ya mjumbe huyo; na<br><br>(ii) Jedwali la tatu la | 4. Marekebisho **Jedwali la** Tatu yamefanyika kwa kufuta **aya ya 1(b)** iliyokuwa inahusu sifa ya wasifu wa jumla wa Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.<br>Vilevile aya ya 3 imefutwa ili kuondoa Mamlaka ya Benki kuu kuongeza vigezo vingine vyovyote | 4. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa mkanganyiko kuhusu wasifu wa mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na kuondoa uwezekano wa kuongeza vigezo pale wanapojisikia kufanya hivyo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Hali hii inaweza kuleta mkanganyiko wakati wa utekelezaji hususan katika upimaji wa wasifu wa jumla wa mjumbe au wajumbe waliopendekezwa.<br><br>**<u>Tatizo la Pili</u>**<br>Kipengele cha Tatu cha Jedwali kinaipa mamlaka Benki Kuu kuweka vigezo vingine vyovyote itakavyoona inafaa.<br>Hali hii inaweza kusababisha kutokufahamika bayana kwa vigezo vinavyohusika, hivyo kuleta mkanganyiko miongoni mwa walengwa. | Kanuni lifanyiwe marekebisho kwa kwa kuondoa kipengele cha tatu kinachoipa Mamlaka Benki kuu kuongeza vigezo vingine vyovyote itakavyoona vinafaa. | itakavyoona vinafaa.<br>Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 456 la tarehe 14, Julai, 2023).** | |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| 30. | *The Banking and Financial Institutions (Financial Leasing) Regulations, 2022* | 1. **Kanuni ya 51(c), (d), (e) na (g)** inaonesha uwezo wa Benki kuu kutoa adhabu mbalimbali inapotokea masharti ya Kanuni hizi yamevunjwa. Masharti hayo yametajwa katika aya ya (c), (d), (e), na (g) ambayo ni kuzuiwa kwa muda kupata huduma za mikopo kutoka Benki Kuu, (*Suspension of capital expenditure)*, fursa ya kutoa mikopo na kuzuia kwa muda mkurugenzi, afisa au mwajiriwa aliyekiuka masharti ya kanuni hizi asitekeleze majukumu yaliyoainishwa chini ya Kanuni hizi. | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka ukomo wa zuio la muda pamoja na mazingira yatakayopelekea kusitishwa na adhabu. | 1. Marekebisho **Kanuni ya 51** yamefanyika kwa kuongeza kanuni ndogo (2) inayoweka mazingira ambayo wahusika au kampuni iliyositishiwa leseni kwa muda kuendelea na majukumu au shughuli zao, ikiwa watafanya marekebisho au maboresho yakuondoa kasoro zilizosababisha kuzuiwa leseni zao kwa muda. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 456 la tarehe 11, Agosti,** | 1. Marekebisho haya yana akisi lengo lililokusudiwa na sheria kuhusu zuio la muda. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni hazioneshi ukomo wa muda wa zuio na wala hazioneshi mazingira yanayoweza kuruhusu wahusika au kampuni kuendelea na majukumu au kazi ikiwa marekebisho au maboresho yatafanyika kuondoa kasoro zilizosababisha kuwekwa kwa zuio la muda.<br>Hali hiyo inaweza kutatiza uzingatiaji wa misingi ya haki kwa kampuni au wahusika waliosahihisha kasoro au dosari hizo. | | **2023).** | |
| | | 2. **Kanuni ya 9** ya Kanuni hizi, inazungumzia ada ya maombi ya leseni yanayotakiwa | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuondoa mwanya wa Benki Kuu kutoza ada | 2. Marekebisho **Kanuni ya 9** yamefanyika kwa kufuta utashi Benki Kuu kuongeza | 2. Marekebisho yaliyofanyika yanaondoa hali ya kutokutabirika kwa |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kuambatana na hundi ya shilingi milioni tano au kiasi chochote kitachoamuliwa na Benki.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>Kanuni imeipa mamlaka Benki kuongeza kiasi chochote mbali na kiwango cha chini cha shilingi milioni tano kilichotajwa.<br>Mamlaka hayo ya matumizi ya utashi kwa Benki yanaondoa mantiki nzima ya uwepo wa kiwango cha chini cha shilingi milioni tano kama ada ya maombi ya leseni.<br>Hali hiyo itapelekea ugumu katika utekelezaji wa takwa hili la kisheria lakini pia ni | ya usajili inayoweza kuzidi au kupungua | ada ya usajili pale itakapoona inafaa. Marekebisho yametangazwa kwenye **Gazeti la Serikali (TS Na. 456 la tarehe 11, Agosti, 2023).** | ada halisi za usajili kwa mtu anayetaka kufanya biashara ya utoaji mikopo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | kinyume na kanuni za uandishi kama ambavyo zimeelekezwa ndani ya Sheria ya Tafsiri za Sheria (Cap 1) ya Tanzania. | | | |
| **WIZARA YA MADINI** | | | | | |
| 31. | *The Mining (State Participation) Regulations, 2022* | 1. **Kanuni ya 6(2)** inamtaka mtu yeyote mwenye leseni ya kuchimba madini kutoa notisi ya siku tisini tangu tarehe ya kutangazwa kwa Kanuni hizi ili Tume ya Madini ianzishe mchakato wa makubaliano ya ushirikiano kuiwezesha serikali kuwa na hisa.<br><br>**Tatizo**<br>Kanuni haioneshi adhabu kwa kushindwa kutoa notisi kwa wakati | 1. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza kifungu kitakachoonesha adhabu kwa kosa la kushindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kikanuni ili kuipa nguvu kanuni hiyo. | 1. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 1. Kutokutekelezwa kwa azimio la Bunge ni kuendeleza dosari ya Kanuni hizi kutoonesha adhabu kwa mtu aliyeshindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kikanuni. Dosari inayoweza kuwa na mtazamo wa kuinyima nguvu kanuni hivyo, kusababisha isiwe na maana yoyote katika kusimamia ushiriki wa Serikali katika sekta |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | uliowekwa kikanuni. Kutokubainishwa kwa adhabu ya kushindwa kutoa notisi kwa wakati uliowekwa kunainyima nguvu kanuni hiyo na kusababisha isiwe na maana yoyote katika kusimamia ushiriki wa Serikali. | | | ya madini. |
| | | 2. Kanuni imerejea kuanzishwa chini ya Kifungu cha 10(4) na kifungu cha 129 cha Sheria Mama.<br><br>**<u>Tatizo</u>**<br>**Kifungu cha 10(4)** kinachorejewa kuanzisha Kanuni hizi hakipo katika Sheria Mama.<br>Hali hii inaweza kuleta mashaka juu ya uhalali | 2. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kufuta kifungu cha 10 (4) kilichorejewa na kanuni hizi kama kifungu wezeshi. Kufutwa kwa kifungu hiki kutaondoa mashaka yatakayoibuka juu ya uhalali wa kanuni hizi. | 2. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 2. Kwa kutokutekeleza azimio la Bunge ni dhahiri kwamba, dosari ya kurejea Kifungu kinachoianzisha ambacho si sahihi inaendelea kuwepo. |

| Na | Sheria Ndogo | Yatokanayo na Uchambuzi | Azimio la Bunge | Hatua Iliyofikiwa | Maoni ya Kamati |
|---|---|---|---|---|---|
| | | wa kanuni hizi.<br><br>3. **Kanuni** hazijaweka vifungu vya makosa na vifungu vya adhabu, vilevile haibainishi sheria au kanuni inayoweza kutumika iwapo masharti ya kanuni hizi yatakiukwa.<br>Hali hii inasababisha kanuni hizi kukosa msukumo kwa watumiaji kutekeleza masharti yaliyowekwa na kanuni hizi.<br>Aidha kwa namna zilivyo kanuni hizi zinaweza<br>kutatiza usimamizi wa masharti sahihi yaliyowekwa. | 3. Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuweka vifungu vinavyoonesha makosa na adhabu zitakazotolewa baada ya makosa hayo kufanyika ili kuongeza msukumo kwa watumiaji kutekeleza masharti yaliyowekwa na kanuni hizi. | 3. Azimio la Bunge halijatekelezwa | 3. Kutokufikia hatua ya utekelezaji wa azimio la Bunge kunasababisha sheria ndogo kuendelea kuwa na dosari ambayo inachochea kutowapa msukumo watumiaji kutekeleza masharti yaliyowekwa chini ya kanuni hizi. |

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante Mwenyekiti kwa kusoma vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuna wachangiaji na tunaanza na Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, wajiandae Mheshimiwa Mpina, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka, Balozi Liberata, Mheshimiwa Aida Joseph Khenani na Mheshimiwa Mariam Omar Said.

**MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuwa mchangiaji wa mwanzo kabisa katika jambo hili la Kamati hii ya Kudumu ya Sheria Ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Allah Subhana Wa ta'ala muumba mbingu na ardhi, akatuwezesha sisi kuwa Wabunge mahiri tunaofanya kazi zetu kwa umakini sana. Lakini pia nitumie fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri sana anayoifanya. Amefika kila eneo, kila jimbo, kila kata kupeleka maendeleo. Tunamshukuru sana, tunampongeza sana, tunampa moyo sana, ili aendelee kufanya kazi hii adhimu ya Taifa hili, kazi ya uzalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashukuru pia kuwemo kwenye Kamati hii, Kamati ya Kudumu ya Sheria Ndogo. Katika vipengele ambavyo vimetajwa leo hapo na Mwenyekiti wakati akiwasilisha mada yake ni kutokutekelezwa kwa Maazimio ya Bunge. Sisi hapa tumekaa tunapitisha maazimio leo. Mfano leo, tumeshasoma na tutapitisha maazimio, kama yalivyoelekezwa katika uwasilishaji wake, na Bunge linaazimia kwamba, jambo hili lirekebishwe, litengenezwe, halafu anatokea mtu hafanyi hilo jambo kwa hiyo, hatekelezi Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi siamini kwamba kuna mtu ana nguvu hiyo, lakini labda huwa nafikiri labda amesahau au hakusikia au sijui niseme neno gani zuri. Maana maazimio

tunayatoa kwa pamoja tunakuwepo humu Bungeni, watu wanasikia, wafau wenzetu wanasheria wanayachukua wanakubaliana na sisi, miezi inapita, mitatu, minne, mpaka miezi sita hajatekeleza, lengo lake huwa ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, labda wanafikiria kwamba Kamati hii ya Sheria Ndogo labda si Kamati ya kisekta, mimi huwa nafikiria vitu kama hivyo, labda si Kamati ya kisekta kwa hiyo, hawajibiki sana hivi, hana wajibu wa kuwajibika wa kutekeleza Maazimio ya Bunge kwa sababu ni watu wa sheria ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ifahamike kwamba, Kamati ya Sheria Ndogo ni sawa na kamati nyingine yoyote ya Bunge na tunaliwakilisha Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, siamini na wala sitaki kuamini kwamba kuna mtu anatubeza kiasi hicho. Sasa, kama yupo tunamuomba aache hilo jambo, aache kabisa, kwa sababu hizi tunazozitengeneza ni sheria na tunazitengeneza kwa ajili ya wananchi wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, utawala bora ni utawala wa sheria. Maana yake ni kwamba, kama sheria ni mbovu, zimerekebishwa na wewe hautaki, maana yake ni kwamba unabomoa utawala wa sheria ambao ndio utawala bora, kazi ambayo itakuwa inatukwaza, si jambo zuri. Na bahati nzuri sana ni kwamba, hizi sheria tayari ziko mtaani na zinawaumiza watu, ni wananchi wenzetu na sisi ni miongoni mwa wananchi. Kwa hiyo tunawaomba wale wanaohusika, wale wadau wenzetu wa sheria wanaohusika na kurekebisha warekebishe. Si vizuri mpaka Bunge lingine linakuja maazimio ya Bunge hayajatekelezwa, si jambo zuri. Lakini mimi ninaamini labda watu wanafanya hivyo kwa sababu ya yale madaraka yao, labda wale wanataka kuyalinda yale madaraka, kwamba hiyo sheria ikibadilishwa inamfanya madaraka yake yapotee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi naomba tena kwa heshima na taadhima wale wanaohusika na kutekeleza Maazimio ya Bunge baada ya Bunge kupitisha maazimio hayo wayatekeleze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno hayo naunga mkono hoja na ninakushukuru kwa nafasi; ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mpina, jiandae Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa ili na mimi niweze kuchangia hii Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kama ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti na ni-*declare* kabisa mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ya utungaji wa sheria ndogo kama ambavyo Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati imezungumza na jinsi alivyobainisha, changamoto ya utungaji wa sheria ndogo katika Halmashauri; changamoto ya kwanza, zinatungwa sheria ambazo zinatofautiana, kwa mfano, viwango vya tozo na ushuru vinatofautiana kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya sekta kama za mifugo, uvuvi, kilimo, zinatofautiana na kusababisha malalamiko makubwa kwa wananchi wanapoona kwamba wenzao wanatozwa kidogo na wao wanatozwa pakubwa. Kwa mfano katika katika uvuvi, ushuru wa samaki, maeneo mengine wanatoza ushuru wa shilingi 100 kwa kilo sehemu nyingine wanatoza shilingi 300 kwa kilo. Suala hili limekuwa likileta usumbufu mkubwa sana na kuwasababishia wananchi manung'uniko kila sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la pili ni kuwepo kwa utitiri wa sheria ndogo nyingi mno. Kutokana na kuruhusiwa kila Halmashauri moja inatunga sheria zake, kila kijiji kimeruhusiwa kutunga sheria zake, kila manispaa imeruhusiwa kutunga sheria zake, matokeo yake tumekuwa na sheria nyingi kiasi kwamba tumeshindwa hata kuzisimamia. Tumekuwa na sheria ndogo nyingi mno kiasi kwamba hatuwezi kuzisimamia sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwa mujibu wa Taarifa ya *Auda's Index* pamoja na Taarifa ya *JUTA Index of Subsidiary Legislations* inaonesha kwamba tangu mwaka 1920 tumeshatunga sheria ndogo 41,051 ambapo sheria ndogo zinazofanya kazi mpaka sasa hivi ni 25,000, na kila mwaka tunatunga sheria ndogo zaidi ya 500. Sasa ukishakuwa na sheria ndogo nyingi namna hii huwezi tena kuzisimamia na zitaendelea kuleta madhara tu kwa wananchi kwa sababu haziwezi kuwa kwenye *scope* nzuri ya usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la tatu kwenye Halmashauri ni kuwepo kwa upungufu mkubwa wa wataalam, jambo ambalo linasababisha sasa zinatungwa sheria ambazo zina mapungufu makubwa, zinatungwa sheria ambazo zinaweka adhabu na faini kubwa kuliko hata zile zilizoko kwenye sheria mama, zinatungwa sheria ambazo zina masharti na makatazo ambayo ni kinyume na sera, makatazo ambayo ni kinyume na Katiba ya nchi yetu, zinatungwa sheria ambazo zinapeleka dhuluma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukishakuwa na utaratibu huu wa utungaji wa sheria unatuletea madhara makubwa sana katika Serikali yetu na malalamiko makubwa sana ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa napendekeza kufanyike nini; kwa nini tusiachane na huu utaratibu wa kila halmashauri inatunga sheria yake, kila kijiji kinatunga sheria zake, kila halmashauri ya mji inatunga sheria yake, kila manispaa tukawa na sheria moja tu kwamba halmashauri zote ziongozwe na sheria ndogo itakayotungwa na Waziri na itumike kwa halmashauri zote, yaani *uniform by-laws,* kwa kuzingatia makundi yote manne ya halmashauri ambayo ni mamlaka za mji, mamlaka za wilaya, mamlaka za miji midogo, mamlaka za halmshauri za vijiji, tunaweza tukafanya hivyo na tukafanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa bahati nzuri sheria inaturuhusu, Sheria ya Serikali za Mitaa, Sura 287 na Sura 288 zinampa Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kutunga kanuni ndogo ambazo zitakuwa ni *uniform* kwa maeneo yote ambayo niliyoyataja na kwa kufanya hivyo ni rahisi

tu kwa sababu itatulazimisha kufanya *amendment* kwenye vifungu vya sheria hiyo ya Serikali za Mitaa, Sura ya 287 na Sura ya 288 katika vifungu vinavyozipa mamlaka hizo, Mamlaka za Miji, Mamlaka za Wilaya, Mamlaka za Miji Midogo na Mamlaka za Halmashauri za Vijiji kuziondolea yale mamlaka zilizopewa kwa mujibu wa sheria, kutunga sheria na badala yake akatunga tu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kutungwa kwa sheria ndogo nyingi zenye dosari, lakini zinaanza kutumika kabla hazijahakikiwa na Bunge, kabla Bunge halijafanya sehemu yake ya *oversight function* tayari hizi sheria zinaenda kutumika. Madhara yake ni nini zinapoenda kutumika?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyekiti wa Kamati amezungumza na mimi ninazungumza kwamba moja, wananchi wanaadhibiwa kwa makosa ambayo si yao. Sheria imetungwa na Serikali, inaenda kutekelezwa ikiwa na dosari, wananchi wanaonewa kwa mambo ambayo ni kinyume cha sera ya nchi, kwa mambo ambayo ni kinyume na sheria za nchi, kwa mambo ambayo ni kinyume na Katiba ya nchi, lakini yameruhusiwa. Imeenda kutungwa kule sheria na kwenda kuleta madhara makubwa sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa bahati mbaya hata inapokuja kutokea kwamba sheria ile ilikosewa, kinachofanyika ni sheria ndogo tu inarekebishwa, halafu madhara waliyoyapata wananchi hakuna anayefidia; mtu aliyesababisha kuingia kwenye matatizo hayo hawajibiki na wala hachukuliwi hatua yoyote. Jambo hili limekuwa likituletea matatizo makubwa sana, lakini pia ni kinyume pia hata ya Ibara ya 8(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo inazungumzia ustawi wa watu.

Kwa hiyo, Serikali na Bunge haziwezi kuruhusu mambo yanayokinzana na ustawi wa nchi yanaenda kutungwa na kwenda kwa wananchi wakati yanakatazwa kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tatu katika hili eneo ni Bunge kunyang'anywa mamlaka yake; kwa mujibu wa Katiba,

Ibara ya 97(5) ambayo imetupa mamlaka ya kukasimu utungaji wa hizi sheria ndogo, umekuwa ukivunjwa mno sasa hivi na mamlaka tulizozikasimiwa kufanya hilo jukumu. Sasa kama zinavunjwa na wananchi wanaenda kutengenezewa mgogoro mkubwa na matatizo makubwa ni lazima kama Bunge hili tuone kwamba tusikubali tena mamlaka yetu hayo yakatumika vibaya. Wananchi wanajua Katiba imelipa mamlaka Bunge la Jamhuri ya Muungano kutunga sheria na hivyo mtu yeyote atakayetunga sheria ya aina yoyote ikaenda kutumika kwa wananchi, moja kwa moja limetunga Bunge. Sasa Bunge hili lijitoe katika hilo, lisikubali tena hizi sheria ndogo kutungwa na kuanza kutumika bila kufanyiwa uhakiki kwanza na Bunge hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu, kuchelewa kufanyiwa marekebisho ya dosari; hata dosari hizo tunapozibaini tunakuja hapa tunaagiza zikafanyiwe marekebisho, zimekuwa zikichelewa mno na wananchi wanaendelea kupata matatizo makubwa katika kanuni hizo. Marekebisho hayafanywi, kwa mfano, tulifanya maamuzi katika kipindi cha Februari, 2023 ambapo mpaka sasa hivi dosari 19 katika kanuni 10 bado hazijafanyiwa marekebisho na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kutoka katika jambo hili, nashauri kwamba tuziondoe changamoto nilizozitaja (a), (b) na (c); sasa napendekeza kila sheria ndogo inapotungwa na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, isitumike kwanza hadi hapo Bunge hili litakapokuwa limefanya uhakiki wa sheria hizo na Bunge hili litafanya uhakiki wa sheria hizo kupitia Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ninalotaka kuzungumza, Mwenyekiti wa Kamati amempongeza Mwanasheria Mkuu wa Serikali nami nampongeza na jambo moja ninalompongeza, hata ukimpigia simu saa saba za usiku anapokea na anakujibu. *(Makofi)*

Sasa suala la kujiuliza ni kwa nini Sheria Ndogo hizi zinatungwa, zinafanyiwa *vetting* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, lakini zinaendelea kuwa na dosari kiasi hiki? Tatizo ni nini katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Tatizo ni sheria

hizi zimekuwa nyingi wameshindwa kuzi-*manage?* Tatizo ni kwamba kuna upungufu wa fedha au wana upungufu wa watumishi au ni nini katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali? Mwanasheria Mkuu wa Serikali lazima atuambie ukweli juu ya jambo hili ili nchi hii isiendelee kupata matatizo inayoyapata hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu isikubali haya mambo yakaendelea kutokea na wananchi wetu wakaendelea kupata madhara makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba Bunge hili sasa lisiruhusu hizi kasoro ziendelee kutokea, wananchi wetu wakaendelea kutozwa tozo kubwa kuliko uhalisia, wananchi wetu wakaendelea kutozwa faini kubwa kuliko uhalisia, wananchi wetu wakaendelea kufukuzwa kwenye makazi yao bila sababu za msingi, wananchi wetu wakaendelea kutaifishiwa mifugo yao kinyume cha sheria na sera za nchi, wananchi wetu wakaendelea kutozwa kodi kubwa na tozo kubwa za maji, simu na mambo mengine kama umeme, unashtukia tu ghafla tozo na ushuru wa umeme umepandishwa na wananchi wanalazimishwa kulipa.

Mheshimiwa, Naibu Spika, haya yote yanafanyika kwa sababu ya Bunge hili kukasimu madaraka ya utungaji wa Sheria Ndogo kama Ibara ya 97(5) inavyosema, lakini eneo hili linatumika vibaya.

Sasa kupitia Bunge hili leo tukatae hayo kwa kuhakikisha kwamba hizo Sheria Ndogo ambazo zinatumika kama uchochoro wa kufanya dhuluma, wa kufanya uonevu kwa wananchi wetu kwa kisingizio cha kutunga Sheria Ndogo, sasa tukatae rasmi kupitia uchochoro huu kwa kukataza hizo sheria zote kupitia kule na matokeo yake ziletwe kwenye Kamati zetu ili tuzifanyie uhakiki kabla hazijenda kuumiza wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa na leo nashukuru nimemaliza yale niliyoandaa kusema. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, ajiandae Mheshimiwa Maryam Omar Said.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji leo hii. Awali ya yote natumia fursa hii kumshukuru sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Rais wa Zanzibar, kwa kazi kubwa wanazozifanya katika kuwatumikia wananchi wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba, miongoni mwa majukumu mama na ya msingi ya Kamati ya Sheria Ndogo, ni kufanya uchambuzi wa Sheria Ndogo zinazowasilishwa Bungeni pamoja na kuangalia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge. Miezi michache iliyopita nyuma, Bunge hili tukufu liliazimia jumla ya dosari 83 ziende zikarekebishwe kutokana na athari zinazowakuta wananchi. Wakati Kamati ya Sheria Ndogo ilipofanya mapitio ya utekelezaji wa maazimio yale, imebaini kwamba kumekuwa na dosari 19 ambazo zimeshindwa kurekebishwa licha ya kuwa baadhi ya Wizara husika tayari walikuwa wameshatangaza marekebisho yao katika Gazeti la Serikali. Ukiangalia ndani, dosari zile hawakuzirekebisha kama ilivyoazimiwa na Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni sawa na kusema kwamba, 22.89% ya Maazimio ya Bunge yaliyotolewa toka tarehe 8 Februari, 2023 hadi kufika tarehe 14 Agosti, 2023, wakati Kamati ya Sheria Ndogo ilipokutana katika vikao vyake vya kupokea taarifa ya utekelezaji, maazimio hayo hayakuwa yametekelezeka. Miongoni mwa Wizara ambazo tulibaini zimeshindwa kutekeleza maazimio hayo kwa kiwango ambacho Bunge liliazimia, ni Wizara ya TAMISEMI. Tulikuja kubaini walikuwa na dosari 16 ambazo wameshindwa kuzitekeleza. Wizara ya Madini na wao walikuwa na dosari tatu ambazo zimeshindwa kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inatupa picha gani? Jambo hili la kushindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge inatoa taswira kwa wananchi kwamba, Wizara hizi zimeshindwa kutii maagizo ya Bunge au zimeshindwa kutekeleza kwa sababu ya kuona kwamba Bunge hili halina nguvu na mamlaka ya kuwalazimisha wao kutekeleza jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kitendo ambacho hakiwezi kuvumilika, kuacha kutumika kwa dosari hizi katika mazingira ya kawaida, kwa sababu kuendelea kutumika kwa dosari hizi ni sawa na kuyakumbatia madhara yanayotokana na dosari ya sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano wa dosari ambazo Bunge liliazimia ziende zikarekebishwe lakini hazikuweza kurekebishwa. Unaposoma Sheria ya Usafi wa Mazingira ya Wilaya ya Misungwi ya mwaka 2023, Ibara ya 22(2), Kifungu hiki kimekuwa na mkanganyiko mkubwa sana wa adhabu, unapoenda kusoma kifungu cha 36(1). Kifungu cha 22(2) kinatoa adhabu ya jumla kwa mtu yeyote yule atakayekiuka masharti yoyote ya Kifungu cha Sheria. Kinatoa adhabu ya kupigwa faini isiyozidi shilingi 200,000 au kifungo kisichozidi miezi 12. Mkanganyiko unatokea utakapoenda kusoma Ibara ya 36(1) ya Kanuni hii ambapo hicho kipengele kinasema; "Mtu yeyote atakayefanya kosa lolote katika sheria hii, atapigwa faini isiyopungua shilingi 200,000 au kifungo kisichopungua miezi sita."

Mheshimiwa Naibu Spika, huu ni mkanganyiko katika utekelezaji wa adhabu unaotokana na sheria. Kwa sababu, wakati ambapo wananchi wanaenda kuadhibiwa kwa sheria hii, changamoto itakayotokea ni kipengele gani cha sheria kifuatwe. Aidha, 36(1) au 22(2). Huu ni mkanganyiko usiokuwa wa lazima na mkanganyiko huu unaendelea kuwepo na kuwaathiri wananchi, kwa sababu tu ya mamlaka inayohusika kushindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge, kwa sababu, Bunge tayari walishawaelekeza waende wakaondoe dosari hizi lakini hawakufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili ndiyo chombo cha uwakilishi wa wananchi, haliwezi na halitoweza kuacha mamlaka yake ya kutengeneza sheria, yatumike kwa namna itakayoweza kuwakanganya wananchi katika kutekeleza majukumu yao. Dosari yoyote inayotokana na athari ya kushindwa kutekeleza au kushindwa kutekeleza kwa muda Maazimio ya Bunge, haikubaliki kuachwa kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili ndiyo chombo cha wananchi, lakini pia ndiyo sauti ya wananchi. Ikiwa kama ndiyo sauti ya wananchi, Bunge haliwezi kukaa kimya kwa zile dosari

ambazo zinaendelea kuwaumiza wananchi wetu. Ndiyo maana Bunge hili lilitoa maazimio ya kwamba, dosari hizi 19 ziondoshwe ili zisiendelee kuleta madhara kwa wananchi. Kusema ukweli hakuna hata kimoja kilichofanyika, kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni uoni wa Kamati kwamba, Bunge hili litazuia utumikaji wa dosari hizi 19, zilizokuwemo katika Sheria Ndogo kumi ili zisiendelee kutumika kwa wananchi, kwa sababu, kama Bunge hili litaachilia kuendelea kutumika kwa dosari hizi, ni sawa na Bunge hili kuridhia kuendelea kukumbatia athari zinazowapata wananchi zinazotokana na Sheria hizi Ndogo. Vile vile, itatafsirika ya kwamba Bunge hili limekubali mamlaka yake iliyokasimu kwa mamlaka nyingine zakutunga sheria, zitumike kinyume na utaratibu unaokusudiwa ambao ndiyo dhamira halisi ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo chochote kinachotokana na madhara yanayotokana na dosari hizi ambazo Bunge limedhamiria ziondoshwe, hakitavumiliwa na hazitaachwa kuendelea kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema kitu kimoja kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla, si udhaifu katika maisha kukubali kukosolewa, kuambiwa na kuelekezwa kwa maslahi ya wengi au wachache, ikiwa jambo lina maslahi kwa Taifa hili. Ni kweli kabisa makosa tunayo katika kuelekezana. Wengine wakali, wabishi na wengine wagumu kuelewa. Kibaya zaidi, wapo miongoni mwetu. Kupata mawazo yao, fikra zao, akili zao pamoja na elimu yao, zionekane hakuna wa kuzipinga kutokana na jinsi wao walivyoelimishwa. Kitendo cha kuwakosoa au kuwaelekeza, kwao wao ni sawa na udhaifu ambao Mungu kawajalia na hawakustahiki kuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge ndicho chombo chenye mamlaka ya kusimamia utungaji wa sheria zote za nchi hii. Kitendo cha kukasimu mamlaka yake kwa Wizara nyingine, haimaanishi kwamba Bunge halikuwa na uwezo wa kutengeneza sheria hizo, lakini limetekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya kukasimu madaraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu, leo hii ni vizuri tukaazimia na kuzitaka Wizara ambazo zimeshindwa kutekeleza Maazimio ya Bunge hili tukufu, zirekebishe kasoro hizo mara moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Maryam Omar, ajiandae Mheshimiwa Aida Joseph Khenani.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi leo nikawa mchangiaji katika Taarifa hii ya Kamati yangu ya Sheria Ndogo.

Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kunijalia nikapata pumzi hii ya kusimama hapa leo. Nisiende mbali sana kwa wingi wa shukrani hizo, naenda moja kwa moja, nijielekeze katika mchango wangu niliokusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tumesikia hapa wakati Mwenyekiti wa Kamati anatuwasilishia Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Ni maswali ambayo hata mimi najiuliza sana, sijui ni kwa mujibu wa jina la Kamati lilivyowekwa, Sheria Ndogo, ndiyo tunapata mwanya wa kuzipuuza hizi sheria au sijui ni kitu gani kinatufanya tunapata huu mwanya wa kuzipuuza sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Azimio lililotolewa na Bunge kwenye Mkutano wa Nane na wa Tisa, wote tunaweza kuona ni *gap* la kiasi gani hapa ambalo Wizara husika zilitakiwa kuchukua hatua na mpaka kufikia leo zilitakiwa ziwe tayari zimekamilisha. Cha kusikitisha tunamaliza Mkutano wa 10, ni miezi kadhaa hapo imepita, lakini ukiangalia bado changamoto hizi zinawakumba wananchi wetu walio kule chini, ni wapigakura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo la wazi lisiloweza kufichika, lazima tuwe makini katika utendaji wa kazi zetu hususan kwenye sheria. Kwa mfano mmoja ambao nitautumia, katika dosari hizi ambazo zimewasilishwa hapa leo, dosari nyingi zinatoka Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kitu ambacho Ofisi ya Rais, TAMISEMI ndiyo

wanaogusa wananchi wetu katika majukumu ya kila siku. Hakuna siku itapita mwananchi asiweze kuigusa Ofisi ya TAMISEMI. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Ofisi hii ya TAMISEMI ndiyo hiyo ambayo ina mkanganyiko mkubwa na mlundikano wa sheria hizi ambazo dosari hawajataka kuzifanyia kazi. Mfano mmoja niutumie, Sheria Ndogo ya Afya ya Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Igunga, Tangazo la sheria lilikuwa Na. 555 ndani ya Mkutano wa Nane wa Bunge. Kifungu cha 14(3) kinaeleza; "Iwapo abiria atatupa taka nje ya chombo cha usafiri, kosa litachukuliwa limetendwa na mmiliki wa gari, dereva ama kondakta wake."

Mheshimiwa Naibu Spika, marekebisho yakatakiwa ibadilishwe na kuwa hivi; "Marekebisho yafanyike katika sheria ndogo hii ili kuhakikisha mkosaji anatumikia adhabu kutokana na kosa alilotenda." Azimio tayari hapa limeshaweka wazi. Sasa sijui Wizara ni kitu gani ambacho ilikuwa inakihitaji zaidi. Si Azimio limeshasema kwamba tuondoe mmiliki wa gari, dereva na kondakta, tumlete mtenda kosa awajibike kutumikia kosa lake. Ni nini changamoto? Kila kitu kimeshafafanuliwa tayari. Ndiyo pale pale tunarudi tunasema labda ni kwa sababu imeitwa Sheria Ndogo, lakini si inatumika kama sheria? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine kubwa zaidi ambayo naiona ni kwamba, bado Tanzania tunatunga sheria kwa kuangalia hapa tu. Hatutungi sheria zitakazoangalia mwaka 2025, 2026 mpaka 2030. Kwa sababu, kama ingekuwa tukitunga sheria zetu tunaangalia kitu kinachokuja mbeleni, huu mkanganyiko wa marekebisho ya Sheria Ndogo ya kila wakati, tungepunguza *gap* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mwenyekiti kampongeza na anayo kila haki ya kupongezwa kwa ajili ya utendaji wake wa kazi. Mimi sijawahi kuwasiliana naye, sijawahi kumtafuta, lakini mchangiaji mwenzangu mmoja hapa alisema kwamba, hata ukimtafuta muda wowote ule anakuwa yupo tayari kwa ushirikiano. Ni sawa, lakini twende tukatunge sheria ambazo zitatupunguzia *gap* la

Sheria Ndogo. Hizi Sheria Ndogo na Kanuni tuzipunguze kwa kutunga sheria zinazoendana na muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tuzipe *gap* sheria zetu ili isiwe kila siku, kila Bunge litakalofuata tuna Sheria Ndogo. Kila siku idadi ya Sheria Ndogo inaongezeka. Nina uhakika hata kama hizi ambazo zinafanyiwa kazi ziko nyingi huku nyuma, kila siku tutaendelea kupitia sheria? Ni wakati wetu sasa, twende tukatunge sheria zitakazoendana na Tanzania ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hilo, naenda kwenye Wizara ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Madini nayo wana jukumu kubwa sana katika nchi yetu, mapato makubwa asilimia kubwa yanatokana na Wizara ya Madini, lakini nao sheria tatu ambazo bado hazijafanyiwa kazi na ukiangalia hakuna sababu ya msingi ya kutokufanyiwa kazi sheria hizo. Mfano, kifungu cha 15 kimeweka sharti la muuzaji ama mchimbaji anapotafuta leseni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, Wizara ya Madini, Kanuni ya 6(2) inamtaka mtu yeyote mwenye leseni ya uchimbaji madini atoe *notice* ndani ya siku 90, tangu tarehe ya kutangazwa kwa Kanuni hizi ili hatua nyingine zichukuliwe, ili kuipa nafasi Wizara iweze kutangaza katika Serikali na kuhakikisha Serikali inapata hisa katika mgao huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tuangalie hapa, hii imewekwa kwamba ndani ya siku 90 lakini baadaye kwenye azimio ikasema hapa kikubwa kinachotakiwa ni kitu kidogo tu, sawa! Wameweka ndani ya siku 90 lakini nini azimio lilishauri? Je, kama hizo siku 90 hakufanya hivyo? Itatakiwa kwamba Kanuni ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza kifungu kitakachoonesha adhabu kwa kushindwa kutoa *notice* ndani ya siku hizo 90, jamani mambo yapo wazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inarekebishwa sheria, inatangazwa, Bunge linaanza kuleta maazimio, kwa nini Wizara isitimize wajibu wao?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono Azimio la Kamati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Aida Khenani, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Leonard Madaraka.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Kamati ya Sheria Ndogo kwa kazi kubwa wanayoifanya, lakini nimekuwepo kwenye Kamati hiyo kipindi cha nyuma kidogo miaka mitano kwenye Kamati ya Sheria Ndogo. Changamoto zilizokuwepo zilikuwa kubwa sana, nichukue nafasi hii kumpongeza Mama yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama, amefanya kazi kubwa kwa kipindi hicho ambacho alikuwepo, lakini bado una kazi ya kufanya, pamoja na pongezi unayo kazi ya kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba yetu pamoja na nia njema kwenye Ibara ya 97 Kifungu Kidogo cha Tano, cha Bunge kuamua kukasimu kwenye mamlaka nyingine kutunga kanuni na hizi sheria ndogo, ile maana yake inaondoka kunapokuwa na makosa mengi sana na kuondoa tafsiri halisi ya kukasimisha ili waweze kuwasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotunga sheria hapa, sheria tukishamaliza kuitunga haiwezi kuanza kutekelezwa bila kutunga kanuni na sheria ndogo, lakini shida inakuja hapo tu wanapoenda kutunga sheria ndogo hizo na hizo kanuni, zinakwenda kuondoa kabisa maana halisi ya ile sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nianze na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hizi dosari ambazo Kamati imezungumza leo ni zile sheria ndogo tu chache zilizofika kwenye Kamati, lakini kuna madudu mengi sana. Mimi nataka kusema kwenye Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mpaka sheria ije kuwa *Gazetted* imepita kwa watu wengi sana, ina maana watu wote hao hawana macho, hawaoni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii shida tunapoiona leo na ukiangalia hapa makosa yote ambayo yanaonekana kwenye hizi sheria ndogo, mengi wanatunga hizi sheria kwa ajili ya tamaa na

kujikita kwenye adhabu zaidi kuliko kuwasaidia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo lazima kama Bunge tuyaseme. Kamati ya Sheria Ndogo imepewa nafasi kubwa ya kuwasilisha taarifa zake mara kwa mara ndani ya Bunge, lakini inapotokea imekuwa ni azimio, Bunge limepitisha tunaamini kabisa kwamba waliopewa nafasi Serikalini watakwenda kutekeleza kwa kuwa Bunge tayari limeazimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inapotokea mpaka leo tunazungumza hapa kwamba dosari, Sheria Ndogo zenye dosari 19 hazijafanyiwa kazi. Kwa namna nyingine hakuna lugha nyingine ya kuzungumza zaidi ya kusema ni dharau kwa Bunge kutokuheshimu Mamlaka ya Bunge. Sasa maumivu yanapotokea kwa Watanzania hawaangalii mamlaka zile ambazo tulikasimu watunge, wanaangalia ni Bunge limeamua kuwaumiza wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tutazungumza nini kipya zaidi ya kuwaambia hawa ambao hawajatekeleza waende kutekeleza au adhabu nyingine zichukuliwe na wao ili wajue kwamba kuna maumivu makali yanatokea kwa wananchi wetu. Mimi nimuombe Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, leo tunapozungumzia Sheria Ndogo unazungumzia maisha halisi ya Watanzania kule chini. Kwa hiyo, inapotokea hizi dosari utakuta mwananchi amehukumiwa kwenye kosa hilo hilo la Sheria Ndogo, ameadhibiwa baadaye ndiyo mnakuja kugundua makosa wakati tayari wananchi wameshaumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo lazima, sasa hivi tunapotunga hizi Sheria Ndogo zianze kupitiwa kabla ya kuanza kutumika. Kwa sababu unakuja kugundua wakati maumivu tayari yameshatokea kwa Watanzania, lakini ukizitazama hizo Sheria Ndogo nyingi zimezungumzia adhabu hazijaweka sehemu ya uwajibikaji wa Serikali, na ndipo shida inapoanzia hapo. Kungekuwa na uwajibikaji nafikiri wote tungerudi kuziangalia hizi Sheria Ndogo kabla ya kuanza kutumika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiangalia hata kwenye Mabaraza ya Madiwani, wale wataalam wetu wanashindwa kyutumia taaluma zao kuwaambia sheria hii haitafaa kama ambavyo wanataka kupitisha, wakati mwingine ni tamaa ya kutaka makusanyo. Kwa hiyo, wanatunga sheria ambazo hawaangalii athari kwa Watanzania, wanangalia makusanyo kwewnye Halmashauri yao. Sasa hatuwezi kwenda hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapotunga hizo kanuni na Sheria Ndogo kuna taratibu za kufuata ni pamoja na kuangalia Sheria Mama imesema nini. Kama inaanza kukiuka mapema Sheria Mama inawezekanaje wataalam waliopo huko ambao ndiyo wawakilishi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wanaruhusu zinapita mpaka zinaanza kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tunaposema kwamba Sheria Ndogo zimeshakuwa *gazetted* leo inawezekana katika zile ambazo tayari mnazipeleka kwenye gazeti la Serikali zilishaanza kutekelezwa huko miaka mingi, halafu mpaka ije ifike kwenye Kamati. Hizi Kamati, kwa mfano yale makosa ambayo ni ya kiuandishi siyo kazi ya Kamati kuja kuangalia hayo makosa, hivi Ofisi ya Mwanasheria hawakuona kwamba hizi hazitakiwi kuingia kabisa kwenye Sheria Ndogo? Mpaka zinakuja kufika kwenye Kamati ndiyo wanagundua, yaani Kamati ndiyo wanagundua kwamba kuna kosa la kiuandishi. Hii Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kunashida gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mimi niombe, inawezekana pia kutokufanya semina elekezi za mara kwa mara kwa Wanasheria wetu kwenye Halmashauri. Tulizungumza mwaka juzi Mheshimiwa Jenista Mhagama, alifanya hivyo mwaka jana, lakini usifanye mara moja moja, hawa watu waiteni ili angalau wabadilishane uzoefu, na wakati mwingine tusitunge sheria kwa sababu sehemu fulani wametunga ndiyo maana inatupeleka kwenye tamaa. Sheria hizi lazima ziendane na mazingira halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Sheria Ndogo ambayo inazungumzia kwamba ni marufuku mwananchi kuzurura kuanzia saa nne usiku, hiyo ni sheria ya wapi? dunia gani? Sasa unaweza ukaona mpaka inatungwa, inapitishwa hivi kweli

hakukuwa na wataalam waliyoipitia mpaka ikafika ikaanza kutekelezwa. Haya mambo hayakubaliki. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mengi ya kuzungumza hapa, lakini hatuwezi kuzungumza wakati kuna maazimio kadhaa ambayo yameshapita hamjatekeleza. Nimuombe Mheshimiwa Mchengerwa ameingia TAMISEMI. TAMISEMI ni kitu kikubwa sana ambacho utekelezaji wake ni mgumu, lakini ukiangalia kwenye dosari hizi Sheria Ndogo ambazo zina dosari nyingi zimeelekea TAMISEMI ambazo hazijatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hatutakuhukumu moja kwa moja, lakini hapo alikuwepo Waziri na Bunge limeshaazimia, haiwezekani Bunge linaazimia tunakuja tena kwenye Bunge lingine yale mambo hamjatekeleza ni dharau kwa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe Kiti chako, hatuwezi kuwa tunapoteza muda kuzungumza mambo ambayo tayari Bunge lilishaazimia ni dharau kwa Bunge. Baada ya kusema hayo kwa kuwa mengi yameshazungumzwa ninaomba Ofisi yako Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ongeza umakini kwenye kupitia sheria hizi ambazo zinaumiza watanzania. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa tunakwenda kwa Dkt. Leonard Madaraka. Jiandae Mheshimiwa Balozi Mulamula.

**MHE. ENG. DKT. LEONARD M. CHAMURIHO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia, nakushukuru kwa hilo. Pili ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuliongoza Taifa hili vizuri.

Tatu, ninapenda kuwapongeza Mawaziri wote waliofanikiwa kuhudhuria katika vikao vyetu vya Kamati ya kudumu ya Sheria Ndogo, kwani kwa kufanya hivyo wamekuja kujadili dosari mbalimbali ambazo tumeziona katika sheria

ambazo wamekasimiwa kuzitengeneza na Bunge lako hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari hizi kwa kweli huwa zinakwamisha utekelezaji wa sheria mama au zinaleta usumbufu katika utekelezaji wa sheria hizi kwa wananchi. Katika Sheria Ndogo hizi huwa kuna majedwali mbalimbali ambayo hukusanya taarifa mbalimbali ambazo zipo kwa wingi na ambazo zinahusu mambo yanayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, dosari katika majedwali haya huwa yanaathiri sana au kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa sheria hizo, ambazo huwa zimetungwa kutokana na Sheria Mama na kama nilivyosema awali zinaleta usumbufu mkubwa katika utekelezaji wake. Nitatoa mifano ya majedwali mawili, kwanza nitaanzia kanuni za usafirishaji wa mazao ya misitu kuingia ndani ya nchi na kutoka nje ya nchi, ambazo ni tangazo la Serikali Namba 266 iliyotolewa tarehe 31 Machi, mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kanuni hizi ilikuwa ni utekelezaji wa Sheria za Misitu, Sura Namba 323 ambayo katika hizo tunapatia mapato ambayo yanachangia katika uendeshaji wa kila siku wa Serikali na Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali hilo kuna vituo vya kuingia na kutoka nchini kwa mazao ya misitu, ukiangalia njia mbalimbali za kutokea nje ya nchi ambazo ni njia za usafiri utaona kila aina ya usafiri, aidha imewekewa au kuna nyingine hazikuwekewa. Nitapitia moja moja, tukianza na barabara, katika njia ya barabara kanuni hizi zimetoa vituo vya kutosha ambavyo vinaweza kutumika katika kukagua bidhaa hizo. Tukienda kwenye usafiri kwa njia ya reli, vituo vilivyotolewa ni Moshi, Arusha, Tunduma na *Kahe junction* tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa unaona dhahiri kwamba kuna vituo vingine ambavyo vinahusisha mazao kutoka nje ya nchi ambavyo havikuwekwa, hivyo kutokuwemo katika vituo hivyo, aidha kutaleta usumbufu kwa wananchi kwamba wakifika katika vituo hivyo itabidi wasafiri umbali mkubwa kwenda kwenye vituo vingine ambavyo vinaweza kusababisha ukaguzi wa mazao

hayo kitu ambacho ni usumbufu. Kwa hiyo, hili limebidi Kamati yetu imeshauri lirekebishwe na tungeomba Wabunge mtuunge mkono ili dosari hiyo iweze kusahihishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika usafiri wa njia ya maji ambao unahusisha bandari, katika Bahari ya Hindi vituo vimewekwa vya kutosha kutoka kaskazini hadi kusini. Vilevile katika Ziwa Tanganyika ambapo ni mpaka kati ya nchi yetu na nchi zingine vituo vimewekwa. Ukiangalia Ziwa Victoria ambalo tunapakana nalo katika nchi mbili, hakuna kituo ambacho kimewekwa kwa kusafirisha mazao hayo. Hivyo basi inamaana wananchi wakitaka kusafirisha mazao yao ya misitu nje ya nchi kwa njia ya maji usafiri ambao unajulikana ulimwenguni kwamba ndiyo usafiri wa rahisi kabisa hakuna vituo. Kwa hiyo, inabidi huyo mwananchi asafiri kwenda katika vituo ambavyo vinaruhusiwa kitu ambacho ni usumbufu mkubwa wakati ambapo vingeweza kuwekwa vituo katika njia hizo za usafiri wa maji katika Ziwa Victoria na ikaweza kurahisisha jukumu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika Ziwa Nyasa hakuna kituo ambacho kimewekwa na wakati Ziwa hilo ni mpaka kati yetu na nchi ya jirani. Kwa hiyo, kukosekana kwa vituo hivyo mazao ya miti kuingia au kutoka kupitia Ziwa hilo ni usumbufu au inamuongezea gharama huyo mtumiaji wa usafiri huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, usafiri wa anga. Vilevile katika usafiri wa anga ambao husafirisha kupitia viwanja vya ndege hakuna kituo hata kimoja ambacho kimewekwa kwa ukaguzi wa mazao hayo. Hiyo nayo inaleta usumbufu kwani ina maana kwamba, unaweza kupata usumbufu mkubwa ukiwa pale wakati ambapo ukaguzi huo ungeweza kufanyika pale kwani inafahamika kabisa kwamba ule ni mpaka ambao unaweza kutumika katatika kusafirishia mazao hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mwingine unatokana na majedwali ambayo yametengenezwa katika Kanuni ya *The Law School of Tanzania Admission Fee and Conduct of Practical Legal Training* Kanuni za mwaka 2022. Katika kanuni hizo ukiangalia majedwali pale hakuna *form* maaalum itakayotumika katika maombi kulingana na kanuni ambayo imetengenezwa, Kanuni

Namba Nne. Huu ni usumbufu mkubwa kwani unaweza ukakuta kwamba katika maombi yale muombaji akashindwa kuweka vitu ambavyo vinavyotakiwa ambayo italeta usumbufu katika udahili wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile katika kanuni hizohizo ukiangalia jedwali la ada limetumia maneno ambayo hawakutoa maana yake ambayo yanaweza kuleta mkanganyiko mkubwa. Kwa mfano, wametumia neno *Tanzanian students* bila kueleza maana yake. Katika uchambuzi wetu tumeona hili neno linaweza kuleta usumbufu kidogo, kwamba je, linamaanisha ni raia wa Tanzania au linamaanisha mtu aliyesomea Tanzania au vinginevyo? Sasa hiyo ili isiweze kuleta huo mkanganyiko katika hayo mambo tulikuwa tumeazimia kwamba maneno ambayo yanaweza kuleta utata katika matumizi yake yaweze kutolewa tafsiri katika kanuni ili kuwafanya watumiaji waweze kuyatumia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ikiambatana na hiyo vilevile kuna neno *non-Tanzanian student* ambayo katika uchambuzi wetu tuliona kwamba linaweza kutafsiriwa kwamba ni mwanafunzi ambaye hakusomea Tanzania. Anaweza kuwa mtanzania ndiyo lakini hakusomea Tanzania na akaambiwa wewe ni *non-Tanzanian student* kwa hiyo, tukasema hii tafsiri zitolewe ili mkanganyiko huu usiwepo kabisa katika kanuni hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jedwali la kwanza vilevile za kanuni hizo ziliwekwa ada mbalimbali ambazo zinatumika katika chuo hicho, lakini unaona ada ya maombi ya kujiunga haina *form* wakati ambapo imeainishwa kule ndani na inaweza kuleta usumbufu. Katika jedwali hilo hilo vilevile imeoneshwa changamoto ya kuomba ada kwa Wanasheria Wasaidizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Sheria Mama ambayo ni *The Law School of Tanzania Act,* Sura ya 425 katika kifungu cha pili, kinatamka waziwazi kwamba sheria hiyo inatumika kwa wanasheria tu, sasa ukikuta kwenye jedwali wameweka ada za Wanasheria Wasaidizi wakati sheria mama inadai sheria hiyo itumike kwa Wanasheria tu wenye shahada ina maana kwamba Kanuni hizi zimevuka mipaka yake na kufanya

kitu ambacho hakiruhusiwi, hivyo inabidi ifanyiwe marekebisho ya kuweza kuondoa kasoro hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo tumeliona waziwazi ni kutohuishwa kwa majedwali kwa wakati. Katika jedwali hilohilo ambalo lilikuwa linahusu ada, kuna ada ya mapitio yanayofanywa na *NACTE,* taasisi ambayo haipo kisheria sasa hivi na imebadilishwa, hivyo uhuishwaji wa Majedwali haya ni muhimu kwa wakati ili yasilete usumbufu katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mchango huu wa majedwali, tumeazimia kwamba majedwali haya yarekebishwe kwa wakati ili tuweze kupata utekelezaji mzuri wa sheria hizi kama ambavyo Bunge liliazimia kwenye kutunga sheria mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Balozi Mulamula, halafu mjiandae Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MHE. BALOZI LIBERATA R. MULAMULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi nami nichangie kwenye taarifa ya Kamati yangu ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo kama ilivyowasilishwa na Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kipekee nimshukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipangia Kamati hii, kwa sababu imepanua wigo wa uelewa wangu wa umuhimu wa Sheria Ndogo katika ustawi wa jamii na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu, Makamu wake, Wajumbe wenzangu wa Kamati na Makatibu kwa ushirikiano mkubwa walionipatia na kuniwezesha kujifunza mengi kama Mjumbe wa Kamati katika kipindi kifupi na kutambua umuhimu wa Sheria Ndogo ambazo zinagusa moja kwa moja maisha ya wananchi katika utekelezaji wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kupoteza muda, naunga mkono hoja ya Kamati yetu ya Kudumu ya Sheria Ndogo na ninakubaliana na taarifa na mapendekezo kama yalivyowasilishwa. Naomba pia nitumie fursa hii kwanza kuipongeza Serikali kupitia Wizara husika kwa taarifa walizotupatia pamoja na semina zilizotolewa na taasisi mbalimbali za Serikali katika kutuelimisha, kutuhabarisha kuhusu utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu kama zilivyopitishwa na Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kamati tumepata wasaa wa kuchambua Sheria Ndogo zilizowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kama ilivyoelezwa na Mwenyekiti wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni, naomba kutoa pongezi kwa Serikali kwa hatua nzuri ya kukamilisha marekebisho ya Sheria Ndogo mbalimbali kutokana na dosari zilizobainishwa katika utekelezaji wa kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kama zilivyowasilishwa leo kwenye Bunge lako tukufu kupitia Hati iliyowasilishwa Mezani na Waziri Mkuu. Leo tumeshuhudia kwamba kumekuwa na Matoleo 22 ya Gazeti la Serikali, kuanzia mwezi Aprili mwaka huu 2023 hadi Mwezi huu wa Septemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua ya kutangaza marekebisho katika Gazeti la Serikali ambayo imefikiwa na Wizara zinazohusika katika kipindi husika, ni mwitikio mzuri wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayolenga kuondoa changamoto zilizobainishwa katika Sheria Ndogo kama ilivyooneshwa kwenye jedwali la utekelezaji wa Maazimio ya Bunge kwenye taarifa ya Kamati. Hatua hii inastahili kupongezwa kwa kuwa ni hatua ya juu ya uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja mbalimbali za Kamati, mamlaka zinazohusika zimeweka juhudi ya kusahihisha dosari zilizobainishwa na Kamati. Kwa kufanya hivyo, madhara ya dosari hizi yameondolewa kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, Sheria Ndogo ya Afya na Usafi wa Mazingira ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mwaka 2022, kifungu cha 14(3) ambacho Mheshimiwa

mwanakamati mwenzangu, Mheshimiwa Maryam alikigusia, kinaeleza kwamba iwapo abiria atakayetupa taka nje ya chombo cha usafiri, kilikuwa kimeweka sheria kwamba mmiliki wa gari, dereva au kondakta ndio aweze kulipa faini isiyozidi shilingi 50,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwamba Serikali imelisikia hili na imeweza kutekeleza maagizo au Azimio la Bunge iliyoitaka kufanyiwa marekebisho ili kumtaka mkosaji mwenyewe aweze kuadhibiwa kwa kosa alilolifanya. Kwa hiyo, tumeona leo kwamba marekebisho ya kifungu hicho yamefanyika kwa kufuta kifungu hicho na kukiandika upya kwa kumwondoa mmiliki na dereva katika makosa yanayotendwa na abiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo inaakisi misingi ya haki ya mtu kuadhibiwa iwapo ametenda kosa na siyo vinginevyo. Pamoja na kuipongeza Serikali kwa hatua hiyo, Kamati kama Wajumbe wenzangu walivyosema, imebaini ucheleweshaji katika kurekebisha dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Sheria Ndogo. Ucheleweshaji huo unasababisha athari hasi za dosari zilizobainishwa katika Sheria Ndogo mbalimbali na hivyo kushindwa kutatua kero ambazo Bunge lako tukufu lililenga kuziondoa kwa ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, zimetajwa sheria mbalimbali ambazo zinacheleweshwa au hazijatekelezwa kutokana na Maazimio ya Bunge, lakini naomba nitoe mfano tu kuhusu hii Sheria ya *Environmental Management Control and Management Carbon Trading Regulation of 2022,* hii inahusu maombi ya biashara ya *carbon*. Tumekuwa tukiongelea hilii hata wakati nikiwa kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara, kwamba hii iweze kutungiwa kanuni ambayo inaeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nafurahi kusema kwamba kama Wajumbe wa Kamati, sote tunaelewa umuhimu wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ambayo imekuwa *engine* ya Bunge lako katika uthibiti wa Sheria Ndogo na utekelezaji wake ulio na tija kwa kuwa sheria hizo zinazogusa moja kwa moja maisha ya wananchi. Ibara ya 8(b) ya Katiba inaeleza kwamba lengo kuu la Serikali ni ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba nirudie kwamba naunga mkono hoja ya Kamati yetu mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Shally Raymond, Mwenyekiti wa *TWPG* anawaomba kuwatangazia Wabunge wanawake wote kuwa tarehe 5 Septemba, 2023 ambayo ni leo mara baada ya kuahirishwa Kikao cha Bunge, Mheshimiwa Spika atakutana na Waheshimiwa Wabunge wanawake wote Ukumbi wa Pius Msekwa. Mnahimizwa kufika bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita, Naibu Waziri wa Madini, jiandae Waziri wa TAMISEMI, jiandae Waziri wa Katiba na Sheria na baadaye atakuja *Attorney General.*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimwa Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kusema kwa kifupi kabisa, kuchangia hii hoja iliyoletwa na Kamati ya Sheria Ndogo na suala mahususi ambalo linahusu marekebisho waliyoagiza Wizara ifanye kwenye kanuni ya ushirikishwaji wa Serikali katika biashara ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, napenda kuipongeza Kamati kwa sababu wanafanya kazi nzuri sana na walitupa fursa ya kuja kuelezea utekelezaji wa hoja hizi ambazo wamezileta leo mbele ya Bunge lako Tukufu, nasi kwa heshima kubwa kabisa tuliwaomba baada ya muda wa wiki moja na nusu tuwaite kwenye semina ambapo tutaitumia kuelezea kuhusu hizi kanuni za ushiriki wa Serikali za mwaka 2022, sambamba na kupewa majibu ya utekelezaji wa hoja ambazo walitupatia tufanye marekebisho kwenye kanuni hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ya tarehe 31 mwezi wa Nane, tulipata hiyo fursa tukatoa elimu na tukawaeleza kwamba marekebisho yote tuliyoagizwa tuyafanyie kazi, tumeshayafanyia kazi, zimepita kwenye mchakato mzima wa kuhakikiwa mpaka na *AG* na zikarudishwa kwetu kwa ajili ya Waziri kutia Saini ili ziweze kutangazwa katika Gazeti la Serikali kupitia *GN.* Kwa bahati nzuri,

maana sitaki kusema kwamba ni mbaya, siku ile ambayo Waziri alikuwa atoke akazisaini, Mungu akamjalia, akamwonekania, akateuliwa kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ile shughuli ya kusaini ili ziende kwenye Tangazo la Serikali likawa limesimama, na ndani ya muda huu mfupi basi, leo tumejikuta tena tupo mbele ya Bunge lako tukufu kujibu hoja ya kuonekana kama tumepuuza maagizo ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ukweli ambao Mungu anaujua, tulipokaa nao tarehe 31, tuliwaridhisha kwamba tumetekeleza, imebaki tu utaratibu wa kutangaza. Nami nafahamu kwamba Kamati hii inafanya kazi nzuri nasi tunaiheshimu kazi yao na Wizara siku zote imekuwa ushirikiano kwa Kamati za Bunge inapohitajika. Kwa hiyo, nitumie tu jukwaa hili kuihakikishia Kamati hii na Bunge lako tukufu kwamba kazi waliyotutuma tukaifanye, tumeifanya kikamilifu na kwa uadilifu wote, sema tu imechelewa kumalizika na kuja Mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na hoja ndogo ya maoni ya wadau wengine kuhusiana na kanuni hizo ambazo tulianza kuzifanyia kazi. Mwanzoni tulidhani tutatoa tangazo moja na marekebisho yote ya Kamati na wadau wengine mbalimbali yangeweza kuingizwa, lakini baada ya kuona kwamba Kamati inataka kuona utekelezaji wa jambo lao tukazileta hizo hoja zao tatu mbele, tukafanyia marekebisho iende kwenye *GN* ambayo ingetoka ambapo baadaye tungetoa nyingine ya ku-*accommodate* maoni mbalimbali ambayo wadau waliendelea kutoa kuhusiana na kanuni hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi tu, nilihakikishie Bunge lako kwamba sisi tumefanya kazi marekebisho yaliyoelekezwa na ndani ya muda mfupi tangazo hilo litakapotoka tutaweza kuziweka mbele ya Bunge lako tukufu ili wajiridhishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Sasa ni Waziri wa TAMISEMI, jiandae Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa maoni na maelekezo ambayo wametupatia Wizara yetu ya TAMISEMI. Lazima nikiri kwamba lengo la Serikali yoyote duniani ni ustawi wa wananchi wake, na hii ndiyo sababu Wizara yetu ya TAMISEMI imedhamiria kuiweka Wizara mikononi mwa wananchi. Tunaposema tunaiweka Wizara mikononi mwa mwananchi, maana yake tunawapa wananchi mamlaka ya kutukagua na kuturekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi huu ni msingi ambao umepatikana katika Ibara ya 8 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 9 na kuendelea mpaka Ibara ya 21, ambayo imewazungumzia wawakilishi wa wananchi katika maeneo yetu. Sauti ya wananchi inawakilishwa na Madiwani na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Bunge hili, Kamati imepewa mamlaka ya kuwawakilisha Waheshimiwa Wabunge wengine. Kwa hiyo, sisi kama Wizara lazima nikiri kwamba tumepokea maelekezo ya Kamati. Inawezekana maelekezo mengi huko nyuma hayakufanyiwa kazi, lakini siyo wakati wangu. Naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba kazi hii kubwa ambayo Kamati imefanya, sisi Wizara tutahakikisha kwamba yale maelekozo ambayo Kamati imetoa, kwetu sisi Wizara tunakwenda kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekubaliana na wenzangu wote kwamba ule utendaji wa kimazoea sasa tunauacha *(business as usual)* tunauacha. Ili tuweze kuwawakilisha wananchi vyema kama ambavyo nimesema nchi ni ya wananchi, wawakilishi wa wananchi ndio hawa Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Madiwani kwa misingi ya Ibara ya 21 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, tutahakikisha sheria zetu, kanuni zetu zinaenda sambamba na tafsiri iliyotolewa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge, tutahakikisha ile misingi na mifumo ya

utungwaji wa kanuni ambayo pengine huko nyuma zilikuwa haziendi vizuri, tutakwenda kuziboresha ili kanuni zetu zote zinazotungwa ziwe ni zile ambazo zinaangalia maslahi ya wananchi wetu katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba niseme mbele ya Bunge lako tukufu kwamba mapendekezo ya Kamati ambayo yametolewa yana msingi wake, kwa sababu Kamati hii ndiyo Kamati ambayo inatoa sauti ya Wabunge wote ndani ya Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, tutakwenda kuyafanyia kazi mapendekezo yote ya Kamati na niwaombe Waheshimiwa Wabunge wajenge matumaini. Tutakwenda kuboresha mifumo yetu ya utungwaji wa kanuni zetu, na pia tutaboresha mifumo yetu ya utungwaji wa sheria zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshawaeleza watendaji katika Wizara hii, kila moja wetu kijipanga hasa kwa sababu ni lazima tulinde maslahi ya wananchi wetu. Ninaposema tunakwenda kulinda maslahi ya wananchi wetu, ni kwenda kutunga kanuni na sheria ambazo zinaangalia maslahi ya wananchi wetu katika maeneo yetu mbalilmbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba ninaipongeza Kamati na ninaunga mkono hoja ambazo Kamati imetoa na sisi kama Wizara tutakwenda kujipanga vizuri, mimi na wasaidizi wangu, kuhakikisha kwamba yale mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa kwa Wizara yetu hii ya TAMISEMI, ambayo ni Wizara ya wananchi, na kwa kuwa tayari nimeshatoa maelekezo kuirejesha Wizara hii kwa wananchi, tutakwenda kulinda maslahi ya wananchi kwa kuhakikisha kwamba kanuni zinazotungwa ni kanuni ambazo zinalenga kulinda na kutetea ustawi wa wananchi katika maeneo yetu yote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata katika misingi ya sheria, tutajikita katika kuhakikisha kwamba sheria zetu zinaendana na tafsiri ya Katiba kama ambavyo Katiba imefafanua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri kwa maneno yako yenye imani kubwa kwa Bunge. Waziri wa Katiba na Sheria, jiandae *AG.*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa imani ambayo ameendelea kunipa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naungana kabisa na maoni mazuri ya Kamati ambayo yametolewa na sisi tumeyapokea na tunaendelea kuyafanyia kazi. Nitumie nafasi hii kusema kwamba majukumu ya Bunge kwa mujibu wa Katiba yetu Ibara ya 62, 63 na 64 ni pamoja na kuisimamia Serikali, kupitisha bajeti na kutunga sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema kutunga sheria ni majukumu ya Bunge, ndani yake ni pamoja na kurekebisha sheria mbalimbali. Hivyo, sheria zinavyopita hapa kuja kutungwa, kurekebishwa ndiyo majukumu ya msingi ya Bunge letu. Nalishukuru sana Bunge letu kuwa na Kamati maalumu ya Sheria Ndogo. Kamati hii maalum ya Sheria Ndogo ni muhimu sana, inatupa maoni mengi mazuri ya kuboresha ya sheria mbalimbali. Kwa hiyo, nilitaka tu kwanza tukumbushane kwamba suala la kutunga sheria ni na kurekebisha sheria ni majukumu ya msingi hivyo. Hivyo, sheria imnaweza ikaja hapa kufuta sheria ya nyuma, kurekebisha, kuongeza na kuboresha. Ndiyo majukumu ya msingi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea maoni mbalimbali na hivi sasa tunakwenda kuboresha Sheria ya Tume yetu ya Kurekebisha Sheria. Tunakwenda kurekebisha sheria hii, tunataka sheria zote za Bunge zinazotungwa, kabla ya kutungwa tupitishe Tume ya Kurekebisha Sheria *(Law Reform Commission)*. Lengo la kupitisha, ni kwamba zifanyiwe tafiti kuona kama sheria hii inafaa, ipo kwa muda muafaka na kama itasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni haya yanatokana na Kamati zetu ikiwa ni pamoja na Kamati ya Sheria Ndogo.

Tunaposema tuziangalie hizi sheria vizuri, kwa hiyo, tunakuja na maboresho, na huu ni mwanzo. Maoni mengi mazuri yametolewa, tutaendelea kuboresha. Kwa hiyo, lazima sheria iendane na Katiba, lazima tufanye tafiti. Tumesema sasa sheria hizi wakati wa marekebisho lazima zipitiwe na tume yetu ya kurekebisha sheria, kufanya uchambuzi na tafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuunga mkono hoja na kuendelea kukumbushana kwamba jukumu la Bunge ni kutunga sheria na kurekebisha. Pia tuzazo halmashauri zetu ambao pia wanalo jukumu la kutunga sheria ndogo kutokana na eneo lenyewe. Kama eneo lina changamoto ya kipindupindu basi watu wasitupe taka hovyo. Kama kuna changamoto ya masuala mbalimbali, nakumbuka wakati wa *Covid* nchi nyingine walisema *lock down* lakini sisi tulisema tunafanya kazi. Kwa hiyo, badala ya *lock down* wengine wanasema basi kutembea iwe mwisho saa fulani ili kudhibiti masuala ya magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na *Covid*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na kuipongeza sana Kamati ya Sheria Ndogo ambayo inafanya kazi nzuri na maoni mliyotoa tutayachukua na kwenda kuyafanyia kazi tukianza na marekebisho ya Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria. Zitapitiwa, zitafanyiwa uchambuzi, zikija huku zinaendelea kuwa vizuri na zitapita katika Kamati zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Attorney General, jiandae Mwenyekiti mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, Kamati pamoja na wajumbe wake na wote waliobahatika kuchangia hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi kusikia dosari ambazo zimetajwa hapa pamoja na maazimio. Baada ya kusikiliza yote jambo la kwanza ambalo ninapenda kukariri ni kwamba, ni kweli kwa mujibu wa mgawanyo wa madaraka ya vyombo vyetu

mhimili kwa mujibu wa Ibara ya 4. Tunatambua kwamba mamlaka yote ya Serikali yanatoka kwa wananchi kwa mujibu wa Ibara ya 8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge hili kwa mujibu wa Ibara ya 63(3)(d) ndiyo linalotunga sheria zetu. Pia tunatambua kuwa ustawi wa wananchi, msingi wake ni ule umewekwa kwenye Ibara ya 146 ambao madhumuni ya kuwepo kwa mamlaka zilizopo, zinazotunga sheria maana yake inafuata ule mlolongo ambao unafuata mamlaka zilizotajwa na mihimili.

Mheshimiwa Naibu Spika, yote ambayo yameelezwa hapa na dosari hizi tunatambua kwamba sheria mama zinapotungwa ndiyo zenye kutamka kuwa nani mwenye dhamana ya kutunga Sheria Ndogo na vilevile ni nani mwenye dhamana ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kubwa imeendelea kufanyika na tunalipongeza sana Bunge hili kwa sababu, kila sheria zinapotungwa kati ya mambo ambayo yamekuwa yakinishughulisha Bunge hili na Waheshimiwa Wabunge ni pale ambapo kuna ugatuaji wa kutugwa kwa Sheria Ndogo au kanuni kufuata masharti ambayo yanakuwa yamezingatia Sheria Mama.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ilivyotolewa na tukiangalia hata kwa mtiririko wa miaka hii miwili. Kumekuwa na maendeleo makubwa ya kupungua kwa dosari mbalimbali. Pia tunatambua kuendelea kuwepo kwa dosari hizi lakini yapo mengi ambayo yanaendelea kufanyika ambayo tunaungana na Kamati kwamba dosari ambazo zimetajwa ni wajibu wetu kama Serikali kuhakikisha kuwa zinatatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Mheshimiwa Mpinga katika mchango wake ameeleza vizuri. Kwamba, tangu mwaka 1920 kanuni ya sheria ndogo ya 4151 zilifungwa lakini kwa sasa kwa zoezi linaloendelea ni kuhakikisha kwamba kuna zoezi la kuhuwisha pamoja na kubaki na zile Sheria Ndogo ambazo zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria mama 446 zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanya hivyo kwa sasa sheria ndogo hai zilizopo kutoka hiyo 4151 zimebaki 25,000. Dosari ambazo zimekuwa zikitajwa hapa na hatua ambazo tumekuwa tukizichukua, tunatambua uwepo wa upungufu katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano mwaka jana tarehe 7 Novemba yalitoka maelekezo kwenda kwa watendaji Wakuu wa Halmashauri, Tawala za Mikoa na Watendaji Wakuu Serikalini, kulipo na upungufu wa wanasheria, kuhakikisha kwamba wanasheria waliopo kwenye ofisi zilizo jirani wanatumika kwenye mazoezi ili kuhakikisha kazi za kisheria zinatekelezwa kwa kufuata misingi ya Sheria Mama na matakwa mengine ya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, hili limesaidia kuendelea kupunguza dosari ambazo zimekuwepo. Pia imeelezwa hapa, mafunzo na maelekezo mengine ya kiutendaji ambayo yanalenga kuboresha namna ya kuhakikisha sheria zetu zinakuwa hai na zinatekelezwa na kupunguza kero kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua ingawa Mheshimiwa Mariam hajawahi kuongea na mimi, ni kweli. Lakini ninaamini kufikika kwangu na watendaji wa ofisi yangu kumechangia sana kuboresha changamoto mbalimbali zinazopatikana kuanzia ngazi za halmashauri na maeneo mengine ya kiutawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni wajibu wetu kuwajibika. Pia siku zote Mheshimiwa *Chief Whip* siku zote ameendelea kuratibu changamoto zinazopatikana na kuzisambaza kwa wadau wetu. Kwa hiyo, hizi ni hatua ambazo zitaendelea kuwa endelevu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizidi kuomba katika hatua hii, nimeelewa kama nilivyo mimi na Waheshimiwa Wabunge kama nyinyi mlivyo na uhusika wenu kwenye mabaraza ya ngazi ya madiwani. Tuendelee kushirikiana wote kuhakikisha kwamba dosari hizi zilizosalia zinapungua kwa kuendelea kufanya kazi vizuri na Wakurugenzi, Wasimamizi wa Mamlaka katika ngazi

mbalimbali na mamlaka nyingine kuhakikisha tunaendelea kuboresha mifumo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ipo mipango mingine mingi ambayo Serikali inaendelea kuifanya, maana Mheshimiwa Kenani ameuliza ofisi yetu tunafanya nini? Kwa sasa tumeendelea sana kuboresha ile *division* ya uandishi wa sheria. Maboresho ya sheria yanakuja ili iweze kuwa na mfumo ambao utawezesha kusimamia vizuri kazi za kisheria hasa kwenye eneo la uandishi, kutoka ngazi za chini hadi ngazi za juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii itaendana na kile ambacho Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ameeleza, mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba *Law Reform Commission* na yenyewe inahusika kikamilifu kuhakikisha sheria zetu zinakuwa zinaongozwa na tafiti na zinakuwa chachu ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na haya yote sisi tutaendelea kuhuwisha sheria zetu na kufanya urekebu na kuhakikisha tunakuwa na sheria kwa lugha ya Kiswahili. Kama nilivyosema katika sheria mama 446 tayari sheria 258 tumeshazitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Sheria zote mpya zinazotungwa sasa zinatungwa kwa lugha ya Kiswahili ambayo nayo hii ni nyenzo muhimu sana kuwafanya wananchi wetu kuelewa hizi sheria na maana zake pamoja na madiwani wetu na watu wote wanaotumika katika mchakato wa kutugwa kwa Sheria Ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimalizie kwa kusema kwamba tunaipongeza sana Kamati pamoja na mapendekezo haya. Faraja yetu ni kwamba muda umetolewa kufikia Tarehe 2 Oktoba, basi hatua mbalimbali ziwe zimechukuliwa. Nitaendelea kufikika na nafikiri ambaye hajanifikia basi atakuwa yeye labda sababu zake. Kila mmoja hapa naamini katika kumbukumbu zangu sijawahi kufikiwa na mtu alafu nisimpatie jibu au nisimpatie huduma inayostahili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana na ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, Mwenyekiti mtoa hoja.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SHERIA NDOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nihitimishe hoja yangu. Napenda kusema nawashukuru sana niseme nawashukuru sana Wabunge kwa kuchangia hoja yetu kwa kuiboresha. Tumepata wachangiaji kumi na moja na nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuongezea pale ambapo palistahili kuongezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria Ndogo ni sheria muhimu sana. Ninaweza kusema ni muhimu kuliko hata sheria kubwa (sheria mama) kwa sababu kwanza zipo nyingi kuliko sheria mama. Unaweza kukuta sheria mama moja ina Sheria Ndogo kumi au ishirini chini yake. Pia Sheria Ndogo zinaathiri wananchi moja kwa moja ndio zinawagusa kwenye *barrier,* kwenye majumba yao, biashara zao, usafiri na siku hadi siku ndizo zinazowaathiri katika maisha yao. Kwa hiyo, sheria ndogo ni sheria muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeeleza hapa na Wabunge wamechangia kwa urefu kabisa. Kuna upungufu mkubwa ambao tumeyabaini kwenye sheria hizi ndogo. Sasa nafikiri ni vizuri tukasisitiza kwamba wale ambao tumewakasimu mamlaka ya kutunga sheria ndogo, wizara, halmashauri na mashirika mbalimbali ya umma wawe makini zaidi katika kazi hii ambayo tumewakasimu. Bunge limewakasimu na tunategemea kazi yao itakuwa nzuri, isiwe ya hovyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wasikiuke Katiba kwa kuwa ipo na wanaijua, kwenye mamlaka hizo kuna wanasheria, kuna wataalam, wanasiasa na wanajua madhara ambayo wakikiuka sheria mama au katiba basi wanakuwa wamesababisha madhara makubwa kwa wananchi. Kwa hiyo, waongeze umakini ili kuondoa adha hiyo ya kuathiri wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tumeisema mara nyingi sana. Nimekaa Kamati hii mwaka wa tatu huu nikiwa Mwenyekiti na kila

nikisimama hapa tunasema rekebisha hiki, rekebisha hiki. Wapo wanaorekebisha lakini wapo ambao hawarekebishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru ambao mmerekebisha wengi tu. Mwezi wa pili nilisimama hapa nikatoa Taarifa ya Kamati na moja ya mambo niliyoyasema ni makelele kwenye makazi ya wananchi. Baa zinapiga muziki mpaka asubuhi, kumbi za harusi na sherehe mbalimbali, makanisa na misikiti yanapiga kelele. Baada ya kutoka hapa BASATA na *NEMC* wakachukua hatua, leo shida hiyo imekwisha. Hawa nawapongeza sana kwa kazi nzuri walioifanya lakini wapo wengine ambao hawafanyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninamshukuru sana Waziri Mchengerwa wa TAMISEMI ameshawaambia watendaji kwenye Wizara yake waache kuchukulia yale mambo ya *business as usual,* bora liende, na mazoea. Wajirekebishe na waongeze umakini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wachangiaji kati ya wale kumi na moja tuliowapata wapo ambao wamependekeza. Tatizo hili kubwa inawezekana kwa sababu sheria hizi zinatumika kwanza, kabla ya kuja Bungeni. Mheshimiwa Luhaga Mpina ni mojawapo Mheshimiwa Aida Khenani na wengine. Nafikiri ni hoja ya msingi kwa sababu hizi sheria zinatungwa kule kwenye mamlaka ndogondogo, zinatumika kabla ya kuja hapa kuchambuliwa na zinaadhiri wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni janga kubwa *(disaster)* mtu akionewa na sheria kwa sababu hana pa kwenda, ukimuendea aliyemuonea anakwambia mimi nina sheria bwana, utampeleka wapi? Anaonewa na sheria ambayo ipo imetugwa na ni sheria halali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaelekea kukubaliana na Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Khenani kwamba ni vizuri sheria zije kwanza hapa Bungeni, zipitiwe kwanza kabla ya kutumika ili wananchi wasiathirike. Sheria zije kwanza Bungeni zichambuliwe kwenye Kamati, kamati iongezewe uwezo na muda

ifanye kazi hii kwa umakini zaidi. Inawezekana sio ngumu kwa sababu, hii nchi sio mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii imekaa miaka 60 na kitu ikiwa huru na sheria nyingi zipo. Kwa hiyo, inayokuja ile mara nyingi ina-*replace* sheria mbalimbali au ina-*amend.* Kwa hiyo, ikiwa imekuja hapa ikachelewa kule hawatakosa sheria, hakutakuwa na *vacuum.* Sheria itakuwepo hadi hii tuipitie hapa ikamilike ndiyo iweze kutumika, isitumike kwanza hadi ipite hapa tumalize kuirekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, hoja imeungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji; kwamba Bunge lipokee na kukubali Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja. Pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa pamoja na mapendekezo yake.

*(Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo kuhusu uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye mkutano wa Kumi na Mkutano wa Kumi na Moja. Pamoja na uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa maazimio ya Bunge kuhusu Sheria Ndogo zilizowasilishwa Bungeni kwenye Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa pamoja na mapendekezo yake Ilipitishwa na Bunge)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wote mmeafiki na sasa hii ni Taarifa Rasmi ya Bunge kwenda Serikalini ili iende ikafanyiwe kazi. *(Makofi)*

Nakushukuru sana Mwenyekiti na Kamati yako kwa kazi nzuri ambayo mmeweza kufikia hatua hii. Vilevile tunashukuru Serikali kwa kupokea maoni na kuanza kufanyia kazi mengine kwa mujibu wa mapendekezo kutoka ndani ya Bunge.

Sasa naahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.35 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 6 Septemba, 2023, Saa Tatu Asubuhi)*